Nipashe

Ijumaa Septemba 13, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580022

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper



## Korti yasema Mbowe, vigogo Chadema wana kesi ya kujibu

UKURASA 3



UCHUMI

Wabuni mradi kinamama 'hohehahe' wapewe ujanja na kumiliki magenge
Ukurasa 19

BUFE

Ijumaa Septemba 13, 2019 Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

Uwekezaji, ajira za wazawa zinapokimbizwa na 'umbu-mbu-mbu' vita ya wageni Afrika Kusini
Ukurasa 14

UCHUMI NACHINGWEA MPYA

Machinga walivyojaa uwanja wa nyumbani kusisimua ujasiriamali
Ukurasa 16

UCHUMI Ukurasa 18

Biashara katika picha Ukurasa 17

UKURASA 13

# Maswali magumu kadi za uchaguzi wa S/Mitaa

Hofu uwezekano wa kughushiwa vitambulisho vya chuo na shule...

*Endelea Ukurasa wa 2*



Majeruhi wa ajali ya moto ya Morogoro, Shabani Abdallah (wa pili kulia) na Omary Mikidaki Issa (kulia), wakizungumza na waandishi wa habari, katika Hospitali ya Taifa Muhimbili, jijini Dar es Salaam jana, baada ya kuruhusiwa. Kushoto ni Daktari Bingwa wa Upasuaji, Dk. Edwin Mrema na (wa pili kushoto), ni Mkuu wa Kitengo wa Dharura cha hospitali hiyo, Dk. Juma Mfinanga. **PICHA: MARY GEOFREY**

## Diwani bosi mpya usalama

UKURASA 3

## Afya ya Askofu Mkuu Ruwa'ichi yaimarika

UKURASA 2

**MICHEZO** SIMBA, MTIBWA HAPATOSHI BARA UK.32

MAONI, KATUNI UK.6



Rais John Magufuli akimwapisha Kamishna Diwani Athumani Msuya kuwa Mkurugenzi Mkuu wa Idara ya Usalama wa Taifa, Ikulu, baada ya kumteua jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU.**

# Maswali magumu vitambulisho uchaguzi wa serikali za mitaa

**Na Gwamaka Alipipi**

OFISI ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), juzi ilitoa mwongozo wa uchaguzi wa viongozi wa serikali za vijiji, vitongoji na mitaa ambao unataja vitambulisho vitakavyotumika kupigia kura katika uchaguzi uliopangwa kufanyika Novemba 24, mwaka huu.

Vitambulisho ni pamoja na kadi ya kupigia kura, kitambulisho cha kazi, hati ya kusafiria, kadi ya bima ya afya, kitambulisho cha shule au chuo, mifuko ya hifadhi ya jamii, leseni ya udereva na cha kitambulisho cha taifa.

Sambamba na vitambulisho hivyo, Tamisemi pia ilieleza sifa za mtu anayestahili kugombea katika uchaguzi huo pamoja na muda wa kuanza na kufunga kampeni kwa vyama vitakavyoshiriki.

Mwongozo huo pia ulielezea uandikishaji wa wapigakura, uteuzi wa wasimamizi wa vituo, namna ya kuchukua na kurejesha fomu za

INAENDELEA UK. 8

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA YA WILAYA
KINONDONI
SHAURI LA MADAI NA 121 YA 2019
ACCESS BANK TANZANA LTD.....................................................MDAI
DHIDI YA
SALHA FESAL ISLAM NA WENZAKE..............................MDAIWA

Kwa
SAID MHANDO HUSSEIN
DAR ES SALAAM

KUITWA SHAURINI

Kwa kuwa Mleta maombi ameleta maombi yake ambayo maelezo yake yameelezwa katika nakala za maombi ambazo zinaweza kupatikana katika Mahakama hii, kwa hiyo unahitajiwa kuhudhuria Mahakama hii binafsi au Wakili au Mwakilishi ambaye anaruhusiwa siku ya **Jumatatu Tarehe 7 Mwezi 10 - 2019 Saa 2:00 Asubuhi**

Kwa mujibu wa maombi hayo,na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kutaja shauri hilo ni lazima ulete hati zote zinazohusu shauri hilo kwa ajili ya kujitetea katika shauri hilo

ANGALIZO:
Kama hukuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu na Mahakama ikithibitisha kama umepokea wito wa kuitwa shaurini itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa.

Hati hii imetolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo tarehe 9 **Mwezi 09 Mwaka 2019.**

HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA WILAYA
KINONDONI

RESIDENT MAGISTRATES
KINONDONI DISTRICT COURT
DAR ES SALAAM

215416402

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA YA WILAYA
KINONDONI
SHAURI LA MADAI NA 121 YA 2019
ACCESS BANK TANZANA LTD.....................................................MDAI
DHIDI YA
SALHA FESAL ISLAM NA WENZAKE..............................MDAIWA

Kwa
JAMILA ABEID
DAR ES SALAAM

KUITWA SHAURINI

Kwa kuwa Mleta maombi ameleta maombi yake ambayo maelezo yake yameelezwa katika nakala za maombi ambazo zinaweza kupatikana katika Mahakama hii, kwa hiyo unahitajiwa kuhudhuria Mahakama hii binafsi au Wakili au Mwakilishi ambaye anaruhusiwa siku ya **Jumatatu Tarehe 7 Mwezi 10 - 2019 Saa 2:00 Asubuhi**

Kwa mujibu wa maombi hayo,na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kutaja shauri hilo ni lazima ulete hati zote zinazohusu shauri hilo kwa ajili ya kujitetea katika shauri hilo

ANGALIZO:
Kama hukuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu na Mahakama ikithibitisha kama umepokea wito wa kuitwa shaurini itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa.

Hati hii imetolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo tarehe 9 **Mwezi 09 Mwaka 2019.**

HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA WILAYA
KINONDONI

RESIDENT MAGISTRATES
KINONDONI DISTRICT COURT
DAR ES SALAAM

215416402

# Hali ya Askofu Mkuu Ruwa'ichi yaimarika

**Mary Geofrey**

HALI ya Askofu Mkuu wa Jimbo Kuu Katoliki la Dar es Salaam, Mhashamu Yuda Thadeus Ruwa'ichi, inaendelelea kuimarika, baada ya kufanyiwa upasuaji wa kuondoa damu iliyokuwa imevimbia kwenye ubongo.

Daktari Bingwa wa Upasuaji wa Ubongo, Uti wa Mgongo na Mishipa ya Fahamu wa Tasisi ya Tiba ya Mifupa Muhimbili

INAENDELEA UK. 8

# ...185 kusimamia

**Na Gwamaka Alipipi**

OFISI ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), imetoa orodha ya wasimamizi wa uchaguzi 185 watakaosimamia uchaguzi wa serikali za mitaa unaotarajiwa kufanyika Novemba 24, mwaka huu.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Waziri mwenye dhamana, Selemani Jafo na kuwekwa kwenye tovuti ya wizara hiyo, wasimamizi hao wataapishwa katika mikoa yao.

Taarifa hiyo ilizitaja halmashauri 185 na mikoa 26 watakapokwenda kusimamia uchaguzi huo.

Hata hivyo, orodha hiyo haikuwataja wakurugenzi wa halmashauri kuhusika katika uchaguzi huo, bali iliwataja wakuu wa idara za elimu msingi na sekondari, wakuu wa vitengo vya ukaguzi, wakuu wa idara ya vitengo vya sheria kwamba watahusika katika usimamizi.

Wengine waliotajwa na kupewa dhamana ya kusimamia ni wakuu wa idara za utawala na utumishi, wakuu wa idara za usafi na mazingira, wakuu wa idara za mifugo na uvuvi.

Wengine ni wakuu wa idara za kilimo, umwagiliaji na ushirika, wakuu wa mipango, takwimu na ufuatiliaji, wakuu wa idara za utawala na utumishi, pamoja na wakuu wa vitengo vya nyuki.

Wasimamizi wengine ni wakuu wa idara za maendeleo ya jamii, wakuu wa idara za afya, waweka hazina, wakuu wa vitengo vya ukaguzi wa ndani, wakuu wa idara ya maliasili na utalii, wakuu wa idara za mazingira na udhibiti taka, wakuu wa idara ya ardhi na maliasili, pamoja na maofisa elimu taaluma sekondari.

## HABARI KITAIFA

# JPM amteua bosi Usalama wa Taifa

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS John Magufuli amemteua na kumwapisha Kamishna Diwani Athuman Msuya kuwa Mkurugenzi Mkuu wa Idara ya Usalama wa Taifa.

Taarifa iliyotolewa na Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu, Gerson Msigwa, ilisema uteuzi wa Kamishna Diwani ulianza jana na alishaapishwa, Ikulu jijini Dar es Salaam.

Kabla ya uteuzi huo, Kamishna Diwani alikuwa Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru).

Akizungumza baada ya kumwapisha, Rais Magufuli alimtaka kamishna huyo kuchapa kazi kwa juhudi na maarifa na kwa kuweka mbele maslahi ya taifa.

Kamishna Diwani anachukua nafasi ya Dk. Modestus Kipilimba, ambaye atapangiwa kazi nyingine.



Wanafunzi wa Shule ya Msingi Daimond wakiwa na furaha, baada ya kumaliza mitihani ya taifa ya darasa la saba jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Mbowe, vigogo Chadema wana kesi ya kujibu

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam imesema vigogo tisa wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), akiwamo Mwenyekiti Taifa, Freeman Mbowe, wana kesi ya kujibu dhidi ya mashtaka 13 ya uchochezi yanayowakabili.

Pia imesema washtakiwa hao wataanza kujitetea mfululizo wiki ijayo Septemba 17, 18 na 19, mwaka huu.

Uamuzi huo ulitolewa jana na Hakimu Mkazi Mkuu, Thomas Simba, anayesikiliza kesi hiyo baada ya jopo la mawakili wa upande wa Jamhuri kufunga ushahidi wao.

Upande wa Jamhuri uliongozwa na jopo la Mawakili wa Serikali Wakuu, Dk. Zainabu Mango, Faraja Nchimbi, Wakili wa Serikali Mwandamizi Wankyo Simon na Mawakili wa Serikali Jacqueline Nyantori na Salim Msemo.

Nchimbi alidai kuwa baada ya kuita mashahidi wanane na vielelezo kadhaa, ushahidi wao unatosha kuthibitisha mashtaka 13 dhidi ya washtakiwa hao.

"Mheshimiwa hakimu tunafunga ushahidi wa kesi hii dhidi ya washtakiwa ushahidi wa mashahidi wanane na vielelezo unatosha kuthibitisha kesi ya Jamhuri," alidai Nchimbi.

Hakimu alisema mahakama yake inaushukuru upande wa Jamhuri kwa kuwa haikuwa kazi rahisi na kwamba kwa kuwa wamefunga kesi dhidi ya washtakiwa sasa ni zamu ya upande wa utetezi.

Alisema bila kuacha shaka Mahakama yake imewaona washtakiwa wote wana kesi ya kujibu.

"Washtakiwa wote mna kesi ya kujibu mahakama hii itaanza kusikiliza ushahidi wa utetezi mfululizo Septemba 17, 18 na 19, mwaka huu," alisema Hakimu Simba huku akinyanyuka kwenye kiti chake na kuondoka katika ukumbi namba moja wa mahakama hiyo na kutoka nje.

Mbali ya Mbowe washtakiwa wengine katika kesi hiyo ni Katibu Mkuu Dk. Vincent Mashinji; Mbunge wa Iringa Mjini, Peter Msigwa; Naibu Katibu Mkuu Zanzibar, Salum Mwalimu; Mbunge wa Kibamba, John Mnyika na Mbunge wa Kawe Halima Mdee.

Wengine ni Mbunge wa Tarime Vijijini, John Heche, Mbunge wa Tarime Mjini, Ester Matiko na Mbunge wa Bunda, Ester Bulaya.

Washtakiwa wanakabiliwa na mashtaka 13 likiwamo la kula njama kwa madai kwamba Februari 1 na 16, mwaka jana, jijini Dar es Salaam waliku a njama ya kutenda kosa la kufanya mkusanyiko usio halali na kukiuka tamko la kutawanyika.

# Kabendera adai kusumbuliwa maumivu makali ya mguu

**Na Hellen Mwango**

MWANDISHI wa Habari za Uchunguzi, Erick Kabendera, anayekabiliwa na kesi ya uhujumu uchumi ikiwamo kuongoza genge la uhalifu na kutakatisha fedha wa zaidi ya Sh. milioni 100, amedai mahakamani kuwa anaumwa na kusumbuliwa na maumivu makali zaidi katika mguu wa kulia.

Kadhalika, amedai kuwa pamoja na kupatiwa matibabu ya Jeshi la Magereza, lakini hawana vifaa vya kutosha kumfanyia zaidi vipimo na kuiomba mahakama akatibiwe hospitali yoyote ya serikali.

Madai hayo aliyatoa jana baada ya kuhojiwa na Hakimu Mkazi Mwandamizi, Augustine Rwizile, kama ameshapata huduma ya matibabu katika mahabusu ya Segerea.

Kabendere alidai kuwa wiki mbili zilizopita alipimwa damu na alichomwa sindano tatu kwa sababu alikuwa na maumivu makali yaliisha na kuhusu miguu madaktari walimshauri kuendelea na mazoezi.

"Mheshimiwa hakimu hakuna vifaa vya kufanya vipimo vya kutosha, siku nane zilizopita maumivu ya miguu yalianza tena nilipata maumivu makali mguu wa kulia mifupa inaniuma sana na madaktari wamesema wanaendelea kuniangalia hali yangu inavyoendelea," alidai na kuongeza:

"Jana (juzi), nimeonana na daktari kule Segerea nikamwelezea hali yangu, lakini kwa sababu walikuwa na wageni amenipangia kesho (leo) ataonana na mimi," alidai Kabendera.

Awali, upande wa Jamhuri ukiongozwa na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Wankyo Simon, alidai kuwa kesi hiyo imepangwa kwa ajili ya kutajwa na upelelezi wake bado haujakamilika.

Hata hivyo, wakili wa utetezi, Jebra Kambole, alidai kuwa bado hali ya mshtakiwa ni mbaya, upande wa utetezi unaiomba mahakama kulielekeza Jeshi la Magereza kumpeleka hospitali ya serikali kwa ajili ya kufanyiwa vipimo.

"Sisi mawakili wa utetezi tunaomba mshtakiwa akafanyiwe vipimo sahihi kwenye hospitali yoyote ya serikali ili tufahamu nini kinamsumbua, mahakama ni chombo cha haki hakuna sehemu nyingine tunaweza kukimbilia," alidai Kambole.

Wankyo akijibu hoja za utetezi, alidai kuwa, Magereza wana taratibu zao za matibabu na ikiwa mshtakiwa anastahili rufani wanafanya hivyo kwa mujibu wa taratibu zao za kitabibu.

Hakimu alimhoji Mrakibu Msaidizi wa Magereza (ASP), Muhogo, kuhusu utaratibu wa matibabu.

ASP Muhogo alidai kuwa utaratibu wa madaktari wa Magereza kila siku lazima wanawapitia mahabusu na

INAENDELEA UK. 8


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P 2888,
40470 DODOMA,

Sept 12, 2019

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya Jumatatu Tarehe **16/09/2019** kampuni ya **EFFCO SOLUTION LTD** itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **DAR ES SALAAM** kuelekea **SONGEA NGAKA COAL MINING**, gari hilo lenye namba za usajili:

   **T875CZT/T901 CZT**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| Urefu | - | mita | 19.50 |
| Upana | - | mita | 2.70 |
| Kimo | - | mita | 4.60 |

3. Njia itakayotumika **DAR ES SALAAM mpaka SONGEA Kupitia MASASI**, gari litasafiri muda wa mchana tu **(Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)**

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.**

Mwaka mmoja wa mafanikio DAWASA

DAWASA Dar es Salaam Water & Sewerage Authority

# Ni mwaka mmoja wa mafanikio DAWASA

- Ni baada ya kuunganisha shughuli za DAWASA na DAWASCO
- Miradi 15 yatekelezwa katika maeneo ambayo hayakuwa na maji
- Wananchi lukuki waunganishiwa huduma ya Maji.



Mwenyekiti wa Bodi ya DAWASA Jenerali Mstaafu Davis Mwamunyange akiwa na baadhi ya Wajumbe wa Bodi walipotembelea mradi wa Maji katika Mji wa Mkuranga unaosimamiwa na DAWASA na kuona shughuli za ulazaji wa mabomba na ujenzi wa tanki la Maji lenye ujazo wa lita Milioni 1.5.

**Mwandishi wetu**, Mwananchi

Tunaweza kusema ni Mwaka mmoja wa mafanikio kwa Mamlaka ya Majisafi na Majitaka (DAWASA) tangu kuunganishwa kwa DAWASA kwa DAWASCO. Aidha Menejimenti ya Mamlaka hii ilizinduliwa rasmi Septemba 8, 2018. Ilikuwa ni jambo la busara kuunganisha taasisi hizi mbili ili kuunda Mamlaka kubwa na yenye nguvu miongoni mwa Mamlaka za Maji nchini.

**Nini siri ya mafanikio haya kwa muda mfupi?**

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa DAWASA, Mkuu wa Majeshi Mstaafu Jenerali Davis Mwamunyange anabainisha kuwa siri ya mafanikio yaliyopatikana ndani ya kipindi hiki kifupi ni uongozi IMARA uliokuwa na malengo ya kufikisha huduma kwa wananchi wengi zaidi pamoja na utayari wa watumishi wa Mamlaka katika kutoa huduma bora ya Majisafi na Majitaka.



Waziri wa Maji, Mhe. Profesa Makame Mbarawa (Mb) akisoma mita ya mteja eneo la Sinza jijini Dar es Salaam wakati wa zoezi la usomaji na uhakika na Mita za Maji za wateja wa DAWASA lililofanyika hivi karibuni.

“Katika yote tunajivunia utayari wa watumishi wetu katika kuandaa mipango endelevu na kutekeleza kwa vitendo maagizo ya viongozi katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ya majisafi na majitaka,”alisema Jenerali Mstaafu Mwamunyange.

Mwaka mmoja wa DAWASA mpya kwangu mimi kama Mwenyekiti wa Bodi na wajumbe ndani ya Bodi ninayoiongoza inatupa faraja ya kuona Mamlaka tunayoisimamia inafanya kazi nzuri inayoonekana na wananchi tunaowahudumia.

Katika kipindi cha mwaka mmoja, miradi mingi iliyoleta ahueni kubwa kwa wananchi ndani ya eneo la huduma la DAWASA imetekelezwa. Miradi ipatayo 15 imekwisha kamilika nayo ni pamoja na Mradi wa Maji Tabata Bonyokwa, Tabata Kisukuru, Mradi wa Maji Kiwalani awamu ya pili na ya tatu, Mradi wa Maji Saranga, Kiembeni, Kitopeni, Kilimahewa, Lulanzi, Salasala, Zinga na Mradi wa Maji Zinga Moto. Hivi sasa wananchi katika maeneo hayo wanaendelea kupata huduma.

Vilevile aliainisha Miradi kumi ya maji inayotarajiwa kuanza kutekelezwa hivi karibuni ambayo ni pamoja na Mradi wa Maji Minazi minane, Makurunge awamu ya pili, Mingo awamu ya pili, Mabwepande, Kilindoni, Kidunda, Zegereni, Disunyala, Kibaha Tamco/ Pangani na kazi ya kuweka mtandao wa Maji eneo la Buza.

“Tulipoanza usimamizi wa Bodi hii, Mamlaka ilitenga asilimia 30 ya mapato yake katika utekelezaji wa miradi. Sasa imeongeza kiwango na kutenga asilimia 45 ya mapato yake katika usimamizi na utekelezaji wa Miradi mbalimbali ya majisafi na majitaka itakayoweza kufikisha lengo la asilimia 95 ya upatikanaji majisafi na 30% ya huduma ya majitaka ifikapo 2020,” alimalizia Jenerali Mstaafu Mwamunyange.

Naye Afisa Mtendaji Mkuu wa DAWASA, Mhandisi Cyprian Luhemeja anasema hadi sasa Mamlaka imefanikiwa kusambaza maji safi na salama kwa asilimia 85 jijini Dar es Salaam.

“Zawadi yetu kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe, Dk. John Magufuli hadi kufikia Disemba 9 mwaka huu ni kukamilika mradi wa Maji wa Chalinze- Mboga utakaohudumia wananchi takribani 125,000,” anasema Mhandisi Luhemeja, na kuongeza kuwa katika kipindi hicho ana hakika kuwa mradi wa Kisarawe nao utakuwa umekamilika. Mradi wa Kisarawe ni agizo la Mheshimiwa Rais wakati akizindua mtambo wa Ruvu Juu, Juni 21, 2016.

Mhandisi Luhemeja anabainisha kuwa awali mwaka 2015 Jiji la Dar es Salaam lilikuwa linapata maji kwa asilimia 68 na jumla ya maunganisho ilikuwa 123,000.

“Kwa wakati huo upotevu wa maji ulikuwa asilimia 53 na Shirika la DAWASCO ilikuwa inakusanya kiasi cha Tsh Bil 3.2 kwa mwezi. Leo hii tunapoongea hali ya upatikanaji maji Jijini imepanda hadi asilimia 85 na maunganisho ya maji yameongezeka kutoka 123,000 hadi kufika 326,000. Aidha upotevu wa Maji kwa mwezi Agosti tunapomalizia mwaka mmoja tunaweka rekodi ya kufikia asilimia 39 ya kiwango cha Maji yasiyolipiwa,” anasema Luhemeja. Ameahidi kuwa jitihada hazitaishia hapo hadi pale ambapo huduma zinazotolewa na DAWASA zitakapokuwa kiwango cha kima-

TOLEO MAALUM

# Mwaka mmoja wa mafanikio DAWASA





Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji Prof. Kitila Mkumbo akikagua ujenzi wa tenki la maji lenye ujazo wa lita milioni 6 litakalohudumia Wilaya ya Kisarawe pamoja na maeneo Pugu, Chanika, Majohe na Gongo la Mboto.



Mwenyekiti wa Bodi ya DAWASA Jenerali Mstaafu Davis Mwamunyange akisikiliza maelezo kutoka kwa baadhi ya wajumbe wa bodi hiyo, walipotembelea mradi wa Maji katika Mji wa Mkuranga unaosimamiwa na DAWASA na kuona shughuli za ulazaji wa mabomba na ujenzi wa tanki la Maji lenye ujazo wa lita Milioni 1.5.



Waziri wa Maji Mhe. Prof Makame Mbarawa akisoma mita ya maji katika kiwanda cha saruji Twiga kilichopo eneo la Wazo jijini Dar es Salaam.

taifa.

Aidha, Mhandisi Luhemeja anasema kiwango cha mapato ndani ya mwaka mmoja na kuungana kimekuwa kutoka wastani wa makusanyo ya Sh. Bil 9.2 kwa mwezi hadi sasa wanakusanya wastani wa Sh. Bil. 11.2 kwa mwezi.

"Kwa mwaka wa fedha uliokwisha DAWASA ilikusanya Sh. Bil. 135 sawa na asilimia 95 ya lengo," alisema Mhandisi Luhemeja.

Mhandisi Luhemeja anabainisha kuwa kwa upande wa huduma kwa wateja imefanikiwa kuboresha namna ya ulipaji wa Ankara. "Wateja wetu wanalipia kupitia mtandao, hiyo imewarahisishia wananchi kulipia huduma," alisema na kuongeza kuwa wateja pia wamekuwa wakikumbushwa mara kwa mara njia za malipo ili kuweza kulipa kwa wakati huduma muhimu ya Maji.

Akishukuru wateja wote kwa uaminifu waliouonyesha kwa Mamlaka katika kipindi cha mwaka mmoja Afisa Mtendaji Mkuu aliahidi kuboresha utendaji wa Mamlaka kwa kutumia teknolojia ya kisasa ili huduma iendelee kupungu-za gharama za uendeshaji. "Nichukue fursa hii kusema katika kipindi ambacho serikali ya awamu ya tano inaingia madarakani DAWASA haijapandisha bili ya maji pia niseme DAWASA haina mpango wa kupandisha bili za maji katika kipindi chote cha uongozi wa serikali ya awamu ya tano," anasema Mhandisi Luhemeja.

Mhandisi Luhemeja anasema DAWASA inaendelea na mpango wake wa kuunganisha wateja kwa mkopo ambapo wengi sasa wanajitokeza.

"Nitumie fursa hii kuwajulisha wananchi kwamba maunganisho ya huduma za maji ya DAWASA ni kwa mkopo kwa yeyote anayehitaji kuunganishiwa huduma," alisema na kuwataka wananchi kutoa ripoti kwa vyombo vya dola kwa yeyote atakayekuwa anatoza fedha kwa ajili ya maunganisho.

Katika kuendeleza azma yake ya kuboresha huduma, DAWASA inaendelea kutekeleza Jumla ya miradi 23 ya Majisafi katika Jiji la Dar es Salaam na baadhi ya miji ya Mkoa wa Pwani. Miradi hiyo ni pamoja na Mradi wa Maji Kibamba- Kisarawe, Jet- Buza, Kisarawe- Pugu, Mradi wa Maji Maneromango, Mradi wa Maji Mkuranga, Mradi wa Maji Gezaulole, Tungutung, Kiharaka, Mpiji, Stakishari, Majumba sita, Vingunguti, Kipawa, Sanzale, Ukuni, Ujenzi wa tanki la kuhifadhia Maji mji wa Bagamoyo, Mradi wa Maji Nyakasangwe, Mradi wa Maji Nia njema na Mradi wa ulzaji wa bomba kubwa la Majisafi kutoka Mlandizi hadi Maneromango.

Kwa mujibu wa Mhandisi Luhemeja, miradi mingine mipya 10 inatarajiwa kutekelezwa na lengo ni kwenda kujibu kero za wakazi hao wa Dar es Salaam na Mkoa wa Pwani.

Utekelezaji wa Miradi hii ni ishara na dhamira ya dhati ya Serikali ya Awamu ya Tano chini ya Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania, Dk John Magufuli kuwaondolea wananchi changamoto ya upatikanaji wa huduma ya Majisafi jijini Dar es Salaam na mkoani Pwani.

## UTEKELEZAJI WA MIRADI MIKUBWA YA MAJI

Julai mwaka huu DAWASA walitia saini utekelezaji wa miradi sita mikubwa ya Usambazaji maji katika miji Dar es Salaam na maeneo ya miji ya Pwani.

- Mradi wa Usambazaji Maji kuanza Matanki ya Chuo Kikuu hadi Bagamoyo.
- Mradi wa Bomba la kusafirisha Maji kutoka Jet hadi Buza.
- Mradi wa Kuchimba Visima ishirini (20) Kimbiji na Mpera.
- Mradi wa Usambazaji Maji Kisarawe- Pugu (Gongo la Mboto, Pugu station, Airwing, Ukonga na Majohe)
- Mradi wa Maji katika Mji wa Mkuranga.
- Mradi wa bomba la kusafirisha Maji kutoka Mlandizi (Ruvu Juu) hadi Kijiji cha Mboga (Chalinze).

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Ufisadi miradi 88 maji ni uuaji

**SERIKALI** imegundua kuwa kuna miradi 88 ya maji ambayo aidha kwa uzembe wa viongozi, ubadhirifu na ufisadi miongoni mwa makandarasi na wahandisi haitoi maji.

Taarifa hiyo ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji, Profesa Makame Mbarawa, inatolewa mkoani Dodoma na anataja baadhi ya vijiji kuwa ni miongoni mwa wateja walioathirika.

Wakati Watanzania wakitafakari ripoti hiyo, ikumbukwe kwamba Shirika la Afya Duniani (WHO), linaeleza kuwa kwa sababu ya ukosefu wa maji salama na safi ya kunywa magonjwa mengi ambayo yangezuiliwa kwa kuwapa watu majisafi yanawaua watu.

Maradhi hayo ni kama kuhara, kuharisha damu, kipindupindu, homa ya ini-hepatitis A, taifodi, kichocho na polio ambayo yanabaki kuwa tishio kwa jamii kubwa za watu maskini.

Ukosefu huo wa majisafi unachangia takribani asilimia 4.0 ya vifo duniani, pia ni chanzo cha ulemavu kwani kukosa maji kunachangia kuwapo kwa polio ambayo husababisha asilimia 5.7 ya ulemavu duniani.

Ukweli ni kwamba waliochakachua miradi ya maji wanawakosea Watanzania. Ni kwa sababu wanafahamu kuwa ukosefu wa maji ni chanzo cha maradhi na vifo vya watu wengi hapa nchini kutokana na magonjwa kama hayo.

Waziri anaposema miradi ya maji imechakachuliwa na fedha zimeliwa lakini mabomba hayatoi maji ni jambo la kusikitisha.

Linaumiza kwa sababu Watanzania wengi wanakunywa maji ya madimbwi, malamboni, kwenye visima vifupi vyenye taka za chooni na ya mtoni.

Lakini, hali ni mbaya kwani kuna wanavijiji wengine wanaoshirikiana maji na wanyama pori na wa kufugwa kama mbwa na ng'ombe.

Vyanzo hivyo si salama, lakini wapo wanaojeruhiwa na wanyama wakali kama simba, fisi na chui wanaposaka maji hayo usiku wa manane.

Tunasikitika wakati maelfu wanaumia wapo wanaochakachua miradi ya maji. Makandarasi hawa na viongozi wakumbuke kuwa maji machafu na ukosefu wa huduma hiyo ni chanzo cha magonjwa kama kuhara damu, taifodi, kichocho, macho (usubi), minyoo na homa ya ini.

Makandarasi hawa na viongozi waliochakachua miradi 88 wanabeba hatia ya kuwaua Watanzania tena kwa makusudi iwapo kesi zao zikifikishwa mahakamani.

Wanaofisadi miradi hiyo wakumbuke kuwa fedha nyingi hutumiwa kutibu maradhi ambayo yasingekuwapo kama wangejenga na kukamilisha miradi ya majisafi na salama.

Tunasikitishwa na taarifa hizo ambazo zinazidi kuwaongezea wananchi hali ngumu ya maisha pamoja na maradhi na hata kukatisha maisha yao.

Tunaamini kuwa haya yasingetokea kama makandarasi na viongozi wangekuwa waadilifu na wazalendo wanaothamini utu na afya za watu.

Mara kadhaa zinatolewa taarifa za malalamiko kuwa wagonjwa wanalazimika kulala na ndoo za maji wodini. Wajawazito nao wanatakiwa kwenda na maji wakati wa kujifungua.

Vyoo vya hospitalini, shuleni na hata kwenye sehemu za huduma muhimu za kijamii kama polisi, mahakamani na ofisi za umma wakati mwingine hazina maji, kisa hakuna maji au miradi ya maji haijakamilika.

Tunaamini waliofanya hivyo watashughulikiwa kwa kuwa maji ni uhai na kuyachakachua ni kuwahujumu wananchi.

Pamoja na nia njema ya serikali kuwafikishia maji wananchi kwa asilimia 85 kwa wanaokaa wilayani na asilimia 95 kwa wakazi wa mijini, usalama na usafi wa maji ni muhimu.

Hii ni kwa sababu makandarasi wengine wanachakachua na wakati kwa kupitisha maji kwenye mitaro ya maji taka.


Tunaiomba serikali pamoja na kuwa makini kuzuia uchakachuaji kwenye miradi ya maji suala la usalama liwe kipaumbele.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji:** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
**Idara ya Matangazo:** 0745 700710
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




# Muungwana Lazima Nilonge



Na Beatrice Moses

## Kutochagua ajira kunavyomtoa mtu kutoka mama wa nyumbani

**PENYE** nia pana njia. Ni kauli ya wahenga inayomaanisha kuwa mtu mwenye nia ya kufanya jambo, basi hawezi kushindwa namna ya kuanza kulitenda.

Rais wa Awamu ya Kwanza, Mwalimu Julius Nyerere, alipoutangazia umma jinsi Tanzania ilivyokusudia kuingia kwenye vita vya kumpiga Nduli Idd Amin Dada wa Uganda. Alitumia maneno yenye hamasa aina yake, yaliogeuka chachu kwa majeshi vitani.

"Tunayo kazi moja tu, Watanzania sasa ni kumpiga! Uwezo wa kumpiga tunao, sababu ya kumpiga tunayo, nia ya kumpiga tunayo. Tunataka dunia ituelewe hivyo, kwamba hatuna kazi nyingine." Hiyo ni sehemu ya nukuu aliyosema Mwalimu Nyerere.

Kimsingi, yaliwapa hamasa wapambanaji na kuashilia ushindi. Ndivyo inavyoweza kutokea hata kwenye ulingo wa uchumi. Mapambano dhidi ya umaskini katika jamii unaosababishwa na mengi, ingawa katika sura ya pili, kuna juhudi zinazofanywa kukabili hali hiyo.

Hivi karibuni, vijana kutoka mikoa ya Dar es Salaam na Pwani walikutanishwa na kukubaliana kuyageuza matatizo yatokanayo na sababu mbalimbali, zikiwamo mila, desturi na umaskini wa fikra, wasiishie kulalamika, bali wachukue hatua kuyakabili kusaka ufumbuzi.

Ni mjadala ulioanika matatizo ya jamii, kuwa ni ukosefu wa majisafi na salama, wajawazito kupungukiwa damu, uchafu wa mazingira na ukatili wa kijinsia unaochangiwa na ukosefu wa kipato. Sasa vijana wanajipanga kuigeuza fursa kwao kujiajiri na kuwaajiri wenzao.

Walifikia makubaliano hayo, baada ya kupata semina elekezi ya wiki moja kuhusu ujasiriamali jamii na hamasa katika uwekezaji iliyotolewa na mashirika yasiyokuwa ya kiserikali; Action Aid na Global Platform.

Bila shaka kuna msamiati maarufu 'golikipa' katika nyanja ya mchezo wa soka inamaanisha mlinda mlango, kwa namna nyingine ya lugha kupanuka inatumika vibaya katika jamii kumdhalilisha mwanamke, ambaye ni mama wa nyumbani.

Mary Daniel, anasema wameamua kupata suluhisho linalokomesha matumizi mabaya ya neno hilo kuhakikisha wanawajengea uwezo wa kiuchumi ndani ya familia, kinamama ambao wanaojishughulisha na kazi za nyumbani.

Anabainisha baada ya kushuhudia hali hiyo aliamua kumsaidia shangazi yake kujihusisha na ufugaji wa sungura ambao hauhitaji mtaji mkubwa hatimaye baada ya miezi kadhaa akaanza kujipatia fedha kwa kuuza wanyama hao na mkojo wao.

George Bundi anasema wamebaini tabia ya kuchagua kazi inawanyima fursa za kipato, hivyo wamejipanga kuhakikisha matatizo yanayoikabili jamii wanayatumia kujiajiri.

Anatoa mfano, shughuli ya usafishaji mazingira, uzoaji wa taka ambao vijana wanakwepa kuzifanya, baadhi wakiamini ni maalum kwa wanawake (kinamama).

Anasema zabuni zimekuwa zikitangazwa katika maeneo tofauti nchini, lakini vijana wanakwenda kwenda kushiriki, wengine wakihofia kuchekwa, licha ya kwamba ni shughuli ambayo inaweza kusaidia mtu kuwa na kipato cha uhakika.

Shauri Yombayomba akizungumzia tatizo la ukosefu wa damu ambalo limekuwa likiwakumba baadhi ya wajawazito na kuhatarisha maisha yao linaweza kugeuzwa kuwa fursa ya ajira kwa vijana.

Meneja Programu wa Shirika lisilokuwa la kiserikali la Youth Partnership Countrywide (YPC) la Kibaha Jane ambalo limeandaa semina hiyo alibainisha kuwa imewasaidia vijana walioshiriki kubadili fikra zao na kuona frusa za uwekezaji kwenye matatizo yanayoikabili jamii.

"Kumekuwa na changamoto kadhaa zinazosumbua kwenye jamii, vijana wamefuzwa kuzitambua na kuzitumia kama fursa za ajira kwa kutokusubiri kuajiriwa au kushinda kulalamikia hali hiyo badala yake wazigeuze kuwa vitega uchumi vyao vitakavyowawezesha kupata kipato," anasema Mulungi.

Anasema fursa hizo zipo kwenye kilimo, biashara, mazingira, masuala ya kijinsia, ambapo vijana hao wameahidi kuzitumia vyema pamoja na kuhakikisha wanaelimisha wengine kujiunga nao ili kuleta chachu katika jamii.

Mwezeshaji Teresiah Warui wa Action Aid kutoka Kenya anasema kuwa vijana wakibadili fikra wanaweza kunufaika kupitia ujasiriamali jamii na kujitengenezea kipato chenye uhakika.

## HABARI KITAIFA

# Mbunge mwingine wa CCM aomba radhi, Spika awapongeza

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

MBUNGE wa Kigoma Kaskazini, Peter Serukamba (CCM), ameuomba radhi uongozi wa chama hicho kutokana na kauli yake kuhusu ujamaa ndani ya chama hicho aliyoitoa bungeni Juni mwaka huu.

Serukamba aliomba msamaha huo bungeni jijini Dodoma jana, wakati Bunge likieleza kuwa maneno yake kuhusu 'ujamaa' yalitafsiriwa kwa dhana tofauti na aliyokuwa amekusudia siku hiyo.

Alisema kwa kutambua hilo, anauomba radhi uongozi wa chama kwa kutoa lugha hiyo katika mazingira ambayo hakupaswa kuitumia.

Katika hatua nyingine, Spika wa Bunge, Job Ndugai, amewapongeza wabunge watatu wa CCM, Nape Nnauye (Mtama), William Ngeleja (Sengerema) na January Makamba (Bumbuli) kwa kumwomba radhi Rais John Magufuli kutokana na makosa waliyoyafanya dhidi ya kiongozi huyo wa nchi.

Alisema kwa kuwa Rais Magufuli ameridhia kuwasamehe wabunge hao, ni nafasi nzuri kwao kujipanga kuanza upya.

Alisema kuomba msamaha ni jambo gumu, lakini kibinadamu ni jambo jema unapobaini umekosea.

Spika Ndugai alitoa kauli hiyo bungeni jana, akieleza kuwa wabunge hao wameonyesha uungwana na wanapaswa kuigwa na wabunge wengine wanapobaini kumkwaza mtu yeyote.

"Kama kiongozi wa Bunge, ninawapongeza kwa hatua hiyo kwa kuwa mmefanya jambo ambalo mmeona kabisa kibinadamu mlikosea," alisema.



Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo Taifa (Chadema), Freeman Mbowe na viongozi wenzake, wakitoka kizimbani katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam jana, baada ya kuonekana wana kesi ya kujibu dhidi ya mashtaka 13 ya uchochezi yanayowakabili. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Majeruhi watatu moto gari mafuta waruhusiwa

**Na Mary Geofrey**

MAJERUHI watatu kati ya 11 wa ajali ya moto wanaoendelea kupatiwa matibabu Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) wameruhusiwa kutoka baada ya afya zao kuanza kuimarika.

Kati ya majeruhi 47 waliofikishwa hospitalini hapo kuanzia Agosti 11, mwaka huu, 36 walifariki dunia na kubakia 11 ambao kati yao watatu wameruhusiwa jana na mmoja akiwa katika chumba cha uangalizi maalum (ICU).

Daktari Bingwa wa Upasuaji wa MNH, Dk. Edwin Mrema, alisema jana jijini Dar es Salaam, alisema kuwa majeruhi hao wameruhusiwa baada ya afya zao kuanza kuimarika.

Alisema licha ya wagonjwa hao kuruhusiwa wataendelea kuhudhuria kliniki ya wagonjwa wa nje ili kufuatilia maendeleo ya afya zao.

"Hadi kufikia leo (jana) tuna wagonjwa 11 miongoni mwao ni hawa wawili na mmoja ataruhusiwa kesho, hawa wagonjwa tulipokea wakiwa katika hali ya hatari zaidi lakini leo (jana) tumefikia hatua ya kuwaruhusu kwenda nyumbani," alisema Dk. Mrema ambaye ni mtaalamu wa kutibu majeraha ya moto.

Alisema hatari walizokuwa nazo zimeisha na sehemu kubwa ya vidonda walivyokuwa navyo vimepona, upumuaji wao ni mzuri na afya zao kwa ujumla zinaruhusu ingawa wataendelea kuhudhuria kliniki ya nje hospitalini hapo.

Aidha, mgonjwa mmoja amekatwa miguu yote kutokana na kupata madhara makubwa ambayo wataalamu hao wameona wangeiacha ingeendelea kuleta shida kwenye mwili wake.

"Wagonjwa wawili ambao waliungua vibaya ilibidi kuwafanyia upasuaji kuondoa baadhi ya viungo na mmoja tulimkata miguu yote miwili ili kuokoa maisha yake na sasa yupo katika chumba cha uangalizi maalum (ICU) na hali yake inaendelea vizuri," Dk. Mrema alisema.

Alisema pia wagonjwa wanane waliosalia wataendelea kuhudhuria kliniki ya saikolojia ili kuwaimarisha zaidi kifikra.

Dk. Mrema alisema wagonjwa wameanza kupatiwa huduma za mazoezi ya viungo kwa sababu majeraha ya moto walioyapata yanaweza kusababisha baadhi ya viungo visikae sawa.

Mmoja wa majeruhi aliyeruhusiwa, Shabani Omary, alimshukuru Rais John Magufuli, kwa kuwatembelea pamoja na kuwagharamia gharama zote za matibabu.

# SSRA yafyekwa

**Na Sanula Athanas, DODOMA**

BUNGE limepitisha Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 6 wa Mwaka 2019, ambao pamoja na mambo mengine, upendekeza kuifuta Mamlaka ya Usimamizi wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii (SSRA).

Muswada huo pia unapendekeza kuweka adhabu kali dhidi ya watu wanaotumia au kusambaza picha za maiti au waathirika wa ajali.

Akiwasilisha muswada huo unaopendekeza marekebisho katika sheria tisa, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Prof. Adelardus Kilangi, alisema mabadiliko hayo yanahusisha Sheria ya Kanuni za Adhabu, Sura ya 16 iliyotungwa mwaka 1930 kwa lengo la kuainisha adhabu kwa makosa mbalimbali.

Alisema tangu kutungwa kwa sheria hiyo, imerekebishwa mara 67 kupitia sheria mbalimbali na marekebisho ya sasa yanalenga kuongeza adhabu ya faini kwa makosa chini ya kifungu cha 29 ili kuondoa adhabu zilizopitwa na wakati kutokana na hali ilivyo sasa.

"Kifungu kipya cha 162 kinapendekezwa kuongezwa ili kutoa adhabu kwa watu wanaotumia na kusambaza picha au video za maiti, waathirika wa majanga na matukio ya kutisha yanayohatarisha amani au kuingilia utu wa mtu," alisema.

Alisema katika muswada aliouwasilisha jana, marekebisho yanalenga kuifuta SSRA na kuhamisha jukumu ka usimamizi wa sekta ya hifadhi ya jamii kwenda kwenye divisheni inayowajibika kwa masuala ya hifadhi ya jamii.

Prof. Kilangi alisema eneo la usimamizi wa masuala ya fedha na uwekezaji wa mifuko litaendelea chini ya uangalizi wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT) kama ilivyo sasa.


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA YA WILAYA
KINONDONI
SHAURI LA MADAI NA 121 YA 2019
ACCESS BANK TANZANIA LTD..........................................................MDAI
DHIDI YA
SALHA FESAL ISLAM NA WENZAKE.................................MDAIWA

Kwa
SALHA FESAL ISLAM
DAR ES SALAAM

KUITWA SHAURINI

Kwa kuwa Mleta maombi ameleta maombi yake ambayo maelezo yake yameelezwa katika nakala za maombi ambazo zinaweza kupatikana katika Mahakama hii, kwa hiyo unahitajiwa kuhudhuria Mahakama hii binafsi au Wakili au Mwakilishi ambaye anaruhusiwa siku ya **Jumatatu Tarehe 7 Mwezi 10 - 2019 Saa 2:00 Asubuhi**

Kwa mujibu wa maombi hayo,na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kutaja shauri hilo ni lazima ulete hati zote zinazohusu shauri hilo kwa ajili ya kujitetea katika shauri hilo

**ANGALIZO:**
Kama hukuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu na Mahakama ikithibitisha kama umepokea wito wa kuitwa shaurini itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa.

Hati hii imetolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo tarehe **9 Mwezi 09 Mwaka 2019.**

HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA WILAYA
KINONDONI

RESIDENT MAGISTRATES
KINONDONI DISTRICT COURT
DAR ES SALAAM

215416402



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA YA WILAYA
KINONDONI
SHAURI LA MADAI NA 121 YA 2019
ACCESS BANK TANZANIA LTD..........................................................MDAI
DHIDI YA
SALHA FESAL ISLAM NA WENZAKE.................................MDAIWA

Kwa
MWANAHAMIS HASHIM NGOPELA
DAR ES SALAAM

KUITWA SHAURINI

Kwa kuwa Mleta maombi ameleta maombi yake ambayo maelezo yake yameelezwa katika nakala za maombi ambazo zinaweza kupatikana katika Mahakama hii, kwa hiyo unahitajiwa kuhudhuria Mahakama hii binafsi au Wakili au Mwakilishi ambaye anaruhusiwa siku ya **Jumatatu Tarehe 7 Mwezi 10 - 2019 Saa 2:00 Asubuhi**

Kwa mujibu wa maombi hayo,na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kutaja shauri hilo ni lazima ulete hati zote zinazohusu shauri hilo kwa ajili ya kujitetea katika shauri hilo

**ANGALIZO:**
Kama hukuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu na Mahakama ikithibitisha kama umepokea wito wa kuitwa shaurini itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa.

Hati hii imetolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo tarehe **9 Mwezi 09 Mwaka 2019.**

HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA WILAYA
KINONDONI

RESIDENT MAGISTRATES
KINONDONI DISTRICT COURT
DAR ES SALAAM

215416402

HABARI KITAIFA

# Maswali magumu vitambulisho uchaguzi wa serikali za mitaa

INATOKA UK. 2

wagombea utakavyofanyika.

Hayo yote ni mambo muhimu katika mchakato wowote wa uchaguzi kwa sababu shughuli hiyo katika muktadha wa kidemokrasia lazima kuwapo na sheria, kanuni na taratibu zinazoongoza.

**MASWALI MAGUMU**

Pamoja na kutangazwa kwa utaratibu huo, jambo ambalo limezua gumzo na maswali magumu kwa wadau wa uchaguzi wakiwamo wafuatiliaji wa masuala ya siasa ni matumizi ya vitambulisho vinane kwenye uchaguzi huo.

Inaeleweka kabisa kwamba ili uchaguzi ufanyikwe kwa misingi ya uhuru na haki, ni lazima kufanyike uandikishaji wa wapigakura ambao hupewa vitambulisho au stakabadhi maalum kama ilivyokuwa zamani kabla ya kuanza kwa mfumo wa daftari la kudumu la kupiga kura.

Kupitia mfumo huo, kwa sasa wananchi walioandikishwa wanapewa vitambulisho vya kupigia kura. Lakini jambo la kustaajabisha ni kwa nini kuwe na matumizi ya vitambulisho vyote hivyo badala ya kile kinachostahili, yaani kadi ya kupigia kura inayotambulika?

**UHALALI WA VITAMBULISHO**

Miongoni mwa vitambulisho vilivyotajwa kwamba vitatumika kupigia kura, hivi sasa havitambuliki katika taasisi yoyote kutokana na uwezekano mkubwa wa kughushiwa. Baadhi ya vitambulisho hivyo ni vya shule au chuo.

Vitambulisho hivyo vinaweza kutengenezwa hata katika ofisi yoyote ya uchapaji nyaraka (stationary). Kutokana na ukweli huo, swali la kujiuliza ni je, mhusika wa vitambulisho kama hivyo atajulikanaje kuwa ndiye mwenyewe?

Kuwapo kwa vitambulisho hivyo, kunatoa mwanya mkubwa wa kukosekana kwa uchaguzi ulio huru na wa haki.

Swali lingine ambalo linaibua ukakasi katika mchakato huo kutokana na tangazo la Tamisemi ni, je, wasimamizi wa uchaguzi watawezaje kugundua vitambulisho ambavyo ni rahisi kughushiwa kama vile kitambulisho cha shule au chuo?

Kwa mantiki hiyo, suala hili linawaweka pia wasimamizi katika wakati mgumu kusimamia uchaguzi kwa misingi ya uhuru na haki na pia uwezo wa kutambua uhalali wa vitambulisho hivyo.

Katika zama za sasa za sayansi na teknolojia, ni rahisi kwa vitambulisho feki kutengenezwa na kuzagaa mitaani. Nafasi hiyo inaweza kutumika kwa watu kujitengenezea vitambulisho kuwa ni wafanyakazi wa taasisi mbalimbali wakati ni uongo.

**UHALALI WA MPIGAKURA**

Kama ilivyoelezwa juu ya aina ya vitambulisho kama cha kazi, chuo au shule, inawezekanaje kubaini kuwa mpigakura husika ni raia halali wa Tanzania au anaishi eneo husika?

Kutokana na ukweli huo, kuna uwezekano mkubwa wa mamluki wa chama fulani kuingizwa kupiga kura hata bila kuwa na uhalali wa kushiriki mchakato huo wa kuwapata viongozi ambao ni chimbuko la maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

Kinadharia, serikali za mitaa ndilo chimbuko la demokrasia, utawala bora na maendeleo ya kijamii na kiuchumi kwa sababu hapo ndiyo maeneo ambayo watu hupanga na kutekeleza mipango yao.

Lakini kuwapo kwa mkanganyiko wa vitambulisho vya kupigia kura, kuna uwezekano mkubwa, kwanza, wapigakura wa sehemu husika kutokuwa halali, na pili, mgombea wa nafasi husika kupandikizwa na chama husika kwa maslahi yake.

**UTATA DAFTARI**

Katika miezi kadhaa iliyopita, kulitolewa taarifa kwamba daftari la kudumu la wapigakura, lingehuishwa kwa ajili ya kutumika katika uchaguzi wa serikali za mitaa.

Swali linaloibuka hapa ni kwa nini hadi sasa mamlaka husika ziko kimya katika suala hili? Itajulikanaje kuwa wahusika watakaopiga kura kwa kutumia vitambulisho vinane ni wakazi wa eneo husika.

Kwa nini hakukuwapo na uharakishwaji wa uhakiki wa daftari la kupigia kura? Je, uwapo wa vitambulisho vingi hautaleta mkanganyiko kwa wahusika ambao wana zaidi ya kimoja?

**UTAMBUZI WAKAZI**

Je, wakazi wa eneo husika wanafahamiana? Kwa sababu sehemu ya mwongozo huo unaeleza kuwa:

Mwongozo uliotolewa unaeleza kuwa endapo mpigakura atakuwa hana kitambulisho cha aina yoyote kilichotajwa katika kanuni za uchaguzi, lakini jina lake limo kwenye orodha ya wapigakura iliyoandaliwa kwa mujibu wa kanuni za uchaguzi, msimamizi msaidizi wa uchaguzi atamruhusu mtu huyo kupiga kura baada ya kutambuliwa na wakazi wa eneo husika.

Kutokana na mwongozo huo, yako maswali kadhaa ya kujiuliza. Kwanza, itafahamikaje kwamba mtu huyo ndiye mwenye jina halisi? Jambo hili linaweza kusababisha mkanganyiko hasa kwa wale wenye majina kama 'John Stephen' au 'Said Hamisi'.

Pili katika baadhi ya maeneo hasa mijini baadhi ya watu hawafahamiani licha ya kupakana milango au mageti. Wengine wakiondoka asubuhi kwenda kwenye shughuli zao hurejea usiku nyumbani. Watu hao wanaweza kutambulikaje kuwa ndio wakazi halisi wa eneo husika? Maswali haya ndiyo yanaibua wasiwasi mkubwa wa kufanyika kwa uchaguzi wa serikali za mitaa ulio huru na haki.


BONITE BOTTLERS LIMITED

## Advertisements of Employment

### 1. Salesman

**Qualification:**

- Applicant should be a holder of form IV/VI with Diploma in Sales and Marketing / Business Administration or any related field from recognized Institution.

**Key skills & Abilities:**

- Skills and knowledge of customer care and customer services.
- Ability and skills of route sales.
- Ability to forecast sales / load to be taken for each day to the location assigned.
- Able to work independently with minimum supervision.
- Self motivated, flexible person and a good team player.
- Ability to seek out and develop news business and maximize all possible opportunities to increase Sales.

√ **Experience** : Any experience in the same related field will be an added advantage.

**Mode of Application:**

All applications accompanied with cover letter, photocopies of certificates and CVs to be sent to undersigned address, reach him not later than 21/09/2019.

**The Managing Director,**
**Bonite Bottlers Ltd,**
**P. O. Box 1352,**
**MOSHI.**

21416602


# Hali ya Askofu Mkuu Ruwa'ichi yaimarika

INATOKA UK. 2

(MOI), Prof. Joseph Kahamba, akizungumza na Nipashe jana kwa njia ya simu, alisema Mhashamu Askofu Mkuu Ruwa'ichi ameanza kujitambua na kufanyiwa mazoezi.

"Mhashamu Askofu Ruwa'ichi hali yake inaendelea vizuri sana, tumeanza kumfanyia mazoezi ya kukaa, pia anaweza kula peke yake ingawa bado yupo chumba cha uangalizi maalum kumtoa sasa hivi bado ni mapema mno," Prof. Kahamba alisema.

Ofisa Uhusiano wa MOI, Patrick Mvungi, aliongezea kusema kuwa Mhashamu Askofu Ruwa'ichi hategemei msaada wowote wa mashine na anaweza kufuata maelekezo ya madaktari, kuongea na kula mwenyewe.

Mhashamu Askofu Ruwa'ichi alifanyiwa upasuaji wa kuondoa damu iliyovimbia kwenye ubongo, usiku wa kuamkia Septemba 10, baada ya kubainika kuwa ni ugonjwa ambao kwa kitaalamu unaitwa 'Chronic Subdural Haematoma'.

Awali alilazwa Hospitali ya Rufani ya KCMC mkoani Kilimanjaro ambako alifanyiwa upasuaji ambao haukusaidia kutibu tatizo lililokuwa linamkabili.

Mhashamu Mkuu Askofu Ruwa'ichi alisafirishwa kwa ndege usiku wa manane akitokea KCMC hadi MOI ambako walimpokea na kufanyiwa upasuaji usiku huo huo.

Daktari huyo anayemuhudumia, Prof. Kahamba, alisema upasuaji huo uliochukua saa nne chini ya madaktari bingwa watatu, na kwamba hali yake inazidi kuimarika.

# Kabendera adai kusumbuliwa maumivu makali ya mguu

INATOKA UK.3

kuwasikiliza shida zao.

"Mheshimiwa hakimu madaktari wanapoona mshtakiwa anastahili rufani wanamrufani kwenda hospitali ya juu," alidai ASP Muhogo.

Hakimu Rwizile baada ya kusikiliza hoja zote alisema kwa sababu mshtakiwa ana ahadi ya kuonana na daktari leo, anapanga kesi hiyo tarehe fupi.

"Mshtakiwa nenda kaonane na daktari kesho (leo), naipanga kesi yako Jumatano ijayo Septamba 18, mwaka huu uje na taarifa za daktari huyo," alisema Hakimu Rwizile.

Katika kesi ya msingi, Kabendera anadaiwa katika siku tofauti kati ya Januari 2015 na Julai 2019, katika maeneo tofauti jijini Dar es Salaam, alitoa msaada katika genge la uhalifu kwa nia ya kujipatia faida.

Pia anadaiwa bila kuwa na sababu za msingi kisheria alishindwa kulipa kodi ya Sh. 173, 247,047.02 ambayo ilitakiwa ilipwe kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA)

Shtaka la tatu anadaiwa alijipatia Sh. milioni 173.2 wakati akijua kuwa fedha hizo ni za kutakatisha na zao la makosa tangulizi ya kukwepa kodi na kujihusisha na genge la uhalifu.

HABARI MIKOANI

# Miaka 20 jela kwa kukutwa na jino la simba

Na Hamisi Nasiri, MASASI

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Mfawidhi Wilaya ya Masasi, mkoani Mtwara imemhukumu Mussa Daudi (47), Mkazi wa Mkoa wa Mwanza kifungo cha miaka 20 jela kwa tuhuma za kukutwa na kipande cha jino moja la simba lenye thamani ya Sh. milioni 10.9

Akisoma hukumu ya shtaka hilo jana, Hakimu Mfawidhi wa mahakama hiyo, Batista Kashusha, alidai mshtakiwa alikuwa anakabiliwa na kosa la uhujumu uchumi kwa kukutwa na jino moja la simba lenye thamani ya Sh. milioni 10. 9 ambalo ni nyara ya serikali.

Hakimu Kashusha alidai mahakamani hapo kuwa kesi hiyo namba saba ya mwaka 2018 ya uhujumu uchumi ilifunguliwa na Jamhuri.

Alisema mshtakiwa alitiwa hatiani kwa kukutwa na nyara ya serikali Oktoba 9, 2018 majira ya asubuhi katika Wilaya ya Masasi mkoani Mtwara maeneo ya stendi kuu ya mabasi na polisi wa kiintelijensia.

Hakimu Kashusha aliendelea kueleza kuwa baada ya mtuhumiwa kufikishwa Kituo cha Polisi Wilaya ya Masasi na kumfanyia upekuzi, walimkuta akiwa na jino hilo lililodhaniwa kuwa ni la mnyama mkali anayekula wanyama wenzake likiwa ndani ya pochi yake ya kuhifadhia hela.

Kashusha alisema polisi kwa kushirikiana na maofisa wa wanyamapori walifanyia uchunguzi jino hilo, ndipo maofisa hao walipobaini kuwa ni la mnyama aina ya simba na kwamba thamani yake ni Sh. milioni 10.9 na mtuhumiwa kukutwa na hatia ya uhujumu uchumi na kuhukumiwa kwenda jela miaka 20.

Alisema upande wa mashtaka, ulieleza mshtakiwa huyo kupitia jino hilo la simba pia alikuwa na tabia ya kuwatapeli wananchi wa Wilaya ya Masasi hasa wakulima wa zao la korosho kupitia imani mbalimbali za kishirikina kwa kutumia jino hilo.

Hakimu Kashusha alisema upande wa mashtaka ambao ni Jamhuri baada ya kuthibitisha shtaka hilo imeridhika na ushahidi ulitolewa.

Kashusha alieleza kuwa kupitia Sheria ya Wanyamapori Namba 5 ya Mwaka 2009 imeridhishwa na shtaka hilo la uhujumu uchumi.

Mwendesha Mashtaka wa Serikali Edwin John, aliiomba mahakama kutoa adhabu kali kwa mtuhumiwa kwa sababu kosa lake la uhujumu uchumi ni kubwa na kwamba linahusisha uuaji wa wanyama ambao ni nyara ya serikali na kwamba serikali kwa sasa ina vita dhidi ya watu wanawaua wanyamapori maliasili ya nchi.

Mshtakiwa alipotakiwa kujitetea, aliiomba mahakama impunguzie adhabu kwa vile ana familia ya watoto wanne na mke mmoja ambao wanamtegemea.



Mfanyabiashara wa mito akitafuta wateja kandokando ya barabara kuu ya Masasi-Newala, katika mtaa wa Wapiwapi A wilayani Masasi, mkoani Mtwara jana. **PICHA: HAMISI NASIRI**.

# Watumishi 46 kufukuzwa kazi kwa vyeti feki

Na Ndalike Sonda, KAHAMA

BARAZA la Halmashauri ya Msalala wilayani Kahama, mkoani Shinyanga limeridhia kuwafukuza kazi watumishi 46 wa kada mbalimbali katika halmashauri hiyo baada ya kubainika kuwa wameghushi vyeti katika kupata ajira.

Akizungumza na waandishi wa habari jana muda mfupi baada ya kumalizika kikao cha baraza hilo, Mwenyekiti wa halmashauri hiyo, Mibako Mabubu, alisema watumishi hao ni kutoka kada ya afya, maji na utawala.

Mabubu alisema kuwa baraza limeelekeza watumishi hao wasitishiwe ajira zao mara moja na kwamba mchakato huo umefanyika baada ya kamati ya maadili kuwabaini watumishi hao kuwa wamefanya udanganyifu kwa kughushi vyeti ili kupata ajira.

Mabubu alisema kutokana na kuwafuta kazi watumishi hao, halmashauri hiyo imekwisha kuandika barua kwenye Ofisi ya Wiziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, (Tamisemi) na Wizara ya Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora, ambapo tayari kwenye kada ya utawala serikali imekwisha kuongeza watumishi.

Wakati huo huo, Mkurugenzi Mtendaji wa halmashauri hiyo, Simon Berege, aliliambia baraza hilo kuwa halmashauri hiyo imejipanga kuanzisha bustani kubwa ya miti kwa ajili ya kusambaza miti katika maeneo mbalimbali ya halmashauri hiyo.

"Tunaanzisha bustani kubwa katika halmashauri yetu na tutaifanyia pale kwenye eneo la makao makuu ya halmashauri na tayari tumempata mdau mmoja ambaye alikuwa anasambaza miti kwenye halmashauri zingine tutakuwa naye kwa ajili ya kufanikisha hilo lengo ni kuhamasisha upandaji wa miti kwa wananchi," alisema Berege.

# Wazazi watakaorubuni watoto kufeli kukiona

Na Shaban Njia, KAHAMA

SERIKALI wilayani Kahama, imesema itawachukulia hatua za kisheria wazazi wote watakaobainika kuwarubuni watoto wao kutofanya vizuri kwenye mitihani yao ya mwisho kwa kisingizio cha kukosa fedha za kuwasomesha.

Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Anamringi Macha, aliyasema hayo jana kwenye kikao cha Baraza la Madiwani cha Halmashauri ya Msalala, robo ya nne ya kumaliza mwaka wa fedha wa 2018/19 na kusema kila diwani anatakiwa kuwa balozi wa suala hilo.

Alisema wazazi wamekuwa chanzo cha kusababisha wanafunzi wengi kutofanya vizuri katika mitihani yao ya mwisho kwa kuwataka kuandika majibu ambayo sio sahihi kwa kisingizio cha kutokuwa na fedha za kumsomesha.

Alisema kuwa, kwa mwanafunzi wa darasa la saba atakayeshindwa kufaulu mtihani wake wa mwisho, atalazimika kufuatilia mwenendo wake wa masomo shuleni na ikigundulika alikuwa anafanye vizuri, atakamatwa mzazi ajieleze.

"Serikali haiwezi kutekeleza wajibu wake wa kusomesha watoto bure, huku mzazi naye anamtaka mwanawe asifanye vyema kwenye mtihani wake wa mwisho, na hili limekuwa likijitokeza mara kwa mara na asilimia kubwa wanaofanya hivyo huwa ni wanafunzi wa kike," alisema Macha.

Hata hivyo, alisema Wilaya ya Kahama ina zaidi ya watahiniwa 16,000 huku Halmashauri ya Msalala ikiwa na watahiniwa 4,000 na kuwataka madiwani kuhakikisha wanawahamasisha wananchi kujenga vyumba vya madarasa ili wanafunzi watakaofaulu wapate mahala pakukaa.

Katika hatua nyingine Macha, aliwataka madiwani wa halmashauri hiyo kuhakikisha wanawahamasisha wananchi kujiunga na Mfuko wa Bima ya Afya iliyoboreshwa (CHF) ili kupambana na gharama za matibabu, wanapofika katika vituo vya afya kupatiwa matibabu.

Alisema mtu anapojiunga na CHF kwa Sh. 30,000 kwa mwaka mmoja anaweza kupata huduma za kiafya yeye pamoja na watu sita tegemezi kwenye familia na gharama za matibabu zitakuwa ndogo anapotakiwa kununua dawa nje.

Diwani wa Kata ya Mwalugulu, Flora Sagasaga, alisema lugha chafu zinazotolewa na baadhi ya wauguzi katika hospitali, vituo vya afya na zahanati ndio sababu ya wananchi kushindwa kujiunga na CHF.

Alisema wagonjwa wengi wanaposikia kauli hiyo hukatishwa tamaa ya kukata bima, kwa kuwa imekuwa ikiwaletea usumbufu kupata huduma za matibabu.

# FBME hatua za mwisho ufilisi

BUNGE limeelezwa kuwa kwa sasa benki ya FBME iko katika hatua za ufilisi, hivyo haiendeshi shughuli zozote za kibenki nchini.

Aidha, hadi Septemba 9, mwaka huu, jumla ya Sh. milioni 2,404.2 zimelipwa kwa wateja 3,426 kama fidia ya bima ya amana.

Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Ashatu Kijaji, alisema hayo jana bungeni jijini hapa alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Baraza la Wawakilishi (CCM), Jaku Hashim Ayub.

Katika swali lake, Mbunge huyo alihoji ni lini benki hiyo italipa wateja amana zao zilizokuwapo kwenye benki hiyo.

"Je, benki iko katika hali gani sasa? Na je, Benki Kuu ya Tanzania ina dhamana gani katika kulinda benki?" Alihoji.

Akijibu maswali hayo, Naibu Waziri huyo alisema kiasi hicho cha fedha ni sawa na asilimia 55.9 ya kiasi chote kilichotarajiwa kulipwa kama fidia ya bima ya amana kwa wateja wote 6,628 walioko Tanzania pamoja na walioko nje ya Tanzania.

"Aidha, jumla ya Sh. milioni 2,401.2 zimelipwa ikiwa ni asilimia 83.3 ya lengo la kulipa Sh. milioni 2,882.6 kwa wateja walioko Tanzania tu," alisema.

Hata hivyo, alisema wateja waliokuwa na amana zaidi ya Sh. milioni 1.5 watalipwa kiasi kilichobaki kwa mujibu wa sheria na taratibu za ufilisi.

"Kiasi kitakacholipwa kwa wenye amana zaidi ya Sh. milioni 1.5 kitategemea fedha zitakazopatikana kutokana na mauzo ya mali za benki pamoja na ukusanyaji wa madeni kutoka kwa wadaiwa wa benki hiyo," alisema.

Awali, alisema benki hiyo ilifutiwa leseni ya kufanya biashara Tanzania na Benki Kuu ya Tanzania (BoT) tangu Mei 8, 2017 kwa tuhuma za kujihusisha na utakatishaji fedha nchini Marekani.

"Pia BoT iliteua Bodi ya Bima ya Amana kuwa mfilisi wa benki hiyo katika kutimiza wajibu wake wa msingi. Bodi ya Bima ya Amana ilianza kulipa fidia kwa mujibu wa sheria kwa waliokuwa na amana katika benki hiyo kuanzia Novemba, 2017 na bado kazi inaendelea.

Kadhalika, alisema Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006 imeipa BoT mamlaka ya kutoa leseni, kutunga kanuni, kusimamia benki zote zinazochukua amana za wateja na kuchukua hatua za kisheria dhidi ya benki zinazoendesha biashara bila kuzingatia sheria, kanuni, taratibu na miongozo iliyopo.



Katibu wa Bunge, Stephen Kagaigai (kushoto), akisalimiana na aliyekuwa Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu (Bunge na Waziri Mkuu), Maimuna Tarishi, alipomtembelea ofisini kwake Bungeni, jijini Dodoma jana, kwa lengo la kumuaga baada ya kustaafu utumishi wa umma na kumshukuru kwa ushirikiano aliompatia kwa kipindi chote alichokuwa anafanya kazi na Bunge. **PICHA: OFISI YA BUNGE**.

# Mahitaji ya nazi nchini bado makubwa

SERIKALI imesema nazi zinazozalishwa nchini bado hazikidhi mahitaji ya soko la ndani ya nchi kutokana na kuongezeka kwa matumizi ya zao hilo ikiwamo ulaji wa madafu.

Aidha, imeelezwa kuwa Tanzania ni nchi ya 10 duniani kwa uzalishaji wa nazi ikiongozwa na Indonesia.

Hayo yalisema jana bungeni na Naibu Waziri wa Kilimo, Omary Mgumba, alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Zaynab Vulu, ambaye alisema zao hilo lina faida nyingi sana kuanzia mti na matawi.

Vulu alihoji ni lini serikali itatafuta soko la kudumu la zao hilo na ina mpango gani wa kuhamasisha kilimo cha nazi kama ilivyokuwa zamani.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri huyo alisema soko la kudumu la zao hilo lipo nchini kwa sababu kiasi cha nazi kinachozalishwa bado hakikidhi mahitaji ya soko la ndani.

Mgumba alisema mafuta ya mwali yanayotokana na nazi yanaendelea kupata umaarufu kutokana na uhitaji wake kuwa mkubwa ndani na nje ya nchi na kwamba kwa sasa lita moja ya mafuta hayo imefikia hadi Sh. 40,000.

"Bidhaa kama fagio, mbao, kamba na samani zinazotokana na mti wa mnazi na uwezo wa zao hilo kutunza mazingira, huongeza thamani ya minazi," alisema.

Naibu Waziri alisema katika kuimarisha soko la zao hilo nchini, msimu wa mwaka 2018/19 wakulima wapatao 74 katika mikoa ya Lindi na Mtwara wamefundishwa namna ya kukamua mafuta ya mwali.

Vilevile, alisema kikundi cha wanachama 50 katika Wilaya ya Bagamoyo kimepewa mashine yenye uwezo wa kukamua lita 500 za mafuta mwali kwa mwaka.

"Aidha, serikali inaendelea kuimarisha masoko ya mazao yote ya kilimo likiwamo zao la nazi kwa kuwaunganisha wakulima na wanunuzi kupitia vyama vya ushirika, masoko ya moja kwa moja kwa viwanda vidogo vya kuongeza thamani," alisema.

Hata hivyo, alisema serikali inaendelea kutoa elimu kwa wazalishaji wa nazi kuendelea kupanda mbegu bora zenye ukinzani dhidi ya magonjwa na zenye tija kubwa.

Alisema Tanzania ni nchi ya 10 duniani kwa uzalishaji wa nazi ikiongozwa na nchi ya Indonesia na kwa Afrika ni nchi ya kwanza kwa kuzalisha wastani wa tani 530,000 kwa mwaka ikifuatiwa na Ghana ambayo huzalisha wastani wa tani 366,183.




# Mbunge ataka lami Singida hadi Simiyu

MBUNGE wa Iramba Mashariki (CCM), Allan Kiula, amehoji serikali lini itajenga barabara ya lami inayounganisha Mkoa wa Simiyu na Singida kupitia daraja la Sibiti lililoko Wilaya ya Mkalama.

Akiuliza swali bungeni jana, Kiula alisema sera ya serikali ya awamu ya tano ni kuunganisha kwa barabara ya lami kati ya mkoa na mkoa.

"Je, ni lini serikali itajenga barabara ya lami inayounganisha mikoa ya Simiyu na Singida kwa kupitia daraja la Sibiti?" Alihoji.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Elias Kwandikwa, alisema mikoa ya Simiyu na Singida inaunganishwa na barabara ya Gumanga hadi Singida mjini yenye urefu wa kilometa 341 na inaunganishwa pia na barabara ya kutoka Bariadi kupitia Kisesa hadi Singida mjini.

Alisema barabara hiyo ina urefu wa kilometa 338 na barabara hizo zinahudumiwa na Wakala wa Barabara Tanzania (Tanroads) mikoa ya Singida na Simiyu.

Kwandikwa alisema ujenzi wa daraja la mto Sibiti lenye urefu wa mita 82 umekamilika na ujenzi wa barabara unganishi zenye urefu wa kilometa 25 umekamilika kwa kiwango cha changarawe na taratibu za ununuzi za kuzijenga kwa kiwango cha lami zinaendelea.

"Barabara ya Sibiti hadi Iguguno yenye kilometa 106 iko upande wa mkoa wa Singida na sehemu ya barabara hii kuanzia Sibiti hadi Mkalama kilometa 27 inaendelea kufanyiwa usanifu wa awali kupitia mradi wa Serengeti Southern By-pass na sehemu iliyobaki ya barabara hii ni barabara ya kiwango cha changarawe na hupitika majira yote ya mwaka," alisema.

Kwa upande wa Mkoa wa Simiyu, alisema barabara ya kuanzia Sibiti hadi Ng'oboko kupitia Lalago-Maswa hadi Bariadi, sehemu ya kuanzia Bariadi hadi Maswa yenye urefu wa kilometa 49.5 inaendelea kujengwa kwa kiwango cha lami," alisema.

Aidha, alisema sehemu ya kuanzia Maswa hadi Sibiti kilometa 146.83 inaendelea kufanyiwa usanifu wa awali kupitia mradi wa Serengeti Southern By-pass barabara inayoanzia Ng'hoboko kupitia Kisesa hadi Bariadi ni barabara ya changarawe na inapitika majira yote ya mwaka.

"Serikali kwa kutambua umuhimu wa barabara hii inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kufanya usanifu wa kina sehemu zingine zilizobaki ili kujengwa kwa kiwango cha lami," alisema.



# RC aagiza ulinzi tangi la maji

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MKUU wa Mkoa wa Arusha, Mrisho Gambo, ameuagiza uongozi wa Kata ya Murriet kuhakikisha wanadhibiti sheria za uchimbaji moramu, ili kuzuia tangi la maji lenye ukubwa wa lita 2,000,000 kuharibiwa.

Gambo alitoa agizo hilo juzi alipokuwa katika ziara ya siku moja ya kuangalia miradi ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Arusha (Auwsa) maeneo ya Kumnyakua, Ngaramtoni, Murriet, Esami, Themi, Chekereni, Maweni, Mbuguni na Valesca wilayani Arumeru na jijini Arusha.

Alisema tangi hilo la maji linalojengwa katika Kata ya Murriet jijini Arusha, litaondoa changamoto ya maji, kwa kuwa ifikapo mwishoni mwa Oktoba, mwaka huu, maji yataanza kupatikana kwa sababu tayari visima 11 virefu vimekamilika eneo la Seed Farm na Magereza vitakavyoongeza cha lita milioni 29 za maji.

Aliwataka viongozi wa kata hiyo, akiwamo Diwani Fransic Mbise na viongozi wengine kuhakikisha wanasimamia sheria, kanuni na taratibu kulinda vyanzo vya maji, ili kudhibiti tangi hilo lisiangushwe kwa sababu ya uchimbaji moramu.

"Naipenda sana kata hii si kwa sababu ni mkazi wa huku, ila lazima tulinde miundombinu hii ya maji. Tumekubali tangi kubwa la maji kujengwa hapa, hivyo lazima sheria na kanuni zisimamiwe ili kulinda tangi hili. Huu uchimbaji wa moramu katika eneo hili udhibitiwe usisababishe mmomonyoko," alisema.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Arusha, Gabriel Daqqaro, alimshukuru Rais John Magufuli kwa kukubali Arusha ipate maji na kuleta mradi huo mkubwa huku akisisitiza kuwa mradi huo utakapokamilika, utatatua kero kubwa ya maji katika Kata ya Murriet na maeneo mengine ya Jiji la Arusha.

"Kero hii ya maji inaenda kuisha kwa kweli. Tunamshukuru Rais Magufuli kwa kutuletea mradi mkubwa wa maji. Nawaomba wananchi mlinde tangi hili kubwa la maji," alisema.

Awali, baadhi ya wananchi waliokuwapo eneo hilo wakiwamo Mwenyekiti wa Umoja wa Wanawake Kata ya Murriet, Zuwena Msangi na Mzee Said walishukuru tangi hilo kujengwa eneo hilo na kumshukuru Rais Magufuli kwa kuondoa kero ya maji hasa kumtua ndoo kichwani mwanamke kwa kuwa maji yatakapoanza kutoka kila mtu atakuwa na bomba lake nyumbani.



Wananchi wa Kata ya Sanu wakimsikiliza Mkuu wa Wilaya ya Mbulu mkoani Manyara, Chelestino Mofuga (hayupo pichani), wakati akizungumza nao juzi. **PICHA: GIFT THADEY**.

## TCRA mitaani usajili wa simu

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

MAMLAKA ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) kwa kushirikiana na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (Nida) imeingia mitaani mjini Babati na kuwataka wananchi kusajili laini za simu ili kudhibiti matumizi mabaya kama ambavyo baadhi ya watu wanafanya.

Mkuu wa TCRA Kanda ya Kaskazini, Mhandisi Imelda Salum, alisema hayo juzi alipokuwa katika uwanja wa stendi ya zamani, wakati akiendesha usajili wa laini za simu na kutoa namba za utambulisho.

Mhandisi Salum alisema usajili wa laini za simu kwa alama za vidole utasaidia kudhibiti utapeli ambao umekuwa ukifanywa na watu wenye tamaa.

Alisema mbali na kudhibiti hilo pia usajili huo utaisaidia serikali kupata takwimu sahihi za watumiaji halali wa simu.

Aidha, aliwataka wananchi kuchangamkia usajili huo wa vidole kabla ya muda kuisha uliotolewa na Rais John Magufuli ifikapo Desemba 31, mwaka huu.

# Wadaiwa kuendesha vikao vya ofisi baa

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

BAADHI ya wanachama wa Chama cha Walimu Tanzania (CWT) mkoani Arusha wamerusha lawama kwa uongozi wa chama hicho mkoa na jiji, kufanyia vikao vya chama katika nyumba za starehe (baa) hadi usiku wa manane, kinyume cha taratibu za uendeshaji wa shughuli za chama.

Viongozi wanaotuhumiwa ni pamoja na Mwenyekiti wa CWT Mkoa wa Arusha, Loota Laizer, na Katibu wake Felix Mnyanyi na Mwenyekiti wa CWT Jiji la Arusha, Grace Msacky.

Tuhuma hizo zimetolewa na baadhi ya wanachama wa CWT Mkoa wa Arusha ambao hawakutaka kutajwa majina yao (Nipashe inayo), wakiwalalamikia pia viongozi wao kwa matumizi mabaya ya fedha na rasilimali za chama hasa magari.

Walitaja moja ya tuhuma hizo ni kikao kilichofanyika Agosti 23, mwaka huu, katika baa ya Mountain View iliyoko katika mji mdogo wa Namanga, mpakani mwa Tanzania na Kenya.

Walisema kikao hicho kiliwahusisha wenyeviti wa CWT wa wilaya za Mkoa wa Arusha ambacho si rasmi kwa kuwa hakuna kanuni ya kisheria inayoelekeza wenyeviti wa chama kukutana na kufanya vikao.

"Kikao kilifanyika katika baa ya Mountain View, Namanga na baadaye jioni viongozi waliendelea kunywa vinywaji (pombe) pamoja na burudani ya muziki na nyama choma hadi usiku wa manane," alisema mmoja wa wanachama ambaye aliomba jina lake lihifadhiwe.

Wanachama hao walisema vitendo vya viongozi wao wanavyofanya kwenye uendeshaji wa chama hicho ni kinyume cha shughuli za uendeshaji wa chama na viongozi wanatumia vibaya madaraka yao pamoja na rasilimali za chama.

Akijibu tuhuma hizo Katibu wa CWT Mkoa wa Arusha, Felix Mnyanyi, kwa niaba ya viongozi wenzake, alikanusha vikali na kueleza kuwa ni majungu yanayolenga kuchafua chama na uongozi, hivyo ni vyema zikapuuzwa.

Alisema kuwa kikao kilichofanyika wilayani Longido ni mwendelezo wa vikao vya wenyeviti wa CWT ambavyo wamejiwekea utaratibu wa kukutana mara moja kwa mwaka na mwaka jana walikutana wilayani Karatu.

"Kikao kilifanyika kwenye ukumbi wa mikutano, tulifika pale saa tano asubuhi tukapewa taarifa za wilaya ya Longido. Mweyekiti wa mkoa alifungua kikao rasmi saa saba mchana na kilimalizika saa 12 jioni. Baada ya hapo wajumbe walikuwa huru kuendelea na utawala binafsi," alisema Mnyanyi na kuongeza:

"Mimi nilialikwa kwa nafasi yangu kama mtendaji wa mkoa kwa ajili ya kutekeleza yale wenyeviti watakayokubaliana na kweli kwenye kikao kile niliagizwa kwenda Dodoma kufuatilia madeni ya waalimu na upandishwaji wa madaraja na safari hii imezaa matunda kwani hivi karibuni walimu wataanza kulipwa madeni yao na kupandishwa madaraja."

Kuhusu suala la matumizi ya magari, alisema yanatumiwa kwa shughuli za CWT pekee na kwenye kila wilaya wenyeviti na makatibu wanatumia gari moja na yanakuwa chini ya usimamizi wa makatibu, lakini inapotokea hawana dereva, makatibu wa wilaya ndio huyaendesha.




# Serikali kumaliza mgogoro madai utapeli wa ada

**Na Godfrey Mushi,** HAI

SERIKALI imepanga leo kumaliza malalamiko ya muda mrefu ya wanafunzi 400 wa Chuo cha Ualimu Moshi zamani Mong'are ambao wanadai kutapeliwa zaidi ya Sh. milioni 78.

Juzi, wanafunzi hao waligoma kuingia katika vyumba vya mitihani ya kumaliza kozi na wengine mitihani ya muhula na kufanya maandamano, wakitaka kujua hatima ya fedha zao za malipo ya ada.

Wanafunzi hao waligomea kuingia katika vyumba vya mitihani ya kuhitimu masomo yao na wengine ambao walikuwa wanafanya mitihani ya muhula iliyokuwa inaanza Septemba 9 hadi Septemba 12, mwaka huu.

Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya, aliiambia Nipashe kuwa baada ya kikao cha majadiliano ya siku mbili na pande zote mbili, leo atatoa majibu yatakayomaliza mgogoro huo.

Wanafunzi wanaodaiwa kulizwa fedha hizo na mhasibu wa chuo hicho, wamo wanaotarajia kufanya mitihani ya taifa ya kada hiyo ngazi ya cheti ya 'Grade' IIIA.

Akizungumza wakati wa maandamano hayo, kabla ya kutawanywa kwa mabomu, Rais wa serikali ya wanafunzi wa Chuo cha Ualimu Moshi (Urom), Herman Tarimo, alisema walibaini kuwapo kwa udanganyifu huo baada ya kufanyika ukaguzi wa ndani Novemba 2018 katika miamala 487 ya kibenki.

Wakala wa benki mojawapo wilayani humo pamoja na chama cha akiba na mikopo kilichopo Moshi Mjini, walitajwa katika sakata hilo.

Alisema chuo kimejaribu kuwasaidia wanachuo hao kufuatilia kwa njia mbalimbali ikiwamo mahakamani ila wanaona kuwa pia haki yao imechelewa na wanahisi kwamba hata watuhumiwa wakitiwa hatiani, fedha zao hawatazipata.

Juzi, baadhi ya wanafunzi walizungumza na Nipashe, Barnabas Inyasi na Aron Alex kwa nyakati tofauti walieleza hawatakubali kuingia kwenye vyumba vya mitihani mpaka hapo watakapojua hatima yao, kwa kuwa watakapokuja kudai vyeti vyao vya taaluma watakwama kuvipata.

Mmiliki wa chuo hicho, Joseph Msaki alimweleza Mkuu wa Wilaya, Ole Sabaya, kwamba wanafunzi hao wanataka kujua hatima yao kwa sababu watakapoondoka baada ya kumaliza mitihani, wakirejea wanajua wataulizwa ada.

# Wafadhili walivyoijenga Same kwa miradi

**Na Godfrey Mushi,** SAME

WAFADHILI wakubwa wa miradi ya maendeleo ya wananchi wa Wilaya ya Same wameondoka rasmi wilayani humo na kufunga ufadhili wao baada ya kipindi cha miaka 17, huku wakiacha alama isiyofutika ya kuwekeza kwenye ujenzi wa zahanati saba, madarasa 54 na vyoo 104.

Taratibu za makabidhiano ya miradi yote iliyotekelezwa na wafadhili hao, ziliongozwa na Mkuu wa Wilaya ya Same, mkoani Kilimanjaro, Rosemary Senyamule na kushuhudiwa na Mwakilishi wa World Vision Australia, Steven Dunham.

Miradi yote iliyotekelezwa na Shirika la World Vision, ilikuwa ikifadhili miradi ya Nakombo AP, iliyopo Tarafa ya Mwembe Mbaga na mradi wa Makindumbe uliofanya kazi katika Tarafa ya Ndungu.

Taarifa iliyotolewa na Mkuu wa wilaya hiyo, inaeleza kuwa miradi iliyokabidhiwa ni madarasa 54, vyoo 104, kompyuta 55, zahanati saba, nyumba za walimu na waganga saba.

Mingine ni mradi wa mifereji ya maji yenye urefu wa kilomita saba, ndiva 10, vyeti vya kuzaliwa 4,114 pamoja na vikundi 83 vya kuweka na kukopa, vyenye jumla ya Sh. bilioni 4.5.

"Haya maendeleo yote yalifanyika chini ya mradi wa Makindumbe uliokuwa ukifanya kazi Tarafa ya Ndungu, kwa ufadhili wa World Vision Switzerland na mradi wa Nakombo uliokuwa ukifanya kazi, Tarafa ya Mwembe Mbaga kwa uliofadhiliwa na World Vision Australia," alieleza Senyamule.

Senyamule alisema muda wa miaka 15 kwa mradi wa Makindube na miaka 17 kwa Nakombo imegusa maeneo muhimu kwa binadamu hivyo ni muhimu ikapewa nafasi ya kuendelezwa kama ilivyokuwa kwa wafadhili.

"World Vision walitushika mkono sasa wanaondoka, tujione kama tunaweza kufanya wenyewe wajibu wetu ni kuona kazi waliyoianzisha tuifanye iwe endelevu. Serikali itachukua hatua kwa kiongozi yeyote atakayefanya uzembe kwenye miradi hii nikija kwenye maeneo yenu moja ya taarifa nitakazotaka kusikia ni miradi ya WVT inaendeleaje."

"Asilimia 97.2 ya watoto wanaenda shule ikilinganishwa na asilimia 76.7 mwaka 2004," alisema Mohamed.

Mwenyekiti wa Mradi wa Nakombo AP uliopo Tarafa ya Mwembe Mbaga, Senge Mkwizu, alisema lengo la mradi wa afya na lishe lilikuwa kuchangia ustawi wa afya na lishe ya watoto ifikapo mwaka 2019.

"Mradi kwa kushirikiana na wadau wa afya umechangia mabadiliko makubwa katika sekta hii ili kuhakikisha kuwa watoto wanakuwa na afya na lishe nzuri wakati wote. Kumekuwa na ongezeko la watoto wanaopata vyakula mchanganyiko vyenye lishe kutoka asilimia 53 mwaka 2012 hadi asilimia 65.4 mwaka 2019."



Mkazi wa mji wa Musoma mkoani Mara, akiwa ameisheheni baiskeli yake kwa mikungu ya ndizi akisaka wateja mitaani jana. **PICHA: SABATO KASIKA**.

# DC ashangaa shule kusuasua kusajiliwa

**Na Godfrey Mushi,** HAI

KUSUASUA kwa miaka 12 kwa usajili wa Shule ya Msingi Mtakuja, kumemshangaza Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya, baada ya kuelezwa wanafunzi wake wanalazimika kwenda shule ya jirani iliyopo kilomita 32 kila siku.

Ole Sabaya ametaka shule hiyo isajiliwe mapema ili kuwapunguzia adha wanafunzi wake kutembea umbali mrefu kufuata masomo.

Jana, alikwenda katika kijiji hicho baada ya wananchi wa Mtakuja kumweleza kuwa pamoja na kukamilika kwa ujenzi wa shule hiyo miaka 12 iliyopita bado, shule hiyo haisajiliwa.

Katika mkutano wa hadhara, wananchi hao walimweleza Mkuu huyo wa wilaya kuwa watoto wao wanatembea umbali wa kilometa 32 kwenda Shule ya Sekondari ya Kia, kila siku na kurudi nyumbani.

Mmoja wa wananchi hao, Saufa Shaban, alisema shule hiyo ilijengwa miaka 12 iliyopita imekamilika miundombinu yote, lakini tatizo ni usajili kukwama.

"Mheshimiwa DC (Mkuu wa Wilaya), kutokana na umbali huo watoto wetu hawapati elimu yenye manufaa kabisa, wanaishia kupata ujauzito wengine wanaacha shule kabisa na wale wanafanikiwa kumaliza shule hawana ufaulu mzuri, hivyo kusababisha kijiji chetu kuendelea kuwa maskini," alisema Saufa.

Mkuu huyo wa wilaya alimtaka Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Hai, Yohana Sintoo, kuhakikisha shule hiyo inapata usajili ndani ya siku 90 ili kuwaondolea wanafunzi adha ya kumbea umbali huo.

Akijibu hoja iliyoelekezwa na Mkuu huyo, Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Hai, Elia Machange, alisema shule hiyo imechelewa kusajiliwa kutokana ma upungufu wa kukosa mabara za sayansi.

"Nikuhakikishie mheshimiwa Mkuu wa Wilaya kwamba mwaka huu, Sekondari ya Mtakuja itasajiliwa na wanafunzi watakaohitimu darasa la saba mwaka 2019 watapangiwa shule hiyo," alieleza Machange.

Pia walitaka umeme uwekwe kwenye zahati ya kijiji hicho, kutengenezewa barabara ya kilometa saba kwa kiwango cha moramu.



Wabuni mradi kinamama 'hohehahe' wapewe ujanja na kumiliki magenge Ukurasa 19

UCHUMI



## Uwekezaji, ajira za wazawa zinapokimbizwa na 'umbu-mbu-mbu' vita ya wageni Afrika Kusini

Ukurasa 14


# BUFE

Ijumaa Septemba 13, 2019

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA





UCHUMI NACHINGWEA MPYA

# Machinga walivyojaa uwanja wa nyumbani kusisimua ujasiriamali

Ukurasa 16


UCHUMI Ukurasa 18

Biashara katika picha Ukurasa 17

UCHUMI

# Uwekezaji, ajira za wazawa z 'umbu-mbu-mbu' vita ya wag

- Kinachojiri, mizizi tukio la miaka minne
- 'Moshi' wanaojitokeza, 'kuni' wametulia
- Uwekezaji hatarini, haujapiku tangu 2015

**Na Nimi Mweta**

VYOMBO vya habari na watafiti nchini Afrika Kusini vimejitahidi kueleza sababu za mashambulizi makubwa dhidi ya wageni, lakini safari hii wameandika kidogo, ikilinganisha na mwaka 2015, mashambulizi hayo yalipoanza kwa ngazi ya nguvu.

Pia ni tabu kupata mchanganuo halisi wa athari za mashambulizi hayo kwa sekta tofauti za uchumi. Kwa kuangalia mtiririko wa takwimu kuna picha inayojitokeza, kwa msingi wa mashambulizi ya 2015 na uchumi ulivyojikongoja baada ya hapo.

Ni kama ilivyo Afrika Kusini inaurudia mkanda huo na inaelekea safari hii, iwe tabu zaidi kurudisha uwekezaji au kupata wafanyakazi kutoka nje ya nchi na mambo yanayofanana nayo.

Imeshuhudiwa kauli za kimataifa, huku nchi kama Nigeria kutuma ndege maalumu, juzi ikiwakusanya raia wake kurudi nyumbani, baadhi walikuwa huko kwa miaka 30 wakiendelea na shughuli mbalimbali, ikiwamo biashara.

Rais Cyril Ramaphosa naye ameshatoa amri kali kupinga kinachofanyika huko, pamoja na hatua za kisheria kufuatilia chanzo na wahusika wa vurugu hizi nchini mwake.

**MZIZI WA VURUGU**

Watetezi wa kinachotokea Afrika Kusini, ingawa hawaungi mkono mashambulizi dhidi ya wageni wenye ajira na hasa biashara katika miji mikubwa nchini humo, wanasema tatizo lilianza wakati wa ukoloni.

Ardhi kubwa ya maeneo ya Wazulu upande wa ama Mashariki au Kaskazini Mashariki ya Afrika Kusini, ilichukuliwa na wahamiaji wa Kizungu waliofungua mashamba.

Kwa miaka mingi Wazulu wakawa wanashindania ajira na wageni, kuanzia wahamiaji wa Kihindi walioletwa na Uingereza kusaidia kujenga miundombinu tofauti.

Katika vurugu za hivi karibuni, hazikusikika kwa nguvu sauti za uchochezi kuwashambulia wageni, labda kwa njia za mitandao au hotuba za hapa na pale.

Lakini, katika wimbi la mashambulizi mwaka 2015 alikuwa ni Goodwill Zwelithini, Mfalme wa Wazulu, ambaye hakuishia kutoa rai tu, pia amri kuwa 'wageni wafungashe virago waondoke' nchini humo.

Hapo anamnyooshewa kidole mwanawe, Jacob Zuma, aliyekuwa Rais wakati huo, aliyabariki kimyakimya. Mashambulizi yalianza kwa sababu mfumo wa kijamii wa nchi hiyo hauwezi kukamata hisia hizo na kuziminya, kama ilivyo Kenya wakati mbunge mwenye historia ya miziki ya kufoka alipotoa rai hiyo, nchi ikamkana.

Afrika Kusini imeshindwa mara kadhaa kukemea rai za kikabila na kibaguzi kama hizo, kwani wageni wanaingizwa katika mizania ya kikabila kama kundi linalopata upendeleo katika ajira au linalosaidiana katika fursa za biashara.

Sababu ya kufanya tatizo la ajira na biashara liwe la kikabila ni tatizo maalum kwa Afrika Kusini. Jamii ya kabila la Wazulu, wamekuwa na



Rais Cyril Ramaphosa; ana kazi nzito kukabili ukakasi wa kiutawala.

> **Katika tamaduni, kwa mfano za kuiba ng'ombe, kuchoma maduka ya wageni na kupora vitu, tofauti hiyo ni ndogo au labda haipo kabisa. Hivyo, makundi ya vibaka yanawafukuza wageni, ili waajiriwe kwa mshahara mzuri wanaotaka kama raia wa nchi hiyo, ambao 'wamenyanyaswa kwa kiasi cha kutosha.'**

nafasi ya kipekee katika nchi hiyo, kama ilivyowahi kujitokeza katika baadhi ya nchi za Afrika Mashariki. Sura ya mshikamano na hitaji la kitabaka.

Baadhi ya vyombo vya habari vinasema kuwa 'rushwa ni chembe muhimu ya uchochezi dhidi ya wageni.' Hapo inamaanisha Afrika Kusini, ina serikali za majimbo zinazochukua fedha nyingi kutoka bajeti ya serikali ya shirikisho.

Siyo rahisi kwa Serikali Kuu kusimamia matumizi ya fedha katika serikali za majimbo, kwani hazina watawala wa kuteuliwa na serikali ila wa jadi.

Kwa mfano, Mfalme Zwelithini anatumia fedha za jimbo anavyotaka na akiona joto linaanza kupanda kuhusu suala hilo, huku anajua matatizo ya watu wake jijini Durban na kwingineko, wanavyosononeka wakiona wageni wameshika biashara, ajira na hata kumiliki wanawake vijana wa Afrika Kusini, anapata fursa kutoa rai za aina hiyo.

Serikali ya Taifa, ikijua vijana hao wanaotembeza mkong'oto kwa kila



Hali halisi ya vurugu ilivyokuwa nchini humo. **PICHA ZOTE: MTA**

# inapokimbizwa na
# geni Afrika Kusini

mgeni watakayemkuta, wanawasikiliza viongozi wao wa jadi na siyo serikali. Inabidi imwombe mfalme awatulize vijana wake, wampe pesa awasaidie.

Kimsingi ni mazingira ya rushwa, ubadhirifu katika serikali za majimbo na kutumia silaha za ukabila na utaifa 'feki' kutoa shinikizo kwa serikali ya shirikisho kuondoa wageni, ili Wazulu kabila linalobeba wengi wasioajirika wapate unafuu, waajiri wawakubali kwa kukosa wengine.

Si rahisi katika makundi hayo yanayoshika fimbo au fito ndefu kuwapiga wageni, kutofautisha kati ya vijana wanaotafuta kazi na vibaka wa kawaida tu.

Katika tamaduni, kwa mfano za kuiba ng'ombe, kuchoma maduka ya wageni na kupora vitu, tofauti hiyo ni ndogo au labda haipo kabisa. Hivyo, makundi ya vibaka yanawafukuza wageni, ili waajiriwe kwa mshahara mzuri wanaotaka kama raia wa nchi hiyo, ambao 'wamenyanyaswa kwa kiasi cha kutosha.'

Sera hiyo ya kuwalazimisha wawekezaji waajiri Wazulu kwa mtutu wa bunduki au marungu na mapanga, si kigezo cha mvuto kwa uwekezaji nchini humo.

**UWEKEZAJI UNAYUMBA**

Takwimu zinaonyesha kwamba, kila vurugu zinapotokea, uwekezaji unapungua kwa kipindi fulani, hadi



NDAO.



Mfalme Goodwill Zwelithini; ananyooshewa vidole.

wawekezaji wasahau, waone hali iko kawaida.

Hivyo, katika takwimu za uchumi za mwaka 2015 hadi 2019 bado zinaonyesha kwamba mwaka 2015 ndiyo ulikuwa na uwekezaji zaidi, ikiweka maana kuwa fedha za uwekezaji zilishapangwa au kufikishwa huko wakati vurugu zinaanza.

Ulipofika mwaka uliofuata na kuendelea hadi mwaka wa fedha uliopita, uwekezaji ulishuka kwa nguvu na kuanza kupanda tena taratibu.

Hapo ina maana kwamba, waliowashambulia wageni wameshatonesha kidonda, kuwa na tabia ya kutotaka kuwaona kuona wafanyakazi wa kigeni, imeota mizizi na itadumu, ikisukumwa na ubadhirifu na rushwa hivyo 'kuitia kabali' serikali ya shirikisho iwategemee wabadhirifu kuwatuliza vijana wao.

Chama cha Wazulu cha Inkatha Freedom Party kipo na kinasimamisha wagombewa, huku upande mwingine kuna African National Congress (ANC) na Democratic Party (DP), vyote vinaungwa mkono katika chaguzi za ngazi zote. Hivyo, waandamanaji na wanaowadhuru wageni siyo vibaka wa kukamatwa, bali ni wapigakura muhimu.

Hiyo inadokeza kuna maana fulani tata, serikali kuu inapokaa kimya, huku msemaji wa polisi akitamka: "Kuna vurugu, ila si chuki ya wageni..."

**HASARA KITAIFA**

Hasara ambazo uchumi wa Afrika Kusini itapata siyo kidogo, kwani jitihada za Umoja wa Ulaya kuweka fedha kwa ajili ya maendeleo ya mkusanyiko wa nchi za Kusini mwa Afrika kutumia Afrika Kusini, kama kitovu cha kuunganisha uchumi wa nchi hizo zitapunguzwa.

Kitovu hiko huenda kitahamishiwa mfano Kaskazini zaidi, kwa Gaborone nchini Botswana au Lusaka, Zambia, kwani Harare bado kuna wasiwasi kuhusu demokrasia nchini Zimbabwe.

Nchi kama China ambazo zingetumia Afrika Kusini kama kitovu cha viwanda kwa nguvu kazi na taaluma 'bei poa' kutoka nchi tofauti za Afrika, zinaweza kuhamishia mipango yao katika mataifa kama Nigeria, Kenya, Tanzania na Misri.

Maana iliyopo hapo ni kwamba, kuwa ule msemo wa 'kufa kufaana' utaonekana kwa kiwango fulani katika uhusiano wa uchumi wa kimataifa na Afrika Kusini, kwa faida ya nchi za jirani hasa za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC).

Badala ya mitaji kuingia nchini Afrika Kusini, halafu kwingine kupelekwa bidhaa kwa muhuri wa eneo la muungano wa ushuru wa forodha, mambo yanakuwa kinyume chake.

Kwa vipi? Bidhaa kupitia mabadiliko Afrika Kusini sasa ndiyo itakuwa inaingiza bidhaa zenye mihuri, kutoka nchi za jirani kulikogeuzwa kitovu, ambako mishahara ni midogo zaidi na wafanyakazi wana tija na nidhamu, hakuna makundi ya vibaka, ni watiifu pasipo amri ya Chifu Zwelithini.

Wachina wana msemo: "Mtu mpumbavu huinua jiwe na kuliangusha katika miguu yake mwenyewe." Hivyo, vibaka wanaomtii Chifu Zwelithini, wanajiharibia ajira zao.

**Makala hii ya uchambuzi ni kwa mujibu wa ufuatiliaji matukio na taarifa mbalimbali za kimataifa kuhusu Afrika Kusini.**

## Nguo zitokanazo na uyoga sokoni

MARA nyingi watu maarufu hutoa msukumo mkubwa kwa watu kufanya uchaguzi wa mavazi aina fulani na soko la mavazi kidigitali, pia umeongeza uhitaji wa nguo kukua kwa kasi.

Barani Ulaya, kunaelezwa kimasoko kasi ya ununuzi imeongezeka mara mbili ya kawaida ya miongo iliyopita. Sasa inaelezwa na watafiti, nguo ni asilimia 20 ya taka zilizopo duniani na kusababisha gesi za ukaa kwa asilimia 10.

Wanaharakati wa mabadiliko ya tabia nchi wanataka watu kupunguza kasi ya kununua nguo. Sasa kuna namna mpya ya kutengeneza nguo, kukabiliana na tatizo hilo kuchukua mbadala wa nguo zinazotengenezwa na pamba na ngozi.

Inaelezwa, ngozi ni bidhaa inayotokana na nyama na inatumia kiasi kikubwa cha maji na kemikali ambazo sio rafiki kwa mwanadamu.

Hivyo 'binadamu hawashindwi' sasa wameanza kuacha matumizi ya ngozi na kuhamia majani ya mananasi, kama vile kampuni moja maarufu ya mikoba imefanya ubunifu huo.

Pia kuna matumizi ya uyoga, ambao umekuwa ukitumika kama chakula, sasa mi malighafi ya nguo. Inaelezwa kwamba wateja wengi wamevutiwa bidhaa hizo ambazo zinaunga mkono katika kampeni ya maendeleo endelevu, ingawa changamoto bado ni gharama kuwa juu zaidi.

Asilimia 40 ya nguo zinazovaliwa duniani zinatengenezwa na pamba na mbadala wake ni nguo zinazotengenezwa kwa nyuzi. Ni utengenezaji unaohitaji asilimia 95 ya maji.

Nguo zinazotengenezwa na miti zinafanana sana na nguo iliyotengezwa na pamba. Utengenezaji wa nguo kwa kutumia pamba, bado unatajwa kuwa ni nafuu, ingawa kuna umuhimu wa watu kuzingatia maendeleo endelevu ili kukabiliana na changamoto ya mazingira.

Ushauri uliopo duniani ni kwamba, kuna uhitaji wa watu kuzingatia namna wanavyonunua bidhaa zao, ni vyema kuwa na kiasi na zenye ubora mzuri.

"Unaweza kununua nguo 30 na zikakutosha bila kuathiri mazingira," anasema mtaalamu wa mavazi, Dk. Blackburn.

Miaka ya hivi karibuni, inaelezwa katika baadhi ya sehemu wateja wa nguo wameanza kuelewa kuwa kununua nguo za gharama nafuu, si jambo jema hata kama matangazo huwa yanavutia, lakini athari ni kubwa kwa muda mfupi.

• **KWA MUJIBU WA TAARIFA ZA KIMATAIFA.**



Akiringa katika mavazi yake yaliyotengenezwa kwa uyoga. **PICHA: MTANDAO.**

UCHUMI

UCHUMI NACHINGWEA MPYA

# Machinga walivyojaa uwanja wa nyumbani kusisimua ujasiriamali

- Kila kona wametinga vitambulisho kifuani
- DC akoshwa, eti naye kilugha '...kucheele'

**Na Sabato Kasika**

UNAPOTAJA msamiati Machinga, kwa wakazi mikoa ya Lindi na Mtwara, wanaanza kwa maana ya kabila, kisha mengine kitaifa.

Mtu anapogeuza matumizi hayo kuanzia sura kitaifa, maana kuu inaanzia wajasiriamali wanaobeba mizigo mikononi wanahama kutoka sehemu moja hadi nyingine na baadhi wa vituo maalum. Ni maduka katika sura ya kijasiriamali.

Jamii hiyo ina historia ndefu ya kuingia katika mfumo kamili wa kuingia katika biashara rasmi, baada ya kupambana kupitia safari ndefu na mamlaka za dola, kuhusu uhalali wakihojiwa leseni, kodi, mahali rasmi pa biashara na uchafu wa mji.

Dar es Salaam, ikiwa makao makuu na mwanzo wao tangu safari huyo ianze, kabla ya kusambaa mikoa mingine, kundi kubwa la wanaofanya biashara hiyo, sehemu kubwa wanadaiwa vijana kutoka mikoa Kusini, kutoka kabila la Machinga.

Ni historia inayofanana sana na mabasi ya daladala ambayo mwanzoni mwa miaka ya 1980, yalipoanza huduma kwa kuiba safari kwa nauli ya shilingi tano na hata yakabatizwa jina 'daladala' kabla ya kuhalalishwa kuwa usafiri rasmi.

Kuhalalishwa huko kibiashara ziliteka soko la mabasi ya umma, Shirika la Usafiri Dar es Salaam (Uda) ambayo zamani yalianzia Dar es Salaam City Transport (DCT) na Dar es Salaam Motor Transport (DMT) kwa vipindi tofauti.

Hizo ni nyayo zinazoshabiliana kutoka kwa Machinga, walioteka soko la maduka makubwa kwa madogo, nao wakiwa sasa wamehalalishwa rasmi kwa ngazi zote.

Ingawa Machinga wanadumu na sifa ya jina, lakini inaelezwa sasa kuna jamii nyingi zimejiunga katika biashara hiyo, wakiwamo vijana wanaotajwa kutoka mkoani Kigoma, wanatapakaa nchini.

Uamuzi wa Rais Dk. John Magufuli, kuandaa vitambulisho maalum kwa ajili ya machinga na wajasiriamali wote wadogo nchi nzima, vilivyokabidhiwa kwa wakuu wa mikoa, waliovishusha kwa wakuu wawagawie wahusika kwa Sh. 20,000, ni habari njema sana kwao.

Imekuwa faraja, kwani kuna zuio la kodi nyinginezo, pia bugudha katika shughuli zao, ingawaje Rais alipoingia tu madarakani alitoa maagizo kadhaa ya 'kuwakingia kifua' dhidi ya bugudha kwa ujasiriamali wao.

Ni hatua inayoenda malengo baadhi ya malengo 17 ya Umoja wa Mataifa (UN), inayohimiza uwapo wa kazi za staha na uchumi jumuishi kwa ajili ya maendeleo endelevu duniani, katika safari ya kuuondoa umaskini ifikapo mwaka 2030.

**KWAO WALIVYO**

KAMA ilivyo miji mingine nchini, mji wa Nachingwea mkoani Lindi, ghafla mtu anapofika na kupata tafakari au uchangamfu wa mji na biashara, ni dhahiri jamii ya machinga, bodododabda maduka, migahawa na mamalishe ataishuhudia imemea kona zote.

Watu hao wametapakaa katika mitaa ya mji huo, ikiwamo katikati ya mji eneo la stendi ya zamani wanakouza nguo mpya, mitumba, viatu na matunda, huku mamalishe hawako nyuma na vyakula, baadhi wakishuhudiwa na vitambulisho vyao kifuani.

Ni ishara ya haraka kuwapo ajira binafsi, kuanzia kinamama wanaopanga biashara zao hadi kando ya barabara.



Mandhari ya Mji wa Nachingwea, unaofanyiwa mageuzi. PICHA ZOTE: MTANDAO.

**MKUU WILAYA**

Mkuu wa Wilaya, Rukia Muwango, anasema alipokea vitambulisho 15,000 vya wajasiriamali na tayari ameshagawa 8,540, huku akiendelea kugawa vingine 6,460 vilivyosalia, kuhakikisha kila mtu mwenye sifa anapata.

> **"Tukigawa vyote tutakuwa tumekusanya shilingi milioni tatu na nina uhakika tutafanikiwa, kwani wilaya yetu ina wanafanyabiashara wakubwa, wa kati na wadogo zaidi ya 300," anasema Rukia.**



Mkuu wa Wilaya, Rukia Muwango, akizungumza.

"Tukigawa vyote tutakuwa tumekusanya shilingi milioni tatu na nina uhakika tutafanikiwa, kwani wilaya yetu ina wanafanyabiashara wakubwa, wa kati na wadogo zaidi ya 300," anasema Rukia.

Anasema wafanyabiashara na wakazi wa Nachingwea, kwa ujumla wamepata elimu ya mlipakodi na tozo za serikali, hivyo anaamini wanatambua umuhimu wa kufanya shughuli zao bila ya usumbufu kisheria.

Rukia anasema, kazi ya kuwatambua wenye sifa ya vitambulisho inaendelea kuanzia ngazi ya vitongoji.

Anasema Nachingwea ina masoko makubwa manne ya wilaya, akiyataja ni; Tunduru Leo, Voda na Kilimani Hewa, sambamba na magulio ya kila wiki katika kata zote 36 wilayani.

"Masoko hayo yapo tarafa ya Nambambo ambayo ipo mjini. Pia, Nachingwea ina tarafa tano na kila tarafa ina masoko manne," anasema.

Anataja shughuli zingine za uchumi wilayani humo ni kuuza baadhi ya mazao anayoyataja; korosho, ufuta, ambayo ni ya biashara, mbaazi ambayo ni chakula na biashara na mengine ya chakula.

"Hayo ni miongoni mwa vyanzo vya mapato ya halmashauri yetu, ambayo msimu wa mwaka 2018/2019 ilitarajia kukusanya Sh. bilioni 2.8, lakini ikafikia asilimia 83 kutokana na sababu ambazo ziko juu ya uwezo wao," anasema.

Kwa upande wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Mkuu wa Wilaya anasema ilipanga kukusanya Sh. milioni 900, lakini ikaishia asilimia 84 ya malengo ya makusanyo.

**BOMOABOMOA?**

Rukia anaeleza katika harakati za kupanua mji wa Nachingwea kuufanya wa kisasa zaidi, baadhi ya nyumba zilizokuwa kando ya barabara zimebolewa, kupisha upanuzi huo.

"Yaani kama ungekuja miaka miwili iliyopita ungekuta nyumba zenye mabati makuu makuu, lakini sasa Nachingwea 'kuchele' (imekucha - inapendeza). Kuna nyumba nyingi za kisasa na maduka mengi mazuri," anasema.

Anazitaja nyumba hizo zilijengwa baada ya ubomoaji, Wakala wa Barabara (Tanroads) wana mpango wa kupanua barabara zinazounganisha mikoa, ili kurahisisha usafiri na huduma nyingine muhimu.

Mkuu wa Wilaya anazitaja barabara ni: Nachingwea hadi Masasi (kutokea Ndanda), Nachingwea hadi Liwale na Nachingwea hadi Ruangwa, zilizoko katika maandalizi ya kupanuliwa na nyumba zilizokuwapo kando zilishashavunjwa.

"Kwa kuwa wananchi wanataka maendeleo, walipoambiwa kubomoa nyumba zao zilizo kando ya barabara, walifanya hivyo haraka sana na kujenga nyingine za kisasa, ambazo sasa zinang'arisha mjini wetu," anahitimisha Rukia, kwa tabasamu lenye ujumbe wa kufurahia mageuzi.

- ***Usikose makala nyingine, Ijumaa ijayo.***

## BIASHARA KATIKA PICHA



Meneja wa Benki ya NBC Tawi la Lindi, Iovin Mapunda (katikati aliyevaa suti), akikabidhi msaada wa mabati 135, pamoja na mifuko 30 ya saruji kwa Mkuu wa Wilaya ya Lindi, Shaibu Ndemanga, jana, kwa ajili ya kusaidia ujenzi wa Kituo cha Polisi cha Rondo Mnara ikiwa ni sehemu ya shughuli za kusaidia jamii. Kushoto ni Mwakilishi wa Kamanda wa Polisi wa Wilaya hiyo, Inspekta Benard Simpemba. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**



Meneja wa Benki ya NMB, Kanda ya Dar es Salaam, Badru Idd (wa pili kushoto), na Mkurugenzi wa Manispaa ya Ilala, Jumanne Shauri (kulia) wakipiga makofi baada ya benki hiyo, kukabidhi msaada wa madawati 50 kwa Shule ya Msingi Kibaga iliyoko Kinyerezi, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**



Vijana wakichoma moto matairi ili wapate waya kwa ajili ya kuuza, kwa ajili ya kujipatie riziki, katika eneo la Jangwani, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

UCHUMI



Mkuu wa Wilaya ya Nachingwea, Rukia Muwango, akiwa katika kikao cha kuhamasisha ulipaji kodi. **PICHA ZOTE: BLOGU YA LIWALE.**

## UCHUMI NACHINGWEA MPYA

# Wazito 'waliposhika chaki' darasa maalum la kodi kwa wananchi wao

- DC: Tunaanza elimu, inafuata sheria
- RC awafunda maana na kazi ya kodi

**Na Sabato Kasika, aliyekuwa NACHINGWEA**

MWISHONI mwa mwezi uliopita, Wilaya ya Nachingwea mkoani Lindi, ilifunga kampeni ya 'Wiki ya Elimu ya Mlipa Kodi na Tozo za Serikali' iliyofanyika kwa muda wa wiki moja.

Ni kampeni hiyo iliyoandaliwa na Ofisi ya Mkuu wa Wilaya, kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wakiwamo Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Wakala wa Misitu Tanzania (TSF), benki na vyombo vya habari.

Elimu hiyo ilifikishwa kwenye tarafa tano za Wilaya ya Nachingwea, ambazo ni Naipanga, Kilimarondo, Lionja, Nambambo na Ruponda, huku viongozi wa tarafa hizo wakitarajiwa kuishusha kwenye kata zote 36 za wilaya hiyo.

Kuendeshwa kwa kampeni za elimu hiyo, kulitokana na hatua zilizochukuliwa na Mkuu wa Wilaya, Rukia Muwango, anayesema kwamba alifanya utafiti na kubaini watu wengi hawana uelewa kuhusu umuhimu wa kulipa kodi.

"Watu wengi wamekuwa wakidai kupata huduma mbalimbali za serikali, kulaumu miundombinu bila kujua kwamba hayo yote yanatokana na kodi ambazo zinalipwa na sisi wenyewe Watanzania," anasema Rukia.

Anawalaumu baadhi ya wakazi wake kutotambua wajibu wa kulipa kodi na tozo mbalimbali za serikali, huku wakidai huduma pekee, hali iliyomfanya kuanzishe kampeni ya 'Elimu ya Mlipakodi na Tozo za Serikali'.

Ni kampeni iliyofungwa mwishoni mwa wiki iliyopita na Mkuu wa Mkoa wa Lindi, Godfrey Zambi, aliyetoa somo kwa wakazi wa Nachingwea, ambalo wakilizingatia litakuwa na manufaa kwao.

**WAKUFUNZI, DC&RC**

Mkuu wa Mkoa, anaanza kwa kuwakumbusha kwamba, kila nchi duniani, maendeleo yake yanapitia katika kodi zinazokusanywa kutoka kwa wananchi, wakiwamo wafanyabiashara wakubwa, wa kati, wadogo na wananchi wa kawaida.

"Kwanza kabisa tumieni elimu mliopata kwa kulipa kodi na tozo mbalimbali za serikali, kwa ajili ya maendeleo ya wilaya yenu. Pia, mnaonunua bidhaa madukani daini risiti kwani kuna kodi ya serikali humo," anasema Zambi.

Anasema maendeleo hayaji kienyeji tu, bali kwa utaratibu maalum uliowekwa, ikiwamo watu kulipa kodi na kwamba ndio maana TRA imepewa dhamana ya kusimamia suala la kodi.

Zambi anaendelea: "Siyo kusimamia tu, bali na kutoa elimu, ili kila Mtanzania atambue umuhimu wa kulipa kodi, badala ya kuwaona watumishi wa TRA kama maadui pale wanapotoza kodi."

Mkuu wa Mkoa anawataka wananchi wake kuona fahari kulipa kodi na tozo mbalimbali za serikali na kutambua kwamba nchi zote duniani, maendeleo yake yanayotokea kwenye kodi wanazolipwa.

"Bila ya wananchi kulipa, nchi haiwezi kuendelea na kumbukeni kuwa huduma zote zinazotolewa na serikali zinatokana na kodi," anasema Zambi.

Mkuu wa Wilaya, Rukia Muwango, anafafanua kuwa Nachingwea ina wafanyabiashara wakubwa, wa kati na wadogo zaidi ya 300, wanapotumia vizuri elimu ya mlipakodi, wanaweza kusaidia kusukuma mbele maendeleo.

"Tuliamua kufikisha elimu hii kwenye tarafa zote tano za wilaya yetu, kwa lengo kwamba viongozi wa tarafa hizo wataishusha kwenye kata hadi itafikia ngazi ya nchi kabisa," anasema Muwango.

Mkuu wa Wilaya anafafanua kwamba, kaunzia sasa suala la kutoa elimu ya mlipa kodi na tozo za serikali litakuwa endelevu hadi kuhakikisha wakazi wote Nachingwea wanaelewa umuhimu wa kulipa kodi.

"Cha msingi ni watu kutambua kwamba suala la kulipa kodi na tozo za serikali lipo kisheria, hivyo watakaoendelea kukiuka watakamatwa na kufikishwa kwenye vyombo vya sheria," anasema.

Anasema Nachingwea kuna shughuli zinafanyika zikiwamo za kilimo, biashara ya mazao ya chakula, mbao na nyingine nyingi, ambazo zinatakiwa kulipiwa kodi na tozo za serikali kwa ajili ya maendeleo.

Miongoni mwa mazao makuu ya biashara wilayani Nachingwea hivi sasa ni korosho na ufuta ambao



Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya Nachingwea wakiwa kwenye kikao. Hao ni wadau muhimu wanaotarajiwa kueneza elimu ya darasa la kodi, lililoanzishwa na Mkuu wa Mkoa, Godfrey Zambi na Mkuu wa Wilaya, Rukia Muwango.

limepata umaarufu hivi karibuni, baadhi ya walimaji wanatoka nje ya wilaya.

Rukia anasema, mapato yatokanayo na kilimo yanapaswa kutozwa kodi na tayari wananchi wameelimishwa na wanaendelea kuelimishwa, lengo ni kutambua kwamba hata wao wanatakiwa kulipa kodi. "Panapo majaliwa, Mei mwaka kesho tutafanya kujua hali ilivyo katika ulipaji wa kodi huku elimu ikiendelea kutolewa, kwani tumedhamiria kutoka hapa tulipo kwenda mbele kwenye ulipaji wa kodi," anasema.

Kwa mujibu wa Mkuu wa Wilaya, lengo la uongozi ni kufikia vijiji vyote 127 wilayani, ili kila mwananchi apate elimu itakayomwezesha kutambua haki yake kulipa kodi, ama kwa kudai risiti au kwenda katika mamlaka husika ya kulipa tozo.

Anasema elimu hiyo ikipenya hapatakuwapo na kulaumiana kati ya wananchi na serikali, badala yake kila mmoja atatimiza wajibu wake kwa ajili ya maendeleo.

Mkuu wa Wilaya anasisitiza, hivi sasa si wakati wa kulaumiana na wananchi kuhusu kodi, bali kutoa elimu na kisha taratibu za kisheria zitafuata kwa wanaokwepa wajibu wao kulipa kodi huku, ilhali wanajua ni mtaji wa maendeleo ya nchi.

Nachingwea ina ukubwa wa kilometa za mraba 7,070 zinazoundwa tarafa tano, kata 36 na vijiji 127, ambavyo vinatumiwa kwa kilimo na nyingine za uzalishaji, kwa ajili ya maendeleo ya wananchi.

Hiyo ni wilaya iliyomo mkoani Lindi, nyingine ni Ruangwa, Liwale, Kilwa na Lindi Manispaa.

UCHUMI

Na Renatha Msungu, DODOMA



Mkurugenzi wa Taasisi ya Endless Success Foundation, Amina Feruz (kushoto), akitoa ufafanuzi kwa mwandishi wa makala hii. Picha nyingine, akitoa mafunzo ya ujasiriamali kwa wahitaji wake. **NA MPIGA PICHA WETU.**

# Wabuni mradi kinamama 'hohehahe' wapewe ujanja na kumiliki magenge

KINAMAMA wa mjini Dodoma sasa wako juu na salama kiuchumi, wakajiunga na miradi mbalimbali ya ujasiriamali.

Hiyo inapitia wapi? Hiyo ni taasisi isiyo ya kiserikali inayofanya kazi kwa ushirikiano na serikali, ili kuinua uchumi wa kinamama, mahsusi wajane na wahitaji kadha wa kadha.

Asasi hiyo iitwayo Endless Success Foundation, imeamua kujikita kwa kinamama, sambamba na makundi mengine maalumu ya kijamii yasiyojiweza.

Lengo hapo ni kuisaidia jamii iweze kukua kiuchumi na kimaendeleo. Mbali na kuisaidia jamii, taasisi pia inawasaidia watoto wenye ulemavu na walioko ndani ya makundi maalum kuhakikisha wanafikia lengo la taifa kufikia uchumi wa viwanda.

Amina Feruz, Mkurugenzi wa asasi hiyo, anasema katika kufanikisha lengo lao, wameunda kampuni iitwayo Genge Special, inayolenga kumwinua mjasiriamali mdogo katika biashara wanazofanya kila siku.

Maeneo ambayo kinamama hao wajasiriamali, wenye ulemavu na wajane wanafundishwa, ni namna ya kupata mkopo na kutunza vyema fedha zake, ili zitumike kwa malengo yaliyokusudiwa.

Amina anasema wameanzisha kampeni hiyo wakinuia kumkwamua mama mjasiriamali wa ngazi ya kumiliki genge ili kuwa na kundi kubwa la wanaomudu maisha yao ya kila siku.

Mkurugenzi huyo anasema, kampeni hiyo itawarahisishia kutoa mafunzo ya utunzaji fedha ambazo wahitaji walizokopa zitumike kwa usahihi.

Anasema wameamua kufanya hivyo, baada ya kubaini wajasiriamali wengi wadogo hawajui matumizi ya mikopo ya fedha na wanaishia kuangukia katika hasara za kibiashara na inawarudisha nyuma.

"Hatutamwacha mwanamke aendeshe biashara ya genge mwenyewe, bila ya kumfuatilia anafanya nini. Lengo ni kuona anatoka na kupanda kiuchumi kupitia biashara yake ya genge," anasema.

Huku akisema kuwa Genge Special, inakusudia kuwainua kiuchumi kinamama wengi, Amina ana ufafanuzi: "Kampeni hii ni muhimu sana tumejikita kuisambaza kwa wajasiriamali wanawake ambao kufanya biashara hizo."

**KAMPUNI INA SHUGHULI MAALUM**

Mkurugenzi Amina, anasema kutaandaliwa vikundi vya watu watano, watakaopewa semina na baadaye wanakabidhiwa mtaji kwa ajili ya kuanzisha genge la bidhaa hasa za vyakula.

Anasema biashara hizo zitakuwa zikifuatiliwa na taasisi ya Endless Success, kuhakikisha mwanamke mjasiriamali anasonga mbele kwa kupiga hatua katika safari ya kuisaka Tanzania ya Viwanda.

Amina anataja aina ya azma na mkakati iliyopo katika ufuatiliaji huo, utawainua kinamama wengi wajasiriamali na kutimiza lengo la Endless Success Foundation, kutaka kila mwanamke ainuke kiuchumi.

"Tunahitaji kuona kila mwanamke mjasiriamali mdogo anainuka kiuchumi. Kupitia kampeni hii, hatumwachi mtu nyuma na lengo ni tusonge mbele katika hatua nyingine," anasema Amina.

Mkurugenzi Amina anaendelea kwamba, mikakati waliopanga kwa ajili ya kundi hilo la wanawake ni pamoja na makundi mengine ambayo ni taasisi hiyo zilizojikita kuwasaidia kuwapa darasa la kila mara, wanaloamini litamsaidia kila mmoja.

Anasema baada ya mafanikio hayo, hatua inayofuata ni wanufaika kutarajia kwenda kuwafunza wenzao na ndio utakuwa mwanzo sasa wa mtandao wa kusambaza ujuzi katika maeneo wanakotoka, kueneza kazi ya Success Foundation.

Huo unaelezwa kuwa mkakati utakaosaidia, kwa sababu ni wenye manufaa kwa wengi kujikwamua na upotevu wa fedha za mtaji wa biashara, jambo ambalo ni kikwazo cha kusonga mbele katika biashara.

Matarajio ya Amina ni kwamba, kampeni ya ofisi yake itafika mbali katika mafanikio, kwa sababu kiasi kikubwa kwa sababu washiriki wengi wameonyesha mwitikio mzuri na kuelewa kile wanachofundishwa, ikiwamo kukubali kufanua kazi chini ya usimamizi wa muda wa taasisi hiyo.



Majumuisho ya mtazamio wa Mkurugenzi Amina, ni pongezi kwa serikali iliyopo madarakani, kutokana na anachokieleza kuwa nia ya kuwainua wajasiriamali, kupitia mikopo mbalimbali inayotolewa kwenye halmashauri husika.

Anasema kwa sasa, serikali iko mstari wa mbele katika kuangalia makundi maalumu ya kijamii yenye uhitaji, jambo linalozitia moyo taasisi zisizo za kiserikali, kuiga mfano wa kuyasaidia makundi hayo.

Kwa mujibu wa Amina, kutokana na jitihada hizo, nao Succes Foundation wamehamasika kuwa mstari wa mbele kuhakikisha wanatoa mchango wa kuyainua makundi hayo kiuchumi, ikiwamo nyanja za kibiashara wanakowanoa na kujiingizia kipato kinachowakimu.

**WAJASIRIAMALI**

Juliana Moses, ni mjasiriamali mmojawapo. Anakiri taasisi hiyo imekuwa mstari wa mbele kuwaunga mkono kinamama wajasiriamali, katika shughuli wanazofanya, kwa lengo la kujipatia kipato.

Pia anataja kuwa na marafiki kinamama wajane, wanaofanya kazi nao, pamoja kuhakikisha wanapata mitaji ya kuendesha biashara zinazowasaidia kuinua vipato vyao na familia kwa ujumla.

Mwingine, Fatuma Ally, anawaasa kinamama wenzake wasikubali maisha ya kujificha na badala yake, wajitokeze kuangalia fursa zinatolewa taasisi mbalimbali, kwa ajili ya kujiletea maendeleo mbalimbali ya familia, katika maisha ya kila siku.

BIASHARA

# Tigo yaeleza ubia wake na serikali intaneti ifike kijijini

## •Dira kufungua mlango wa uchumi

**Na MwandishiWetu**

"Siri ya mafanikio ni kuwezeshwa ushirikiano kati ya kampuni hiyo na serikali, kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF)... ruzuku inatolewa kuvutia waendeshaji kampuni za mawasiliano ya simu, zisogee katika maeneo ambayo kwa sasa hayavutii uwekezaji, kutokana na kuwapo mzunguko mdogo wa shughuli za kiuchumi."

DUNIANI kwa sasa suala la mawasiliano linapewa kipaumbele, kutokana na mchango wake katika kukuza uchumi wa mtumiaji mmoja mmoja.

Hiyo inatokana na uhalisia, mawasiliano yanatumika katika maeneo mengi hususani kwenye shughuli za kibiashara kila siku na kurahishisha mambo mbalimbali, ikiwamo biashara kwa makundi tofauti.

Ukuaji wa teknolojia, umefanya matumizi ya simu za mkononi na mtandao wa intaneti kugeuka msaada mkubwa katika kuwafikia kwa muda mfupi watu wengi, pia wafanyabiashara wakubwa kwa wadogo.

Mmoja wa wadau wa uunganishaji huo, ni kampuni ya simu za mkononi ya Tigo, ambayo inajigamba kwamba ndani ya kipindi cha miaka mitano sasa, imeshawaunganisha Watanzania kwa idadi ya maelfu kwenye huduma ya mawasiliano, hasa waliopo maeneo mbalimbali vijijini.

Mkuu wa Kitengo cha Mipango na Uhandisi kutoka Tigo, Emmanuel Mallya, anasema siri ya mafanikio ni kuwezeshwa ushirikiano kati ya kampuni hiyo na serikali, kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF).

Mallya anasema, serikali iliuanzisha mfuko wa UCSAF, kama namna ya kuziba pengo la mawasiliano lililopo kati ya Watanzania katika maeneo ya mijini na vijijini, ili kuchochea ukuaji uchumi.

"Takwimu zilizopo zinaonyesha kwamba tangu mwaka 2013, Tigo imeweza kuunganisha wakazi katika kata 111, kwa gharama ya Sh. bilioni 17," anasema Mallya na anaongeza:

"Katika awamu ya kwanza ya UCSAF, tuliunganisha wateja 190,942 katika kata 51, ambapo kata 27 kati ya hizo ziliunganishwa katika teknolojia ya mtandao wa 2G na kata 24 ziliunganishwa katika teknolojia ya mtandao wa 2G na 3G."

Anasema ni mchakato uliotumika kwa mtazamo kwamba huduma za mawasiliano kwa njia ya simu zitaharakisha uboreshaji hali ya uchumi katika maeneo ya vijijini.

"Kutokana na faida zitokanazo na uwekezaji unaofanywa na kampuni za mawasiliano kuchukua muda kupatikana, serikali ilibuni mfuko wa UCSAF ambao utakuwa unazipatia ruzuku kampuni za mawasiliano ya simu, kwa lengo la kurahisisha usambazaji wa huduma hii muhimu katika maeneo ya vijijini," anasema Mallya.

Anaongeza kuwa, ni ruzuku inatolewa kuvutia waendeshaji kampuni za mawasiliano ya simu, zisogee katika maeneo ambayo kwa sasa hayavutii uwekezaji, kutokana na kuwapo mzunguko mdogo wa shughuli za kiuchumi.



Mkurugenzi Mtendaji wa Tigo, Simon Karikari, akitia saini mkataba wa kuwezesha kusambaza mawasiliano kwa wote, walengwa wakuu wakiwa vijijini. Kushoto ni Ofisa Mtendaji Mkuu wa Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF), Mhandisi Peter Ulanga. **MPIGAPICHA WETU**

> **"Tumekuwa tunashiriki kwenye zabuni za UCSAF tangu mwaka 2012 na tutaendelea kufanya hivyo, kwa lengo la kuhakikisha maeneo ya vijijini yanaunganishwa kwenye huduma za mawasiliano," anasema Mallya.**

Mallya anasema, katika awamu ya pili ya mfuko wa UCSAF, Tigo iliunganisha wateja 57,543, waliosambaa katika kata 60, kati yake kuna kata 41 zimeunganishwa katika teknolojia ya mtandao wa '2G' na kata 24 kati ya hizo, zimeunganishwa katika teknolojia ya mtandano wa '2G' na '3G.'

Anasema, kasi hiyo ya usambazaji wa huduma za mawasiliano, imeongezwa nguvu na uwezo wa kampuni yake kusambaza teknolojia ya mtandao wa '2G' na '3G' kwa takribani asilimia 85 ya wakazi wa maeneo ya vijijini.

"Tumekuwa tunashiriki kwenye zabuni za UCSAF tangu mwaka 2012 na tutaendelea kufanya hivyo, kwa lengo la kuhakikisha maeneo ya vijijini yanaunganishwa kwenye huduma za mawasiliano," anasema Mallya.

Anafafanua kuwa mradi wa UCSAF ulikuwa ni ubunifu wa muhimu wa serikali, kwani unajenga na kuwezesha waendeshaji wa mitandao ya simu kutoa huduma kwa wakazi walioko vijijini, ambao ndio sehemu kubwa ya Watanzania.

Anajigamba kwamba hivi sasa wamekusudia kuziba pengo la mawasiliano kati ya maeneo ya mjini na vijijini kabla ya mwaka 2020, lengo ni kukuza maendeleo ya kijamii, kielimu na kiuchumi.

"Tunachukua fursa hii kuthibitisha kusudio letu la kuendelea kutimiza mkakati wetu wa kuwapatia wateja wetu huduma za kidigitali nchi nzima," alibainisha Mallya.

Anafafanua kuwa Tigo imewekeza kwa kiasi kikubwa katika uboreshaji miundombinu ya mawasiliano katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, dhumuni ni kuongeza ubora wa huduma za mawasiliano inazozitoa.

"Cha muhimu zaidi, uwekezaji umekusudia kuongeza kiwango cha ubora wa huduma kwa mteja anayetumia huduma za intaneti," anasema na kutaja

matumaini yaliyopo ni ongezeko la upatikanaji intaneti utakaotoa fursa kwa jamii za vijijini na kupata huduma muhimu kama za afya na elimu kwa njia ya mtandao.

Pia anataja matarajio mengine ya intaneti kwamba, itafungua milango ya huduma za malipo mbalimbali ya serikali kwa njia ya mtandao, jambo litakalobadilisha namna watu wanavyojifunza na kufanya biashara.

Kwa mujibu wa ofisa huyo, hatua hiyo ni msaada kwa nchi nzima kuweza kupata manufaa ya kiuchumi, kielimu na manufaa ya kijamii, kuwa kichocheo cha uharakishaji maendeleo na ustawi wa jamii.

# Ada ya taka yawa kikwazo

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

HALMASHAURI ya Jiji la Mbeya, imewahimiza wananchi katika kila kaya, maeneo ya biashara na sehemu za kutolea huduma za kijamii, kulipa ada ya kuzolea taka ili kupunguza malalamiko ya kuwapo taka kwenye baadhi ya maeneo.

Ofisa Habari wa Jiji la Mbeya, John Kilua, alisema jana kuwa uzoaji taka umekuwa ukilalamikiwa kwa sababu ya mwitikio mdogo wa wananchi kuchangia fedha za kuzolea taka na kusababisha mrundikano ambao unaweza kuhatarisha afya za wakazi wanaoishi jirani na maeneo ya kuhifadhia taka.

Kilua alisema kumekuwa na ongezeko kubwa la watu katikati ya jiji la Mbeya hali ambayo pia imeongeza uzalishaji wa taka unaofikia tani 270 hadi 300 kwa siku.

"Tulitoa maelekezo kuwa kila kaya, sehemu za kufanyia biashara na maeneo yanayotoa huduma za kijamii ada ni Sh. 1,000 kwa mwezi. Watu wanaona fedha hiyo ni kubwa na wanashindwa kutoa. Ukiangalia wao ndio wazalishaji wakubwa wa taka, hivyo hutuwezi kuweka mazingira safi kama baadhi hawawajibiki," alisema Kilua.

Alieleza changamoto nyingine kuwa ni utupaji holela wa taka kwenye maeneo yasiyoa rasmi hali inayowalazimu kuingia gharama za kukusanya.

Katika kukabiliana na changamoto ya mrundikano wa taka ndani ya jiji hilo, Kilua alisema magari ya kuzolea taka ni matano na wako mbioni kutengeneza magari mengine matatu huku akibainisha kuwa kuna vituo 90 vya kuhifadhia taka.

Mmoja wa wananchi kutoka kata ya Mwakibete, Stefano Abraham, alisema ili kuondoa mrundikano wa taka na kuzolewa kwa wakati serikali kupitia serikali za mitaa na kata zitunge sheria ndogo za usimamizi ambazo zitahimiza uzoaji na uthibiti wa utupaji holela.

Abraham alisema sheria hizo ndogo zitawapa nguvu viongozi wa serikali za mitaa kuwawajibisha wananchi wanaovunja sheria.

"Mji wetu unakua na taka zinaendelea kuzalishwa maeneo mengi, hazizolewi kwa wakati ili kukabiliana na hali hiyo kila mwananchi anapaswa kutambua umuhimu wa usafi kwa kuhakikisha anatunza mazingira," alisema Abraham.

# Wasionyonyesha waonywa kupata kansa

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MTAALAMU wa lishe amesema mwanamke asiyemnyonyesha mtoto anakuwa katika hatari ya kupatwa na saratani ya matiti.

Hayo yalisemwa juzi na Ofisa Lishe katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Mbeya, Dk. Charles Msigwa, alipokuwa akizungumzia juu ya athari zitokanazo na unyonyeshaji.

"Ziko athari zitokanazo na mama kutomnyonyesha mtoto ikiwamo kupata saratani ya matiti kwa sababu maziwa yanayotakiwa kutoka yanagandia ndani na kutengeneza mafuta.

Sambamba na hilo, alisema baadhi ya wanawake ni chanzo cha utapiamlo kwa watoto kutokana na kushindwa kufuata ushauri wa wataalamu wa afya juu ya namna ya kunyonyesha.

Alisema mtoto asiponyonyeshwa maziwa ya mama kwa kipindi cha miezi sita ya mwanzo, ana hatari kubwa ya kukosa virutubisho muhimu ambavyo vinahitajika kwa ajili ya ukuaji wake, hivyo kusababisha utapiamlo.

Alisema baadhi ya watoto wanaopimwa kliniki katika hospitali hiyo afya zao si za kuridhisha kutokana na wengine kudhoofu na wengine kuwa na tumbo kubwa.

Dk. Msigwa alisema miongoni mwa sababu zinazochangia utapiamlo kwa watoto ni baadhi ya kinamama kuwa na shughuli mbalimbali za uzalishaji na ujasiriamali, hatua inayosababisha kushindwa kumaliza miezi sita wakihofia kukwamisha kazi zao.

"Mtoto asiponyonyeshwa kwa miezi sita ya mwanzo anaweza kupata utapiamlo. Tumejitahidi kutoa elimu ya unyonyeshaji kwa kinamama, lakini wengine hawazingatii na matokeo yake watoto wanapata maradhi," alisema Dk. Msigwa.

Mmoja wa wanawake kutoka Mtaa wa Juhudi jijini Mbeya, Jenifer Kabuka, alisema kinachosababisha kuwaachisha maziwa watoto ni hali ngumu ya maisha, hivyo hulazimika kwenda mashambani au kufanya shughuli za ujasiriamali ili kupata fedha za kuendesha maisha.

Kabuka alisema kwa sababu ya kuwa shughuli nyingi za kujiingizia kipato, watoto hunyweshwa uji ambao humfanya kuacha kusumbua.




Wakazi wa jijini wakiwa wameegesha magari yao kando ya Barabara ya Magogoni, nje ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, jijini Dar es Salaam jana, licha ya kuwapo kibao cha ilani ya katazo. **PICHA: JOHN BADI**

# Watakiwa kuchangamkia maonyesho biashara

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

WAFANYABIASHARA katika mikoa ya Nyanda za Juu Kusini wamehamasishwa kushiriki maonyesho ya tatu ya kibiashara yajulikanayo kama 'Biashara Bazaar' ambayo yanatoa fursa ya kuonyesha na kuuza bidhaa jijini Mbeya.

Mratibu wa Maonyesho hayo, Muhsin Mkongo, alisema jana kuwa mwaka huu maonyesho yatakuwa ya tofauti kwa sababu wafanyabiashara wamejifunza ubunifu mpya wa kutengeneza bidhaa kwa kuzingatia mabadiliko ya teknolojia.

Alisema maonyesho hayo ambayo yatadumu kwa muda wa siku tano, yataanza Septemba 25 hadi 29 katika viwanja vya OTTU jijini Mbeya na kuhusisha wadau mbalimbali zikiwamo taasisi za serikali na Chama cha Wafanyabiashara wenye Viwanda na Kilimo Tanzania (TCCIA) Mkoa wa Mbeya.

"Tunawahamasisha wafanyabiashara wote katika mikoa ya Nyanda za Juu Kusini na maeneo mengine kutumia maonyesho hayo kutangaza bidhaa zao. Naamini watapata wateja lakini pia watabadilishana uzoefu katika shughuli zao," alisema Mkongo.

Aliongeza kuwa wadau na wafanyabiashara wakubwa nchini nao wamealikwa kushiriki maonyesho hayo kwa lengo la kuwahamasisha wajasiriamali wenye ndoto za kuwa wafanyabiashara wakubwa kujifunza njia za kisasa katika uzalishaji wa bidhaa na kutafuta masoko.

Ofisa Mtendaji wa TCCIA Mkoa wa Mbeya, Emile Malinza, alisema maonyesho hayo ni makubwa kwa sababu yatawahusisha wafanyabiashara kutoka maeneo mbalimbali.

Alisema wameandaa eneo maalum kwa ajili ya wafanyabiashara na vikundi mbalimbali vikiwamo vya wanawake, vijana na walemavu walionufaika na mikopo isiyo na riba inayotolewa na halmashauri, kuwahamasisha wengine kutumia fursa hiyo kupata fedha za kuendeshea biashara zao.

Alisema mpaka sasa Sh. milioni 200 zimetolewa na halmashauri za mkoa wa Mbeya kwa sharti lisilokuwa na riba na kuwanufaisha watu wenye ulemavu, vijana na wanawake ambao tayari walijiunga kwenye vikundi na kukidhi vigezo vya kupata mikopo.

Ofisa Biashara Mkoa wa Mbeya, Stanley Kibakaya, aliwahamasisha wafanyabiashara kutumia maonyesho hayo kutangaza na kuuza bidhaa zao, lakini kuongeza elimu na kuboresha uzalishaji.





# Ujerumani yamwaga mabilioni sekta afya

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WIZARA ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, imetia saini mkataba wa makubaliano na serikali ya Ujerumani wa Sh. bilioni 26.6 ambao umejikita katika maeneo makuu manne yanayolenga kuimarisha sekta ya afya nchini.

Akizungumza jana baada ya kusaini makubaliano hayo, Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Dk. Zainab Chaula, alisema hatua hiyo ni mwendelezo wa uhusiano ulioanza tangu mwaka 1961.

Dk. Chaula alisema tangu 2003 mkataba huo ni wa tano na hufanyika kila baada ya miaka mitatu.

Alisema mkataba huo kuwa umejikita katika maeneo ya kuimarisha afya ya msingi ngazi ya halmashauri katika zahanati na vituo vya afya.

"Mkataba huu umejikita katika maeneo makuu manne ambayo ni uimarishaji wa taarifa zetu, kuimarisha afya ya mama na mtoto, uzazi wa mpango bima kwa wajawazito na utawala bora," alisema.

Katibu mkuu huyo alisema katika suala la utawala bora linalenga namna ya kuzitumia fedha hizo kulingana na kanuni na taratibu za nje.

"Huu ni mwendelezo wa miradi inayofanyika ya kuboresha sekta ya afya na mtakumbuka kuna vituo vingi tumefanya ukarabati na tulianza mwaka 2017," alisema.

Dk. Chaula alisema hadi sasa kuna vituo 470 katika ngazi ya zahanati, vituo vya afya na hospitali za wilaya na serikali iliwekeza Sh. bilioni 100.5 kwa hospitali za halmashauri.

Hata hivyo, alisema wamekubaliana kutumia mfumo wa 'Force Account' ambao ulileta mafanikio makubwa katika ujenzi wa vituo vya afya badala ya kutumia makandarasi.

"Hawa wenzetu walikuwa wanatumia makandarasi wao, fedha wanakaa nazo wao. Tulikuwa tunajaribu kuweka makubaliano kwamba tutafurahi hizi fedha kama zitatolewa kwa wakati mmoja ili kuweza kusimamia kwa kutumia mfumo wa 'Force Account'," alisema.

Aliahidi kuhakikisha fedha hizo zinaleta matokeo makubwa kwa kipindi kifupi.

"Sekta ya afya tunafanya vizuri. Kwa sasa wanaokwenda kujifungulia vituo vya afya inakaribia kuwa asilimia 80. Tuimarisha utoaji huduma," alisema.

Pia alisema wanaendelea kuweka mikakati mbalimbali kuhakikisha kinamama wote wanajifungulia katika vituo vya kutolea huduma.

# Jafo aomba wasomi kuchangia elimu

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Seleman Jafo, amewaomba wasomi na makundi mengine kuendelea kuunga mkono juhudi za serikali katika kuchangia sekta ya elimu nchini.

Ombi hilo alilitoa jana jijini hapa alipokuwa akipokea nakala za malipo ya benki yenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 3.5 kutoka Taasisi ya Dk. Msuya ikiwa mchango wa kusaidia ada na sare za shule kwa wanafunzi wa kike waliofaulu kujiunga kidato cha tano kutoka katika mazingira magumu.

Jafo aliwaomba wasomi na makundi mbalimbali kujitokeza kusaidia jamii katika sekta ya elimu ili kuwezesha watoto hao kutimiza ndoto za kufikia malengo yao ya kupata elimu.

"Ninawashukuru sana Taasisi ya Dk. Msuya kwa kuona umuhimu wa kuunga mkono juhudi za serikali katika kutoa elimu hapa, nawaomba wasomi wengine nchini kujitokeza kusaidia kuchangia elimu," alisema.

Alisema kupitia msaada uliotolewa na taasisi hiyo, wanafunzi wanaotoka kwenye mazingira magumu watatimiza ndoto zao za kupata elimu ya kidato cha tano na sita.

Jafo alibainisha kuwa serikali ilipotangaza kutoa elimu bila malipo kuanzia msingi hadi kidato cha nne kuwa kila kitu ingekuwa bure kuna mahitaji mengi ya wanafunzi.

"Elimu bila malipo ilitafsiriwa vibaya, hii si sawa maana ya elimu bila malipo ni kuwa gharama ambazo walikuwa wakilipa wazazi wa watoto hao kwa ngazi zilibebwa na serikali, hivyo isitafsiriwe tofauti," alisema.

Aidha, Jafo alisema kuna changamoto kwa baadhi ya wanafunzi wanaotoka kwenye mazingira magumu waliochanguliwa kujiunga na kidato cha tano hadi cha sita kutokana na kukosa mahitaji muhimu kama karo na sare za shule.

Kwa upande wake, Dk. Ombeni Msuya ambaye ni Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Dodoma alisema taasisi hiyo ilianzishwa mwaka 2018 kwa lengo la kuwasaidia wanafunzi wa kike waliofaulu kwenda kidato cha tano wanaotoka kwenye mazingira magumu.

Alisema sababu ya kuanzisha taasisi hiyo ni kutokana na changamoto ya mahitaji waliyokuwa wakipata wanafunzi hao ambao walichaguliwa kujiunga na kidao cha tano.

Dk. Msuya alibainisha kuwa fedha hizo zinatokana na yeye kujiwekea akiba na kuchangisha kwa marafiki zake kwa lengo hilo na mpaka sasa wana zaidi ya Sh. milioni 10.

Alisema karatasi za malipo ya benki walizokabidhi kwa Waziri Jafo huyo zinathamani ya Sh. milioni 3.5 kutoka mikoa 23 na bado akiba ipo, hivyo wanakaribisha maombi ya wanafunzi wengine kupitia wakurugenzi wa halmashauri husika.




Kamanda wa Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani Wilaya ya Dodoma Mjini, ASP Mathew Ntakije, akizungumza kwenye ufunguzi wa mafunzo ya alama za barabarani kwa ajili ya watu wenye ulemavu, jijini Dodoma jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**.

# Wenye ulemavu kuchangamkia mikopo

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WATU wenye ulemavu nchini wametakiwa kuchangamkia fursa ya mikopo ya asilimia mbili, inayotolewa na halmashauri mbalimbali ili kuanzisha miradi itakayowasaidia kujikwamua kiuchumi.

Rai hiyo ilitolewa jana na Mwenyekiti wa Kamati ya Taifa ya Usalama Barabarani kwa Watu wenye Ulemavu, Jutoram Kabatele, alipokuwa akizungumza na watu wenye ulemavu wa aina mbalimbali katika mafunzo ya alama mpya sita za usalama barabarani.

Alisema wenye ulemavu wanatakiwa kuwa wabunifu katika kuanzisha miradi itakayowawezesha kiuchumi.

"Serikali imewatambua watu wenye ulemavu nchini na kuwatengenezea hii fursa ya mikopo ya asilimia mbili ili kujikwamua kiuchumi, hivyo changamkieni hii fursa na kuacha kulalamika," alisema.

Pia aliwataka watu wenye ulemavu ambao watakopa fedha hizo kuhakikisha wanarejesha ili wengine wapate fursa hiyo.

"Mnapokopa mikopo hii jamani mlipe kwa wakati na si kusingizia ulemavu wetu na kuacha kulipa mikopo hii ya asilimia mbili inayotolewa na serikali," alisema Kabatele.

Aidha, aliwataka wenye ulemavu kuacha tabia ya kubaguana bali washikamane na kubadili mitazamo yao.

"Ulemavu wetu ni wa maumbile na si tuwe na ulemavu hadi akili zetu. Lazima tubadilike tuwe na mshikamao ili kujikwamua kiuchumi bila kujali aina ya ulemavu wetu," alisema.

Akifungua mafunzo hayo, Ofisa Usalama Barabarni wa Wilaya ya Dodoma, Mrakibu Msaidizi (ASP) Mathew Ntakije, alisema katika baadhi ya ofisi za umma bado kuna changamoto za miundombinu rafiki kwa watu wenye ulemavu.

Pia alisema katika matukio ya ajali nyingi ambazo zimekuwa zitokea, sababu kubwa ni watu kutotambua alama za usalama barabarani, hivyo kuna aja ya kuendelea kutolewa kwa elimu.

Hata hivyo, ASP Ntakije aliwataka watu wanaohusika na suala la utoaji wa leseni za udereva kuangalia vigezo kwa watu wenye ulemavu ambao wanastahili kupatiwa ili kuondoa malalamiko kwa kundi hilo.



# Nigeria yatua Zanzibar kujifunza

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MWENYEKITI wa Kamati ya Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (Tasaf) Zanzibar, Ayoub Mohamed Mahmoud, amesema mfuko huo unatarajia kuzigusa shehia zote 388 visiwani hapo, ili kuzihudumia kaya maskini.

Utekelezaji huo utafanyika kwa mwaka 2019/2020 chini ya programu ya Tasaf awamu ya nne.

Alisema hayo wakati akizungumza na timu ya waratibu wakuu wa majimbo 36 ya Nigeria waliowasili nchini kwa ziara maalum ya kujifunza mafanikio ya Tasaf.

Mohmoud ambaye ni Mkuu wa Mkoa Mjini Magharibi aliwaeleza waratibu hao waliofika Zanzibar kujifunza mpango maalum wa kuhudumia kaya maskini kwamba shehia zinazohudumiwa kwa sasa zimeshafikia 233 kati ya 388.

Alisema katika mwelekeo huo hakutakuwa na eneo ambalo halitaguswa kwenye masuala ya kuzifikia kaya maskini, jukumu litakalokwenda sambamba na mapitio ya shehia ambazo zinaendelea kuhudumiwa kwani zina kigezo cha kuingia katika kaya maskini, lakini hazikuguswa kutokana na ufinyu wa bajeti katika awamu iliyopita.

Mohmoud alisema kwamba mapitio hayo yatachambua na kuzitathmini shehia ambazo zilikuwa na kaya maskini lakini kwa sasa zimekuwa kiuchumi.

Mwenyekiti huyo wa kamati ya mfuko wa Tasaf Kisiwa cha Unguja aliwafahamisha waratibu wakuu wa majimbo 36 ya Nigeria kwamba yapo mafanikio makubwa yaliyopatikana katika uimarishaji wa ustawi wa jamii kupitia Tasaf.

Alisema uundwaji wa vikundi vya kijamii katika shehia mbalimbali Unguja na Pemba umesaidia kuibua miradi tofauti iliyowezesha wananchi kiuchumi na hatimaye kupiga hatua kubwa ya mapambano kumaliza umaskini.

Aliwaambia sekta ya kilimo imeleta faida kubwa ndani ya Tasaf ingawa bado zipo baadhi ya changamoto zinazowakazwa wananchi hasa kwenye sekta ya afya na elimu.

Kiongozi wa timu ya Wanigeria Naibu Mkurugenzi wa Taasisi ya Ustawi wa Jamii, Garba Baba Gambo, alisema ziara yao imelenga kuona mafanikio makubwa yaliyopatikana katika mpango wa kuhudumia kaya maskini.

Alisema Tanzania ni miongoni mwa nchi chache duniani zilizofanya vizuri na kuchukua nafasi ya juu katika kuendeleza mpango huo, huku Visiwa vya Zanzibar vikifanya vizuri zaidi ikilinganishwa na Tanzania Bara.

Alisema ujio wao utawapa nafasi ya kuibua njia zitakazowasaidia kupata mbinu za mwelekeo wa kupambana na changamoto zinazowakabili katika kutoa huduma kwa wananchi wao takribani milioni 200 wanaoishi kwenye majimbo 36.

Akitoa taarifa Mwakilishi wa Mfuko wa Tasaf wa Kanda, Saida Saleh Adam, alisema zaidi ya Sh. bilioni 27 zimeshatolewa katika mpango maalum wa kuhudumia kaya maskini Unguja na Pemba.



Balozi Mdogo wa Jamhuri ya Watu wa China aliyepo Zanzibar, Xie Xiaowu (kulia), akicheza ngoma ya Msewe, iliyopigwa na kikundi cha Sanaa cha Taifa, wakati wa ufunguzi wa mafunzo ya mapishi na ukarimu yanayoendeshwa na wakufunzi kutoka Serikali ya China, Kikwajuni Mjini Zanzibar juzi. **PICHA: IKULU ZANZIBAR**.

# Wafunzwa ili kuongeza tija

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

HATUA ya serikali ya Zanzibar, kuiomba China kufanya mafunzo ya upishi na ukarimu Zanzibar, inatoa fursa ya watumishi wa umma kujifunza kutekeleza matakwa ya kisheria na kanuni za utumishi wa umma.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Issa Haji Gavu, alisema katika ufunguzi wa mafunzo ya upishi na ukarimu, yanayoendeshwa na wakufunzi kutoka China.

Mafunzo hayo yanayowashirikisha watumishi 45 wa umma, yatafanyika kwa wiki nne, yakiwa na lengo la kuwaongezea ufanisi, uwajibika na kuleta tija katika utumishi wa umma.

Akizungumza na washiriki wa mafunzo hayo, Gavu alisema serikali kuomba kufanyika mafunzo hayo nchini kunalenga kuwapa fursa watumishi wengine zaidi kupata fursa hiyo kwa vitendo katika mazingira wanayofanyia kazi.

"Napenda kukusitiza kwa washirki wa mafunzo kuiunga mkono na kuthamini dhamira njema ya mheshimiwa Rais ya kuhakikisha watumishi wa umma wanapatiwa mafunzo ya muda mrefu na mfupi," alisema Gavu.

Aliwataka washiriki wa mafunzo hayo kudumisha nidhamu katika kipindi chote cha masomo na kujenga ushirikiano na wakufunzi hao pamoja na kubeba dhima ya kuwa walimu kwa watumishi wengine waliokosa fursa hiyo.

Alisema mafunzo hayo sio tu kuwa yatawanufaisha watumishi na kupata maarifa mapya katika kuwahudumia viongozi wakuu na vitengo maalum, lakini pia yatachangia dhamira ya kuimarisha sekta ya utalii nchini.

Aidha, alisema hatua hiyo itawapa fursa wakufunzi hao kutoka China kuyafahamu vyema mazingira ya Zanzibar na kupata fursa ya kujifunza mila, silka na utamaduni pamoja na kuona vivutio mbali mbali vya kitalii.

"Tunategemea wenzetu watakapoondoka watakuwa mabalozi wazuri wa kutangaza utajiri wa vivutio vya utalii tulivyonavyo, hivyo kuimarisha sekta ya utalii, ikizingatiwa kuwa China ni eneo jipya tunalotarajia kupokea watalii wengi zama hizi," alisema Gavu.

Waziri Gavu alipongeza uhusiano na ushirikiano wa muda mrefu kati ya China na Zanzibar na Tanzania kwa ujumla, sambamba na hatua ya taifa hilo kusaidia katika uimarishaji wa sekta mbalimbali za maendeleo na ukuaji wa uchumi.

Aliishukuru Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China pamoja na Taasisi ya 'China National Research Institute of Food and Fermentation Industries Corporation Limited kwa kufanikisha mafunzo hayo.

Balozi mdogo wa China aliyeko Zanzibar, Xie Xiaowu, alisema mafunzo hayo yatawawezesha kuwajengea uwezo washiriki, sambamba na kuchochea ukuaji wa uchumi na ustawi wa jamii.

Vile vile aliipongeza Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa ushirikiano mkubwa uliowezesha kufanikisha kufanyika kwa mafunzo hayo, hivyo kupanua wigo wa uhusiano na ushirikiano wa muda mrefu kati ya China na Zanzibar.

# Benki yajitosa kuchangia elimu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KATIKA kuunga mkono jitihada za serikali ya Zanzibar kukuza elimu hasa ya sayansi na masomo ya kibiashara, Benki ya Watu wa Zanzibar, kwa mara nyingine inatarajia kuwazawadia wanafunzi wa kidato cha sita waliofanya vizuri katika mitihani ya kitaifa.

Akizungumza na waandishi wa habari Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa benki hiyo, Khadija Shamata Mzee, alisema taasisi hiyo ina utaratibu wa kuwazawadia wanafunzi bora kila mwaka na sasa muda umewadia.

Alisema mwaka jana waliwatunza wanafunzi 196 wa masomo mbalimbali lakini mwaka huu wamepanga kuwapa zawadi wa masomo ya sayansi na biashara ili kutoa hamasa kwa wanafunzi kupenda kuyasoma masomo hayo.

"Tunatarajia kuwazawadia wanafunzi wa kidato cha sita waliofanya vizuri leo Ijumaa," alisema Mzee.

Aidha, alieleza kuwa benki hiyo inakusudia pia kuisaidia shule za mwisho zilizofanya vibaya katika mitihani ya kidato cha nne hasa kwa Sekondari ya Kijini ambayo mazingira yake ni magumu.

"Kijini imekuwa ikifanya vibaya katika mitihani ya taifa hivyo tumeamua kuisaidia kutokana na mazingira magumu," alisema Mzee.

# Mahakamani tuhuma kukwepa kodi bil. 2.5/-

**Na Friday Simbaya,** IRINGA

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA), mkoani Iringa imewafikisha wafanyabiashara wawili wa mbao mahakamani kwa tuhuma ya kukwepa na kutolipa kodi ya mapato ya zaidi ya Sh. bilioni 2.5.

Akisoma mashtaka hayo mbele ya Hakimu Mkazi wa Mahakama ya Wilaya ya Iringa, Magolyo Paul, Mwendesha Mashtaka wa TRA, Juma Kisongo, alidai washtakiwa hao wanatuhumiwa kutenda makosa mbalimbali yakiwamo kukwepa kodi na kutokulipa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT).

Alidai washtakiwa kwa nyakati tofauti walishindwa kulipa kodi mbalimbali kwa mamlaka na kuikosesha mapato ya zaidi ya Sh. bilioni 2.5.

Watuhumiwa hao wametajwa kuwa ni Heavy Sanga na Emmanuel Mtokoma, wafanyabiashara wa mbao wa mjini Mafinga na walikana mashtaka yao na kunyimwa dhamana kutokana na mazingira ya kesi.

Washtakiwa wanatetewa na Wakili Moses Ambindwile, walirudishwa rumande hadi Septemba 16, mwaka huu.

Hakimu wa Mahakama ya Hakimu Mkazi, Magolyo alisikiliza pande mbili za utetezi na Jamhuri na kuahirisha kesi hiyo hadi Septemba 16 kwa ajili ya kutolea ufafanuzi suala ya dhamana kwa washtakiwa baada ya upande wa Jamhuri kupinga dhamana kulingana na mazingira ya kesi.

Mamlaka hiyo inaendelea na operesheni kwa kushirikiana na vyombo vingine vya usalama ya kuwabaini wafanyabiashara ya mbao ambao baadhi yao sio waaminifu.

Meneja wa TRA mkoani Iringa, Lamson Tulyanje, alisema kwa takriban wiki mbili mamlaka hiyo kwa kushirikiana na vyombo vingine vya usalama, iliendesha msako wa kukagua nyaraka mbalimbali zinazohusiana na kodi kwenye magari ya mizigo hasa yale yanayobeba mbao.

Alisema katika msako huo walibaini kuwapo na udanganyifu wa wafanyabiashara wa kununua risiti kutoka kwa watu wanaouza risiti yaani madalali, wanaonunua mbao sehemu nyingine na risiti sehemu nyingine.

Tulyanje alisema kumekuwa na biashara ya kuuza risiti kinyume na risiti ya kielektroniki (EfD) kwa kutumia vishoka.

Alitoa rai kwa wafanyabiashara na wananchi kulipa kodi kwa usahihi ili serikali iweze kukusanya mapato kwa maendeleo ya uchumi.

Aliwataka wafanyabiashara na Watanzania kwa ujumla kujenga tabia ya kulipa kodi kwa kuwa ndiyo msingi wa maendeleo ya nchi yoyote duniani.

Tulyanje aliongeza kuwa watu wakilipa kodi kwa usahihi na serikali ikakusanya vizuri, inaweza kuhudumia jamii kwa mambo mbalimbali ikiwamo miundombinu, afya, maji na elimu.



Mkuu wa Kitengo cha Masoko na Mawasiliano wa Benki ya KCB, Christina Manyenye (kulia), akizungumza na wafanyabiashara zaidi ya 300, wakati wa kongamano la klabu ya biashara ya benki hiyo, jijini Dar es Salaam kwa dhumuni la kutoa mafunzo katika nyanja mbalimbali za kuendesha biashara na fursa ndani ya klabu hiyo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**.

# KCB kukutanisha wafanyabiashara zaidi ya 300

**Na Mwandishi Wetu**

WAFANYABIASHARA wadogo na wa kati zaidi ya 300 wanatarajiwa kukutanishwa na Benki ya KCB Tanzania katika kongamano litakalofanyika jijini Dar es Salaam.

Kongamano hilo linatokana na Programu KCB Biashara Club iliyobuniwa na benki hiyo kwa dhumuni la kutoa fursa mbalimbali kwa wafanyabiashara zikiwamo mafunzo ya uendeshaji biashara, kuwapa wafanyabiashara jukwaa la kushirikiana pamoja na kuwakuzia mtandao wa masoko ndani na nje ya Tanzania.

Taarifa ya benki hiyo ilieleza kuwa KBC imeendelea kuonyesha dhamira yake ya kukuza biashara katika sekta ya wafanyabiashara wadogo na wakati (SME) kwa kutoa huduma bora za kibenki pamoja na kuwaonyesha mbinu za kukuza mitaji ya shughuli zao za kibiashara.

Vile vile, mwezi Machi 2019, Benki ya KCB iliendesha

kongamano kama hilo jijini Arusha kwa wafanyabiashara walio katika sekta ya utalii.

Akiongea wakati wa kufungua semina hiyo, Mkuu wa Masoko na Mahusiano, Christine

Manyenye, alisema Benki ya KCB imefanya juhudi za kuwaleta wadau kama Injinia Jane Kadoda kutoka Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira (NEMC), ambaye alizungumzia athari za biashara kwa mazingira pamoja umuhimu wa kutii sheria za kulinda mazingira zilizowekwa na serikali.

Kwa upande wake mdau kutoka European Investment Bank (EIB), Fasili Boniface, alizungumzia umuhimu wa kuweka kumbukumbu za kifedha na jinsi ya kuainisha matumizi ya binafsi na ya kibiashara.

Naye Saada Sipemba kutoka Sadio Travel and Tourism ambaye ni mtaalamu wa safari za kibiashara alizungumzia fursa za kibiashara zinazopatikana nchini China na juhudi za benki hiyo kuhakikisha inawatengenezea wateja wake mianya ya kuchukua fursa hizo kwa urahisi.

# Viongozi ACT-Wazalendo mahakamani

**Na Steven William,** MUHEZA

JESHI la Polisi mkoani Tanga, linawashikilia viongozi wanne wa chama cha siasa cha ACT- Wazalendo kwa kosa la kufanya mkusanyiko wa watu bila kuwa na kibali.

Viongozi hao walifikishwa katika Mahakama ya Wilaya ya Muheza kwa kusomewa shtaka lao.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Tanga, Edward Bukombe, alithibitisha kukamatwa kwa viongozi hao na kueleza kuwa viongozi hao na wanachama wao walianza kufanya mkutano wa ndani na hatimaye walihamia nje na kukusanya watu bila kibali na polisi walipata taarifa na kwenda kuwakamata.

Bukombe aliwataja waliokamatwa na kufikishwa mahakamani kuwa ni Katibu wa ACT-Wazalendo Mkoa wa Tanga, Abrahamani

Lugone, Katibu wa chama hicho Jimbo la Muheza, Hamadi Chombo, Mjumbe Jimbo la Muheza, Jamila Makalachilo na Mwenyekiti wa

chama hicho Mkoa wa Tanga, Hawa Saidi.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Wanawake wa ACT-Wazalendo, Mkoa wa Tanga, Rehema Ally, alisema viongozi hao walikamatwa wakati wanafungua ofisi ya chama hicho zilizopo katika Kata ya Tanganyika, Orofea wilayani Muheza.

Alisema wakati mgeni rasmi Katibu Mwenezi wa ACT-Wazalendo kutoka taifa, Addo Shaibu, anapandisha bendera ya chama hicho kama ishara ya kufungua ofisi mpya, ghafla walitokea polisi na hatimaye kuwakamata.

Alisema kuwa baada ya maelezo viongozi hao wamefikishwa katika Mahakama ya Wilaya ya Muheza kujibu shtaka hilo

na wanatetewa na Wakili wa chama hicho kutoka jijini Dar es Salaam, Bonifasia Mapunda.

Rehema alisema huo ni mwendelezo wa kuzima vyama vya siasa katika Serikali ya Tanzania na Katiba inasema kuna vyama vingi, lakini hawafuati sheria ya vyama vingi.

Kesi hiyo inasikilizwa na Hakimu wa Mahakama ya Wilaya ya Muheza, Liliani Lutehangwa na washtakiwa wote wapo nje kwa dhamana.

## HABARI KIMATAIFA

# Ofisi ya Rais yatuhumiwa upotevu mabilioni

**KINSHASA, Congo**

KESI ya kupotea kwa Dola milioni 15 imezua hali ya sintofahamu Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), huku mashirika ya kiraia yakiomba uchunguzi wa kina ufanyike ili kupata ukweli wa mambo.

Wakati huo huo, wakosoaji wa Mkurugenzi wa Ofisi ya Rais, Vital Kamerhe, wanamuhusisha kiongozi huyo kwa kesi hiyo, licha ya yeye kukana tuhuma hizo.

Kupotea kwa fedha hizo kumeibua maswali mengi kati ya mashirika mbalimbali na wakosoaji wa serikali ya DRC.

Kamerhe ambaye wakosoaji wake wanamwita rais wa pili amepuuzia mbali madai hayo akisema kuwa lengo la wapinzani wake ni kumchafua tu.

Kamerhe ni miongoni mwa viongozi wanne ambao Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali unawahusisha katika kesi hiyo ya kupotea kwa dola milioni 15.

Mwezi mmoja na nusu baada ya kesi hiyo kuanza, Rais wa DRC, Felix Tshisekedi, hajatoa tamko lolote kuhusu suala hilo. Ukimya ambao wanaharakati wa mashirika ya kiraia wanalaani.

Wanaharakati hao wanamkumbusha Rais Tshisekedi kuhusu ahadi yake ya kupambana dhidi ya ufisadi kuwa ni moja wapo ya vita kwa muhula wake.

Ofisi Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, tayari imefungua uchunguzi wa awali. Katika mahojiano na Gazeti la Jeune Afrique, Kamerhe, Mkurugenzi wa Ofisi ya Rais Tshisekedi, amefutilia mbali kuhusika kwake katika kesi hiyo na amekanusha suala la kupotea kwa fedha hizo.

Kamerhe pia alisitisha uchunguzi mwingine uliozinduliwa na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, ikiwa ni pamoja na uchunguzi kuhusu matumizi yote kwenye wizara mbalimbali tangu Rais Tshisekedi kuchukuwa madaraka, kwa mujibu wa vyanzo kadhaa kutoka serikalini.

**RFI**

**Ofisi Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, tayari imefungua uchunguzi wa awali. Katika mahojiano na Gazeti la Jeune Afrique, Kamerhe, Mkurugenzi wa Ofisi ya Rais Tshisekedi, amefutilia mbali kuhusika kwake katika kesi hiyo na amekanusha suala la kupotea kwa fedha hizo.**

# Familia ya Mugabe yageuka 'mbogo' kisa mazishi

**HARARE, Zimbabwe**

FAMILIA ya aliyekuwa Rais wa Zimbabwe, Robert Mugabe, imesema imeshtushwa kwa kutoshauriwa na serikali kuhusu mipango ya mazishi ya baba yao.

Mugabe, alifariki wiki iliyopita akiwa na umri wa miaka 95, wakati akiwa anapatiwa matibabu katika hospitali moja huko Singapore.

Mwili wake unatarajiwa kupewa heshima za mwisho kitaifa katika uwanja wa soka katika mji mkuu wa Zimbabwe, Harare.

Familia yake na serikali bado zinatofuatiana kuhusu sehemu atakapozikwa Mugabe.

Familia ya Mugabe inasema mwili wake utalazwa nyumbani kwake katika kijiji cha Kutama Jumapili usiku, na atazikwa katika mazishi ya faragha.

"Mwili wake utapewa heshima za mwisho Kutama Jumapili usiku na kufuatiwa na mazishi ya faragha - pengine Jumatatu au Jumanne na sio katika makaburi ya kitaifa ya mashujaa wa uhuru. Huo ni uamuzi wa familia nzima," alisema binamu yake, Leo Mugabe.

Rais wa Zimbabwe, Emmerson Mnangagwa, alimtangaza Mugabe kuwa shujaa wa kitaifa baada ya kifo chake, na kuashiria kuwa anapaswa kuzikwa katika eneo hilo la kitaifa.

Waziri wa Elimu, Paul Mavhima, alisema hakuna shaka Mugabe anastahili kuzikwa kama shujaa wa kitaifa.

"Mtu muhimu wa aina hiyo, ambaye mazishi yake yatahudhuriwa na zaidi ya viongozi 50 wa taifa na wa zamani. Mwasisi wa taifa hili hakupaswi kuwa na majadiliano ya hilo, hakupaswi kuwa na mzozo wowote. Uamuzi unapaswa kuwa wa wazi, anastahili kuzikwa katika kaburi la kitaifa," alisema Mnangagwa na kuongeza:

"Itakuwa ni makosa makubwa kuwa na mpiganiaji uhuru wa taifa hili, mhamasishaji mkubwa wa raia wa Zimbabwe kuzikwa katika eneo lingine kando na kaburi la itaifa. Wito ni kuiomba familia, huyu sio wenu tena, ni kiongozi wa taifa. Ni kiongozi wa Afrika. Ni kiongozi duniani, anastahili kupewa heshima anayoistahili. Kwa hivyo atazikwa katika kaburi la kitaifa."

"Tumetambua na kwa wasiwasi mkubwa, namna serikali ya Zimbabwe ilivyoratibu mpango wa mazishi ya marehemu Robert Gabriel Mugabe pasi kuishauri familia yake marehemu iliyo na jukumu la kuwasilisha maombi yake ya mwisho kuhusu mazishi yake," familia hiyo ilisema katika taarifa na kuongeza:

"Kama familia yake ya karibu, tumetambua na kwa mshtuko kuwa serikali ya Zimbabwe inajaribu kutubembeleza tukubali ratiba ya mazishi ya marehemu Robert Gabriel Mugabe ambayo inakwenda kinyume na maombi yake ya kutaka mwili wake uhifadhiwe."

Taarifa hiyo inaongeza kuwa mojawapo ya maombi ya marehemu ilikuwa ni kutaka mkewe, Grace Mugabe, asiondoke karibu na jeneza la Mugabe wakati wa mazishi mpaka atakapozikwa.

Familia ya Mugabe inasemekana kuwa na uchungu kwa namna Mugabe alivyotimuliwa na aliyekuwa mshirika wake Mnangagwa miaka miwili iliyopita.

Mugabe alimfuta kazi Mnangagwa mwaka 2017, katika kile ambacho wengi waliamini ni njia ya kumtayarisha mke wake kumrithi.

Mwili wa Mugabe utalazwa katika uwanja wa michezo wa Rufaro Alhamisi kabla ya kuelekea katika makazi yake ya Zvimba kwa misa ya wafu.

Mugabe alikuwa kiongozi wa kwanza wa Zimbabwe baada ya taifa hilo kupata uhuru mwaka 1980.

**BBC**



Mwili wa aliyekuwa Rais wa Zimbabwe, Robert Mugabe, ukiwasili katika uwanja wa ndege wa taifa hilo ukitokea Singapore, anatarajiwa kuzikwa siku ya Jumapili. **PICHA: ALLIANCE**

# Wanigeria 188 wawasili nyumbani

**LAGOS, Nigeria**

KUNDI la kwanza la raia wa Nigeria waliokimbia vurugu zinatotokana na chuki dhidi ya wageni nchini Afrika Kusini limewasili mjini Lagos.

Raia hao wapatao 188 waliokuwa ndani ya ndege wakitoka jijini Johannesburg ni wa kwanza kurejea miongoni mwa takriban raia 600 wa Nigeria ambao walikuwa tayari kurejea nyumbani baada ya kutokea vurugu ambazo zililenga biashara za raia wa kigeni.

Mmoja kati ya waliorejea, Israel Oluwaseun, alisema: "Nimekutana na mazingira ya vurugu za chuki nchini Afrika Kusini. Nilishawahi kukumbana na hali hiyo mwaka 2014, nilikutana na tukio lingine ambalo halikuwa baya sana, lakini ukiitazama, inakua."

"Si jambo ambalo limerekebishwa, lakini muda wangu nchini Afrika Kusini haukupotea bure, sijutii kuwa Afrika Kusini. Ilikuwa funzo kubwa kwangu...imenifanya kuwa na bidii sana katika kufanya kazi. Kufanya kazi kwa bidii na kufikia malengo niliyojiwekea."

Mwanaume mmoja ambaye alikuwa fundi magari nchini Afrika Kusini, alisema watu waliingia kwenye karakana yake na kuchoma moto eneo lote na kuyachoma magari yote.

Kutokana na vurugu hizo, watu 12 walipoteza maisha lakini kwa mujibu wa serikali ya Afrika Kusini, 10 kati yao ni raia wa Afrika Kusini na hata wengine wawili si raia wa Nigeria.

Rais wa Nigeria, Muhammadu Buhari amepeleka ujumbe wake nchini Afrika Kusini kwa ajili ya kueleza masikitiko kuhusu namna wanavyotendewa raia wake.

Katika taarifa, Ofisi ya Rais iliomba Afrika Kusini kuchukua hatua kukomesha vitendo vya chuki dhidi ya raia wa kigeni kutoka mataifa mengine ya Kiafrika.

Kadri wiki zinavyokwenda, watu wamekuwa wakitumiana video kwa WhatsApp kuonyesha vitendo vya mashamulizi dhidi ya raia wa Nigeria. Lakini video hizo zimekuwa zikidaiwa kupotosha watu.

Raia wa Nigeria 640 walisajiliwa katika ubalozi wa Nigeria nchini Afrika Kusini baada ya kutokea mashambulio dhidi ya raia wa kigeni nchini Afrika Kusini.

Kulingana na taarifa iliyotolewa na Wizara ya Mambo ya Nje ya Nigeria kwenye ukurasa wake wa twitter ilieleza kuwa inakadiriwa kuwa idadi ya raia 313 watachukuliwa kutoka Afrika Kusini katika awamu ya kwanza na waliosalia watasafirishwa leo na kesho.

**BBC**

# Majaliwa aonya watendaji wanaokwamisha wawekezaji

**Na Sanula Athanas, DODOMA**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema mtendaji yeyote wa serikali atakayekwamisha mchakato wa uwekezaji katika eneo lake, atachukuliwa hatua kali za kisheria.

Majaliwa aliyasema hayo bungeni jijini Dodoma jana, alipojibu swali la Mbunge wa Viti Maalum, Jacquiline Msongozi (CCM), wakati wa kipindi cha 'Maswali kwa Waziri Mkuu'.

Mbunge huyo alitaka kauli ya serikali kuhusu changamoto zinazowakabili wawekezaji na hatua zinazochukuliwa dhidi ya watendaji wanaokwamisha uwekezaji nchini.

Waziri Mkuu alisema pamoja na mambo mengine, serikali kupitia ngazi mbalimbali inaendelea kupokea kero katika sekta ya uwekezaji.

Alisema viongozi katika ngazi za mikoa na halmashauri wanatakiwa kupokea wawekezaji wenye nia ya kuwekeza kwenye ngazi hizo na mikoa sasa itawezeshwa kuhakikisha mwekezaji huyo anapata huduma ya uwekezaji na anapata maelekezo sahihi na baadhi ya mambo yanaweza kutolewa uamuzi katika ngazi za chini.

"Lakini (mambo) mengine lazima yaende Kituo cha Uwekezaji (TIC) na mengine lazima yaende wizarani kwa utekelezaji zaidi, kwa hiyo kama yuko mtendaji anakwamisha uwekezaji, huyo atakuwa hana nia njema na nchi yetu.

Waziri Mkuu pia alisema bado serikali inatoa fursa kwa wawekezaji na wamewahusishwa wawekezaji wenyewe.

Alisema kumekuwa na vikao na watu mbalimbali na Rais amekutana na wafanyabiashara na wawekezaji wengi na watendaji wengine na yeye mwenyewe amekutana na makundi hayo kusikia kero zinazoyagusa.

"Na sasa hivi tumeandaa mifumo ambayo inaonyesha mabadiliko ya mifumo mbalimbali ya uwekezaji (Blue Print) ambayo inarahisisha uwekezaji hapa nchini, zaidi na tunaendelea kupokea kero za wawekezaji ili tuendelee kuboresha na ndiyo sababu unaona sasa idadi ya wawekezaji inaongezeka.

Waziri Mkuu pia alizungumzia changamoto zilizojitokeza katika ununuzi wa pamba msimu huu, baada ya Mbunge wa Sumve, Richard Ndassa (CCM), kuhoji kuhusu malipo ya pamba kwa wakulima ambao wameiuza kwa mkopo.

Katika majibu yake, Waziri Mkuu alisema hadi kufikia Jumanne ya wiki hii, ununuzi wa pamba nchini msimu huu ulikuwa umefika asilimia 80.

Alisema tayari tani 285,000 zilikuwa zimeshanunuliwa na kwamba Jumanne walikuwa na kikao na wanunuzi na wadau wa pamba wakiwamo wabunge kuhusu suala hilo.

Alisema serikali itahakikisha pamba yote inanunuliwa kabla ya kuanza kunyesha kwa mvua na kila mkoa wenye pamba umepangiwa wanunuzi ambao wanakopeshwa fedha na benki.




Mkurugenzi wa Jiji la Dodoma, Godwin Kunambi (kulia), akifurahia uzinduzi wa Klabu ya Wafanyabiashara ya Benki ya NBC ya Mkoa wa Dodoma uliofanyika juzi jijini humo. Wengine ni baadhi ya wateja na maofisa wa benki hiyo akiwamo Mkurugenzi wa Idara ya Wateja wa Kati na Wadogo, Elibariki Masuke. **MPIGAPICHA WETU**

# Wagundua kemikali kufukuza mbung'o

**Na Margaret Malisa, TANGA**

WATAFITI kutoka Wakala wa Maabara za Mifugo Tanzania (TVLA) kituo cha Tanga kwa kushirikiana na wa Shirika la Utafiti wa Mifugo na Kilimo Kenya (KARLO) wamegundua kemikali ya kufukuza mbung'o wanaosababisha ugonjwa wa malale kwa binadamu na ndigana kwa wanyama.

Hayo yalibainishwa jana na Ofisa Utafiti wa Mifugo, Deusdedit Malulu, kutoka TVLA kituo cha Tanga, wakati akitoa mada ya utafiti katika mafunzo ya wanahabari na watafiti yaliyoandaliwa na Tume ya Sayansi na Teknolojia yanayoendelea jijini hapa.

Alisema katika kukabiliana na mdudu huyo, wamegundua mnyama aitwaye Kuro ambaye harufu yake inaweza kumfukuza mbung'o kwa asilimia 60 kuliko kemikali zilizoko sokoni.

Kutokana na ugunduzi huo, alisema kwa sasa wako katika hatua ya mwisho kwa kushirikiana na kiwanda cha A To Z kilichoko Arusha, kuzalisha vifaa vitakavyotumika kusambaza kemikali hiyo kitakachofungwa kwenye mnyama na pia kusajili teknolojia hiyo kwenye mamlaka husika.

Alisema ili kuhakikisha teknolojia hiyo inamfikia mfugaji, watafiti wanaandaa kifaa hicho maalum cha kubebea harufu hiyo. "Kifaa hicho kitakuwa kinafanya kazi kumlinda na kung'atwa na mbung'o, kinaweza kufungwa sikioni kwa ng'ombe na kitakuwa kikitoa harufu iliyoko ndani ya kifaa ambayo itasambaa na kufukuza mbung'o," alisema.

Alitaja faida ya kifaa hicho kuwa ni nyingi mojawapo ikiwa ni kumpunguzia mfugaji gharama za kuogesha mifugo na dawa ambazo wakati mwingine zimekuwa zikiripotiwa kusababisha usugu kwa wadudu.

Malulu akawataka wafugaji kuendelea kufuga ng'ombe kwa wingi ili kupata faida kwa kuwa changamoto mbalimbali za magonjwa zinapatiwa ufumbuzi.

Ugonjwa wa malale kwa binadamu na nagana kwa wanyama umeathiri zaidi katika nchi za kusini mwa Jangwa la Sahara na umekuwa na athari kubwa kwa binadamu na mifugo.

## Walimu 16 mbaroni tuhuma kuruhusu mwanafunzi feki mtihani darasa 7

**Na Beatrice Shayo**

WALIMU 16 wa Shule ya Msingi Kenyamanyori, mkoani Mara wamekamatwa na polisi kwa madai ya kuruhusu mwanafunzi feki kufanya mtihani wa kuhitimu darasa la saba.

Awali ilidaiwa kuwa walimu hao walibainika kutokana na taarifa kupelekwa kwa Ofisa wa Elimu Mkoa wa Mara kuwa kuna mwanafunzi feki anafanya mtihani ambao ulianza juzi nchi nzima.

Baada ya taarifa hiyo walimu hao walikamatwa kwa ajili ya mahojiano ya kumruhusu mwanafunzi huyo feki kuingia chumba cha mtihani kinyume cha sheria.

Nipashe ilimtafuta Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mara kuzungumzia tukio hilo, simu yake ilikuwa haipatikani.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Mji wa Tarime, Elias Ntiruhungwa, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo na kueleza walimu hao wamekamatwa na kwamba inaonyesha kuna mchezo ulichezwa.

## Wito wafanyabiashara kuchangamkia fursa

**Na Mwandishi Wetu, DODOMA**

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Bilinith Mahenge. ametoa wito kwa wafanyabishara jijini humo kuhakikisha wanachangamkia fursa za mikopo inayotolewa na taasisi za kifedha ili kunufaika na ongezeko kubwa la fursa za kibiashara zinazoibuka katika jiji hilo ambalo ni makao makuu ya nchi.

Akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa mkoa huyo wakati wa hafla ya jioni ya Uzinduzi wa Klabu ya wafanyabiashara ya Benki ya NBC ya mkoa wa Dodoma, Mkurugenzi wa jiji hilo, Godwin Kunambi, mbali na kuipongeza benki hiyo kwa mabadiliko makubwa ya kihuduma alisema ipo haja ya makusudi kwa wafanyabiashara wa jiji hilo kuitumia vema benki hiyo ili kupata nguvu ya kiuchumi itakayowawesha kufaidi vema fursa ya mabadiliko ya ukuaji wa uchumi katika jiji hilo.

"Dodoma kwa sasa kuna utekelezaji wa miradi mikubwa mingi ikiwamo barabara, stendi ya mabasi ambayo ni kubwa zaidi Afrika Mashariki, upanuzi wa uwanja wa ndege, ujenzi wa viwanja vya mapumziko ambayo vitachochea mzunguko mkubwa wa pesa na ongezeko la watu. Hivyo ni fursa kwa wafanyabiashara kushirikiana vema na benki kama NBC ili kukuza mitaji itayowawezesha kufanya uwekezaji utakaowanufaisha na mabadiliko hayo," alibainisha.

Alitolea mfano umuhimu wa wafanyabiashara hao kuwekeza kwenye sekta ya usafiri ambapo kwa sasa serikali jijini humo ipo kwenye mpango wa kuondoa magari madogo ya abiria maarufu kama 'vipanya' kwenye mizunguko ya mjini ili kutoa fursa kwa gari kubwa 'coaster' kufanya kazi hiyo.

## TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

### VIWANJA / MASHAMBA

**SHAMBA LENYE NYUMBA NDANI LINAUZWA,** Liko eneo la Lumumba Pangani mkoa wa pwani. Lina ukubwa wa heka mbili. Kwa Mawasiliano 0767332830, 0686137871, 0686807366


**NIPASHE NI JIBU LAKO**

NJOO UTANGAZE NASI BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz,

au piga simu: 0767 223311


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

Katika mahakama ya mwanzo
**MJINI MOROGORO**

Usimamizi wa mirathi NO;**175/2019.**

Ombi la **MARIA JOSEPH PIUS** Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu **JOSEPH PIUS NAWAMBWA.**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 03/10/2019 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 09/09/2019.

215416001

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA MAMBO YA NDANI**
**IDARA YA UHAMIAJI**

**MAOMBI YA URAIA**



**ALBINA NALIAKA BARASA** mwenye picha hapo juu anaomba uraia wa Tanzania kwa Mh. Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi. Utaifa wake wa sasa ni MKENYA. Nchi atokayo ni KENYA. Yupo hapa nchini tangu 1970. Kwa yeyote mwenye taarifa/sababu za kwanini mwombaji asipewe Uraia wa Tanzania, atume taarifa ya maandishi kwa Kamishna Jenerali wa Uhamiaji S.L.P 512, Dar es salaam. Kumb. Na. DN. 203824.

115417401

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA**
**KAGERA LILILOPO BUKOBA**
**MAOMBI NA: 177/2019**

**IDDI RWIZA ........................MDAI**
**DHIDI YA**
**EDWARD DAUDI ....................MDAIWA**

**KWA: EDWARD DAUDI**
**(POPOTE PALE MLIPO)**
Mnaarifiwa/ unaarifiwa kuwa Maombi Na: 177/2019 yamepangwa kutajwa tarehe 10.10.2019 mbele ya mwenyekiti wa baraza , E. MOGASA saa 2:00 asubuhi.

Hivyo, unaamuriwa kuhudhuria wewe mwenyewe/ mwakilishi wako mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa. Usipohudhuria Baraza litasikiliza shauri upande mmoja dhidi yako na hukumu kutolewa.

AMRI hii imetolewa kwa mkono wangu na MUHURI wa baraza hili leo tarehe 22.08.2019

115417602

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KTK MAHAKAMA YA MWANZO MJINI**
**ILIYOPO MOROGORO**

**TANGAZO LA KUITWA SHAURINI**

**SHAURI LA MADAI NAMBA: 215/2019**

**Mdai:............................. CHARLES DISMAS KATANZI**

**DHIDI YA**

**Mdaiwa: .......................... BARAKA ISAAC CHALLE**

**Kwa: BARAKA ISAAC CHALLE**
**WA KAYENZI-VIWANDANI**
**MOROGORO**

**Ombi la Mdai: ....CHARLES DISMAS KATANZI**
**Madai ya: PESA SHILINGI 7,760,000/=**
Unatakiwa kuudhuria hapa mahakamani ktk shauri tajwa hapo juu bila kukosa.Shauri limepangwa kusikilizwa mnamo tarehe 13 mwezi 09 mwaka 2019 saa 02:30 Asubuhi.
Angalia kama hukuudhuria/hamkuudhuria siku iliyotajwa hapo juu.Mahakama ikidhibitisha kama umepokea/mmepokea kuitwa shaurini,hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa /mmeshindwa.
Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakama hii leo tarehe 11 mwezi 09 mwaka 2019.

115416302

**KUPOTELEWA NA KADI YA GARI**

**HUMUDI ALLY SALUM** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 432 ANG TOYOTA CARINA.** Chassis namba **19140007257.** Engine namba **7A.FE 1762.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **KJN/RB/7972/2018.**

115415802



**NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO**

**KWA BEI NAFUU SANA**

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz

au piga Simu: 0767 223 311


**KUPOTEA KWA CHETI**



**MAHAMUDU H MKAKILE** amepotelewa na Cheti cha elimu ya kidato cha nne alichosomea ktk shule ya Secondari TUKUYU,Alichomaliza mwaka 2015 na chenye index namba **S1043-0173.** Kwa yeyote atakae kiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi,Taarifa ya polisi; **MOR/MOR/RB/282979/2019.**

115416202

Nipashe MWANGA WA JAMII

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P 2888,
40470 DODOMA,

12/09/2019

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya JUMAMOSI tarehe 14/09/2019 kampuni ya **FAMARI INVESTMENT** itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **DAR ES SALAAM** kuelekea **TUNDUMA.** Gari lenye namba za usajili

   **T 374 DLQ/ T 446 DQY**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

   Urefu - mita 5.45
   Upana - mita 3.40
   Kimo - mita 21

3. Njia itakayotumika: **KURASINI hadi TUNDUMA** kupitia **VIGWAZA-MAKAMBAKO**

   Gari litasafiri muda wa mchana tu (kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12.00 jioni)

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.**

2154116502

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P 2888,
40470 DODOMA,

12/09/2019

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya **JUMAMOSI** tarehe **14/09/2019** kampuni ya **FAMARI INVESTMENT** itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **DAR ES SALAAM** kuelekea **TUNDUMA**. Gari lenye namba za usajili

   **T 476 DQE/ T 412 DQY**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

   Urefu - mita 5.45
   Upana - mita 3.40
   Kimo - mita 21

3. Njia itakayotumika: **KURASINI hadi TUNDUMA** kupitia **VIGWAZA-MAKAMBAKO**
   Gari litasafiri muda wa mchana tu **(kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12.00 jioni)**

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.**

2154116502


**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku

Tupigie
0767 223 311

Nipashe MWANGA WA JAMII



TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.




# UMTITI
## AKATAA KUMFUATA LACAZETTE

**BARCELONA, Hispania**

SAMUEL Umtiti amemjibu rafiki yake, Alexandre Lacazette, kuwa hataweza kucheza naye katika klabu ya Arsenal.

Umtiti na Lacazette ni marafiki na Juni walikwenda likizo pamoja huko Miami nchini Marekani - jambo ambalo liliibua uvumi mwingi kwamba beki huyo wa Barcelona alikuwa akijiangaa kutua Arsenal, kwa sababu kwa wakati husika kocha Unai Emery alikuwa akisaka beki wa kati wa kiwango bora.

Lakini juzi tu, wakiwasiliana kupitia Twitter, Lacazette alimtumia video Umtiti akimwambia anamsubiri huko Emirates.

Arsenal ilihusishwa na Umtiti katika kipindi chote cha uhamisho wa majira ya kiangazi, ambapo ilikuwa ikisaka beki wa kati wa kiwango cha dunia ili kuimarisha safu yake ya ulinzi.

Lacazette mwenye umri wa miaka 28, ambaye alijiunga na Arsenal mwaka 2017, alimwambia swahiba wake huyo "nakusubiri".

Lakini, Umtiti, ambaye hakuwamo kwenye kikosi cha Ufaransa kilichoichapa Albania magoli 4-1 kwenye mchezo wa kufuzu mashindano ya Euro 2020, huku akiwa amekosa pia mechi zote tatu za kwanza za Barcelona ilizocheza kwenye La Liga msimu huu, alimjibu rafiki yake huyo jibu la kwanza hawezi kwenda Arsenal.

## WENGER: SALAH NI BORA, LAKINI MCHOYO

**LONDON, England**

KOCHA wa zamani wa Arsenal, Arsene Wenger, amesema nyota wa kimataifa wa Misri, Mohamed Salah anaweza kuwa bora kama Lionel Messi, lakini anatakiwa kupunguza uchoyo.

Wenger ambaye alikuwa akiripotiwa kwamba yuko mbioni kurejea kwenye majukumu yake ya ukocha, anaamini Salah ana uwezo wa kufananishwa na Messi, lakini kuna vitu vichache anatakiwa kuvifanyia kazi.

Kocha huyo, alisema Salah anatakiwa kutofautisha muda ambao anapaswa kulazimisha kufunga na ule ambao atalazimisha kuingia kwenye ngome ya wapinzani kwa lengo la kutoa usaidizi kwa mchezaji ambaye yupo kwenye eneo zuri zaidi.

"Ana uwezo mzuri wa kufunga. Navutiwa na uwezo wake kwa sababu ni mchezaji mzuri, anatakiwa kulifanyia kazi suala la kucheza kitimu kwa kutoa 'asisti' muda mwingine kwa wengine," alisema Wenger akinukuliwa na gazeti la Daily Mail.

Katika ushindi wa mabao 3-0 ambao Liverpool waliupata dhidi ya Burnley, Salah alipondwa baada ya kushindwa kumpasia Sadio Mane kipindi cha pili wakati mchezaji huyo alipokuwa kwenye eneo zuri zaidi la kufunga.



Mane alionyesha wazi kukerwa na kitendo cha Salah kumnyima pasi.

## RONALDO AZISHINDA KLABU KWA MSHAHARA MKUBWA

**TURIN, Italia**

CRISTIANO Ronaldo ndiye anayeongoza kwa kulipwa mshahara mkubwa zaidi ya wachezaji wote wa Ligi Kuu Italia, Serie A.

Ronaldo analipwa mshahara wa pauni milioni 28 kwa mwaka pale Juventus ukiwa ni mara tatu ya wachezaji wengine wanaomfuatia kwa kulipwa huko kwenye Serie A, huku akizifunika klabu zaidi ya nne kwenye bili yao ya mishahara kwa mwaka.


Nyota huyo wa Ureno mwenye umri wa miaka 34, kwa msimu mmoja analipwa fedha nyingi kushinda klabu kadhaa kwenye Serie A mishahara yao yote inayowalipa wachezaji wao ndani ya mwaka.

Mshahara wa Ronaldo ni zaidi ya bili za mishahara za klabu za SPAL, Udinese, Brescia na Verona kwenye mishahara yao, zinazowalipa wachezaji wao wote ndani ya mwaka.

Juventus iliinasa huduma ya Ronaldo kutoka Real Madrid mwaka jana kwa ada ya pauni milioni 99.

Hata hivyo, kwenye orodha ya mishahara mikubwa Serie A, Juve ndio inayolipa kiasi kikubwa zaidi.

**Kwenye 10 bora, Romelu Lukaku ndiye mchezaji pekee asiyekuwa wa Juventus, aliyeingia kwenye orodha hiyo akilipwa mshahara wa pauni milioni 6.7 kwa mwaka, akishika namba tatu kwa kulipwa fedha nyingi, akilingana na Gonzalo Higuain, ambapo mishahara yao ni kama theluthi moja tu ya kile anachokivuna Ronaldo kwa msimu**





# GORETZKA AIPA PIGO BAYERN

**MUNICH, Ujerumani**

KLABU ya Bayern Munich itaingia uwanjani wikendi hii kucheza dhidi ya wapinzani wao katika kilele cha msimamo wa Bundesliga RB Leipzig, bila ya kiungo wa Leon Goretzka.

Goretzka mwenye umri wa miaka 24, alipatwa na majeraha ya paja la mguu wa kushoto akiwa katika mazoezi ya kikosi cha Timu ya Taifa ya Ujerumani juma lililopita, na tayari imeshaelezwa atafanyiwa upasuaji mdogo.

Kocha wa mabingwa hao wa Bundesliga, Niko Kovac, amesema anatambua ugumu wa kukosekana kwa kiungo huyo, lakini atajitahidi kuziba pengo lake, ili kufanikisha mikakati ya ushindi ndani ya dakika 90 dhidi ya RB Leipzig.

"Goretzka alikuwa na umuhimu mkubwa kuelekea mchezo wetu wa mwishoni mwa juma hili, lakini sina budi kukubaliana na hali halisi, nitafanya kila linalowezekana ili kuziba kikamilifu pengo lake." Amesema Kovac alipozungumza na waandishi wa habari.

Bayern wanashika nafasi ya pili katika msimamo wa Ligi ya Bundesliga, baada ya kulazimishwa sare ya mabao 2-2 dhidi ya Hertha Berlin majuma mawili yaliyopita.

Bayern Munich walifikisha alama saba, huku RB Leipzig, wakijitanua kileleni kwa kumiliki alama tisa, zilizotokana na ushindi wa michezo mitatu iliyochezwa tangu kuanza kwa mshike mshike wa ligi hiyo msimu huu wa 2019/20.

Matokeo ya mchezo wa mahasimu hao utatoa picha kamili, kama RB Leipzig wataendelea kuongoza msimamo wa ligi, ama kuwapisha mabingwa watetezi kukaa kileleni.

## Adidas yatajwa kumzuia Pogba kutua Madrid

**MANCHESTER, England**

IMEFICHUKA kwamba, kampuni ya vifaa vya michezo ya Adidas ndio iliyoingilia kati na kuzuia uhamisho wa staa wa kimataifa wa Ufaransa, Paul Pogba kutoka Manchester United kwenda Real Madrid katika dirisha kubwa lililopita.

Adidas ina mkataba na Manchester United pamoja na kiungo huyo na ilifanya kikao cha amani baina yao baada ya staa huyo kutangaza kuondoka klabuni hapo wakati akiwa katika ziara yake ya kibiashara kule Japan.


Nyota huyo wa kimataifa wa Ufaransa alisema alihitaji kupata changamoto nyingine nje ya Manchester United.

Pogba ameanza mechi zote nne za United msimu huu na amepika mabao mawili lakini bado anatazamiwa kuondoka Old Trafford mwishoni mwa msimu, huku Madrid pia ikiwa imepania kumtwaa staa huyo.

Inadaiwa Kocha wa Real Madrid, Zinedine Zidane ndiye aliyekuwa chachu ya Mfaransa mwenzake huyo kutaka kutua Santiago Bernabeu.



# MESSI: NATAKA SANA NEYMAR ARUDI BARCELONA



**BARCELONA, Hispania**

LIONEL Messi amesisitiza kuwa hakuumizwa na kitendo cha klabu ya Barcelona ya kushindwa kumrejesha nyumbani, Neymar msimu huu.

Neymar alicheza kwa mafanikio zaidi na Messi na Luis Suarez na kuunda utatu, uitwao MSN ndani ya Camp Nou uliotikisa soka la Ulaya.

Utatu huo, ulimudu pamoja kuiongoza Barcelona kwenye idara yao ya ushambuliaji na kutwaa makombe mawili ya Ligi Kuu Hispania 'La Liga' ndani ya miaka yao mitatu huku pia wakibeba Copa del Rey na Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu wa 2014-15.

Muunganiko wao, ulivunjika mwaka 2017 wakati Neymar alipoamua kuondoka Camp Nou kwa kujiunga na Paris Saint-Germain kwa rekodi ya Euro milioni 222.

Hata hivyo, majira haya ya joto iliripotiwa kuwa nyota huyo wa Brazil alikuwa tayari kuondoka pale Parc des Princes kwa kurejea Hispania, lakini ilishindikana kutokana na FC Barcelona na PSG kushindwa kufikia makubaliano katika mchakato wa uhamisho.

"Nilipenda kuona Neymar anarejea. Binafsi, sijui kama Barca walifanya kila linalowezekana kumfanya akarejea, lakini nafahamu kuwashawishi PSG wamwachie sio jambo jepesi," alisema Messi.

Aliongeza kusema: "Bado natamani Neymar arudi hapa Barcelona, na hilo ni suala la klabu, lakini naamini anaweza kurudi tena hapa."

## HABARI MICHEZO

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# ZIDANE AJIPANGA KUMSAJILI KANTE

Kiungo huyo Mfaransa atajwa kuwa kwenye orodha ya nyota wanaotakiwa...

**MADRID, Hispania**

KIUNGO wa Chelsea, N'Golo Kante, ametajwa katika orodha ya nyota wanaotakiwa na Kocha Zinedine Zidane katika kikosi cha Real Madrid kwenye kipindi cha usajili cha majira ya joto mwakani.

Zidane ameweka wazi anahitaji kusajili viungo wenye ubora ili kuimarisha kikosi chake, kwa lengo la kufanya vema kwenye mashindano yote watakayoshiriki.

Klabu hiyo maarufu The Blues tayari imekubali kuzidiwa nguvu na Real kwa misimu miwili iliyopita, mwaka jana ikichukuliwa golikipa wake Thibaut Courtois na pia imempoteza mshambuliaji Eden Hazard ambaye alitua Hispania mapema katika kipindi cha majira ya joto mwaka huu.

Lakini kwa mujibu wa taarifa kutoka katika klabu ya Athletic, vigogo hao wa Hispania wanaelezwa wako tayari kurejea kutoa ofa nyingine kwa Chelsea ili kumsajili kiungo huyo wa Timu ya Taifa ya Ufaransa ambaye anauwezo wa kucheza katika kiwango cha juu kwa muda wote bila kuchoka ifikapo mwisho wa msimu huu.

Kwa muda mrefu, Madrid imekuwa ikimtaja kiungo wa Manchester United Mfaransa Paul Pogba kwamba ndiye mtu sahihi katika kuboresha idara yake ya kiungo, lakini imeonekana wazi kwamba mchakato wa kumsajili nyota huyo umekwama, licha ya mchezaji huyo kuonyesha yuko tayari kuondoka Old Trafford.

Pogba na Kante ni wachezaji ambao wanaweza kutengeneza pacha ngumu lakini inafahamika kwamba ni moja ya wachezaji ambao wanaweza kumalizia vema na uwezo huo unatambulika duniani.

Kwa sababu hiyo, ndiyo maana Kante alijumuishwa katika kikosi cha wachezaji 55 cha FIFPRO World XI ambacho kilitangazwa wiki iliyopita.

Ni mchezaji pekee wa Chelsea aliyemo kwenye kikosi hicho cha wachezaji mahiri duniani.

Mapema katika kipindi cha majira ya joto msimu huu, Kante aliweka wazi kwa kifupi kwamba alikuwa na mazungumzo na moja ya klabu kubwa ya Ulaya ambayo ilitaka kumsajili.

Kante alisema: 'Ni heshima sana kutakiwa na klabu kubwa, inapofika wakati makocha wanaonyesha nia ya kukuhitaji, hiyo ni ishara kwamba kiwango chako kiko kwenye ubora wa juu. Lakini ninafuraha na uamuzi nilioufanya wa kuwa hapa Chelsea. Ninampango wa kuendelea kuwa katika klabu hii ya Chelsea kwa msimu mwingine ujao."

## KWA UFUPI

**DYBALA KUTUA SPURS**

TOTTENHAM inajipanga kumtoa kiungo wa Timu ya Taifa ya Denmark, Christian Eriksen (27), kwa Juventus ili kumpata mshambuliaji wa Argentina, Paulo Dybala (25), katika dirisha la usajili la Januari litakapofunguliwa. ***(Tuttosport, via Express)***

**NEYMAR ALIMKWAMISHA POGBA**

KIUNGO wa Manchester United, Paul Pogba (26), alikuwa amekubali kulipwa mshahara wa pauni 429,000 kwa wiki akijiunga na Paris St-Germain kabla ya dirisha la usajili halijafungwa, lakini mchakato huo ulikwama kwa sababu Neymar alishindwa kukamilisha uhamisho wake wa kurejea Barcelona. ***(Calciomercato, via Sun)***

**FERNANDES RASMI SOKONI**

NYOTA anayetakiwa na Tottenham, Bruno Fernandes (25) wa Sporting Lisbon anaweza kuuzwa na klabu yake hiyo ambayo imesema itakuwa tayari kumtoa kwa dau la pauni milioni 62. ***(A Bola, via Sport Witness)***

**UKWELI KUHUSU ZAHA**

KOCHA wa Crystal Palace, Roy Hodgson, amesema kuwa hakuna ofa yoyote iliyowasilishwa kwa ajili ya winga wa Timu ya Taifa ya Ivory Coast, Wilfried Zaha (26), kutoka kwa klabu mbalimbali zilizokuwa zimeonyesha nia ya kutaka huduma yake katika kipindi cha majira ya joto. Nyota huyo aliiambia klabu yake anataka kuvunja mkataba baada ya kushindwa kuondoka klabuni hapo. ***(Mirror)***

**WENGER ALIMHITAJI SANCHO**

KOCHA wa zamani wa Arsenal, Arsene Wenger, ameweka wazi kuwa alijaribu kufanya mchakato wa kumsajili winga wa Timu ya Taifa ya England, Jadon Sancho (19), wakati alipokuwa akiichezea Manchester City, kabla ya kuelekea Borussia Dortmund. ***(Express)***

**SANCHO ALIIKATAA UNITED**

MKURUGENZI wa Michezo wa Dortmund, Michael Zorc, amekiri katika mahojiano maalumu kwamba kulikuwapo na mchakato wa uhamisho wa winga, Jadon Sancho kuelekea kwa Manchester United lakini nyota huyo wa England hakuwa na nia ya kuondoka kwenye klabu hiyo inayoshiriki Ligi ya Bundesliga. ***(Mirror)***

**UNITED KUONGEZA KIUNGO**

MANCHESTER United inatarajia kumpa baraka kocha wake, Ole Gunnar Solskjaer, ya kusajili kiungo katika dirisha dogo la Januari, baada ya bodi ya klabu hiyo kuwa tayari kutoa fungu la fedha katikati ya usajili ili kuimarisha kikosi chake. ***(Manchester Evening News)***

**MOSES HAKIJAELEWEKA**

WINGA wa Chelsea, Victor Moses (28), ameonyesha kutofurahia mchakato wake wa mkataba wake wa mkopo na Fenerbahce kubadilika na kuwa wa kudumu, licha ya klabu hiyo ya Uturuki kuwa na kipengele kinachowaruhusu kumsajili moja kwa moja Mnigeria huyo. ***(Star)***

**SINCLAIR AMFAGILIA STERLING**

WINGA wa zamani wa Timu ya Taifa ya England, Trevor Sinclair, amesema kuwa kiwango cha sasa cha mshambuliaji wa Manchester City, Raheem Sterling, ni kizuri kama alivyo Lionel Messi na Cristiano Ronaldo. ***(Talksport)***

**WILLIAMS: UNITED WALINIHITAJI**

MSHAMBULIAJI wa Timu ya Taifa ya Hispania, Inaki Williams (25), ameweka wazi kwamba alikuwa na mazungumzo na Manchester United kabla ya kufikia makubaliano ya kusaini mkataba wa mpya wa kuendelea kuitumikia Athletic Bilbao. ***(Cadena Ser, via Independent)***

**CITY, UEFA MAMBO BADO**

UAMUZI wa kesi kati ya Shirikisho la Soka Ulaya (Uefa), kuhusiana na matumizi mabaya ya fedha dhidi ya klabu ya Manchester City utajulikana ikifika mwisho wa msimu. ***(Times - subscription required)***

**EVERTON WALIIGOMEA DORTMUND**

MABOSI wa Everton walikataa ofa kutoka kwa Borussia Dortmund ambayo ilikuwa inahitaji saini ya kiungo mshambuliaji, Anthony Gordon (18), katika kipindi cha majira ya joto. Nyota huyo anaichezea pia Timu ya Taifa ya vijana wa umri chini ya miaka 19 ya England (U-19). ***(Football Insider)***

## HABARI MICHEZO

# WANARIADHA WATANZANIA KUCHUANA SAUZI JUMAPILI

**Na Moshi Lusonzo**

WANARIADHA wanaochipukia, Jamila Abdullah na Lister Pakua, wanatarajia kuondoka jijini Dar es Salaam leo na kuelekea Afrika Kusini kwa ajili ya kushiriki mbio za kimataifa za Cape Town Marathon ambazo zinatarajiwa kufanyika kesho kutwa nchini humo.

Nyota hao waliagwa rasmi jana na kukabidhiwa tiketi za safari hiyo na Ofisa Mtendaji wa Kampuni ya Bima ya Sanlam, Khamis Suleiman, ambaye kampuni yake imedhamini wanamichezo hao.

Akizungumza jana jijini, Suleiman, alisema kuwa anawapongeza wanariadha hao kwa kupata nafasi ya kwenda kushiriki mbio hizo na anaamini wataiwakilisha vema nchi katika mashindano hayo.

Suleiman alisema kuwa anaamini walifanya maandalizi mazuri kuelekea mbio hizo ili watakapokuwa huko, wafanye vizuri na hatimaye kulitangaza vema jina la Tanzania.

"Kampuni yetu haikukosea kuwadhamini kwenda kushiriki katika mbio hizi za kimataifa, nina matumaini makubwa kuwa mtaipeperusha vizuri bendera ya Tanzania kwa kushika nafasi muhimu za juu, tunaamini pia mlijiandaa vizuri kwenda kushindana, " alisema Suleiman.

Kwa upande wa balozi wa Sanlam, mtangazaji maarufu nchini, Maulid Kitenge, aliishukuru kampuni hiyo kwa kukubali kuwadhamini wanamichezo hao na kueleza kwamba wakiwa nchini humo wanatarajia wataonyesha ushindani kutokana na kujiandaa vema kurejea na medali.

"Tunawaamini wawakilishi wetu, wamefanya mazoezi ya kutosha kwa sababu wamejiandaa kwenda kushindana, pia naweza kuwahakikishia wadau kwamba wanariadha hawa wana ari kubwa ya kufanya vizuri," alisema Kitenge.

Wanariadha hao wanatarajiwa kuambatana na wadau wengine wa mbio hizo ambao ni pamoja na Stephen Mndeme, Innocent Shaku na Kitenge.

Washiriki hao walipata nafasi ya kwenda kupeperusha bendera ya Tanzania katika mbio hizo baada ya kufanya vema katika mbio maalum za kutafuta wanariadha wenye vipaji yanayojulikana kwa jina la "Life Marathon' yaliyofanyika Agosti 6 mwaka huu kwa kushirikisha nyota kutoka klabu mbalimbali za riadha hapa nchini.

# Ndayiragije ajipanga kuimaliza Triangle

**Na Faustine Feliciane**

WAKATI joto la pambano la kimataifa la Kombe la Shirikisho Afrika kati ya Azam na Triangle United ya Zimbabwe likizidi kupanda, Kocha Mkuu wa 'Wanalambalamba' hao, Etienne Ndayiragije, amesema ana uhakika kikosi chake 'kitawafumua' wapinzani wao na kusonga mbele katika mashindano hayo.

Ndayiragije alisema kuwa maandalizi kuelekea mechi hiyo yamekamilika na kikosi chake hakina sababu ya kupoteza mchezo huo wa nyumbani.

"Ni lazima tupambane tupate ushindi nyumbani... kuna faida ya kucheza nyumbani, na lazima tuitumie hii nafasi kama kweli tunataka kusonga mbele," alisema Ndayiragije.

Kocha huyo alisema pia amewafuatilia wapinzani wao na tayari amewaandaa vema wachezaji wake kukabiliana na changamoto kutoka kwa wageni hao.

"Kabla hatujaufikiria mchezo wa marudiano, ni lazima kwanza tufanye kazi kubwa hapa nyumbani kwa kuhakikisha tunapata ushindi, tena ushindi mkubwa utakaoturahisishia kazi kwenye mchezo wa marudiano," Ndayiragije alisema.

Azam FC wanatarajia kuwakaribisha Triangle United keshokutwa kwenye Uwanja wa Azam Complex na timu hizo zinatarajia kurudiana baada ya wiki mbili jijini Harare na mshindi wa jumla atakuwa amefuzu hatua ya makundi ya michuano hiyo.



Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Harrison Mwakyembe, akisalimiana na Sarah Kimario, mmoja wa wahitimu wa Akademi ya Filamu ya MultiChoice kwenye Viwanja vya Bunge jijini Dodoma jana. Kushoto ni Mkuu wa Uhusiano wa MultiChoice Tanzania, Johnson Mshana, Jane Moshi, Jamal Mohamed na Wilson Nkya. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mwakyembe awafunda wahitimu wa filamu

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Harrison Mwakyembe, amewataka wanafunzi waliohitimu mafunzo maalum ya uzalishaji filamu kutumia vema elimu waliyoipata ili kuandaa vizuri kazi zao, imefahamika.

Wanafunzi hao wamepata mafunzo hayo chini ya programu ya kuendeleza vipaji inayosimamiwa na MultiChoice Talent Factory ambao walihudhuria kikao cha Bunge la Tanzania kama wageni maalum wa Wizara ya Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo.

Mwakyembe aliwaambia wahitimu hao kuwa wakitumia vema mafunzo waliyopata, watakuwa katika nafasi nzuri ya kufanya vema kwenye soko la filamu hapa nchini.

Pia kiongozi huyo aliwakumbusha wahitimu hao kutumia mafunzo maalum waliyoyapata katika kuleta mapinduzi ya tasnia ya filamu hapa Tanzania.

Katika ziara hiyo, wanafunzi hao pia walikutana na wadau mbalimbali wa sanaa, akiwamo Naibu Spika, Dk. Tulia Apson, Naibu Waziri wa Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Juliana Shonza na Naibu Waziri wa Kazi, Vijana, Ajira, Anthony Mavunde.

Shonza aliwaeleza kuwa tasnia ya filamu ni moja ya tasnia zinazokuwa kwa haraka hapa nchini, hivyo ni muhimu wanatasnia wawe na mafunzo ya kutosha na yanayoendana na wakati ili iweze kupambana na nchi nyingine katika soko la filamu.

Naye Katibu Mkuu wa Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Suzan Mlawi, amesisitiza kuwa serikali inaahidi kuendelea kushirikiana na wadau wa tasnia mbalimbali ili kuharakisha ukuaji wa tasnia hizo.

Mlawi alisema kuwa ushirikiano kati ya serikali na wadau ni muhimu na kwamba wamejipanga kuendelea kuhakikisha sera na kanuni zinaboreshwa ili kuakisi hali halisi ya ukuaji wa tasnia ya filamu.

Awamu ya pili ya programu hiyo ya mafunzo inatarajiwa kufanyika mapema mwezi ujao kwa kushirikisha wanafunzi wengine 60.

# Ruvuma Marathon kufanyika Oktoba

**Na Gideon Mwakanosya, SONGEA**

WAKAZI wa mkoa wa Ruvuma wametakiwa kuupa umuhimu na thamani mchezo wa riadha kwa lengo la kuimarisha afya zao badala ya kuuchukulia kuwa ni sawa na adhabu.

Ushauri huo, ulitolewa jana na Mkuu wa Ruvuma, Christina Mndeme, wakati wa uzinduzi wa Tamasha la Riadha la Kunyumba Marathon linalotarajiwa kufanyika Oktoba 26, mwaka huu kwa kushirikisha wanariadha zaidi ya 200 kutoka mikoa mbalimbali hapa nchini.

Mndeme alisema kuwa mbio hizo zinatarajiwa kutoa fursa nyingi kwa vijana kwa kuwaunganisha pamoja ili waweze kuboresha zaidi mchezo huo na wabadili mawazo kwa kuutambua kutokana na kusaidia kujenga afya zao na kuwafanya waache kushinda kwenye vijiwe.

Kiongozi huyo aliwataka wananchi wa mkoa huo kujitokeza kwa wingi kushiriki mbio hizo ambazo naye anatarajia kuwaongoza katika umbali wa kilomita 10.

Naye Mratibu wa mbio hizo, ambaye ni Mkurugenzi wa Vayo Events, Violet Kiyanya, alisema kuwa kampuni yake imeandaa tamasha hilo kwa lengo la kuanzisha maonyesho mengine ya michezo, utamaduni, utalii na shughuli nyingine za jamii ya wananchi wa mkoa huo.


Kiyanya alisema kuwa madhumuni makuu ya mashindano hayo ya Kunyumba Marathon ni kukuza utalii, kuinua vipaji na kuimarisha afya za wakazi wa mkoa wa Ruvuma, pamoja na kuwakutanisha vijana na wadau ili kupanga mipango ya kuijenga Tanzania ya Viwanda.

Naye Katibu Mkuu wa Chama cha Riadha Mkoa wa Ruvuma, Faustine Mhagama, alisema kuwa wamefarijika kuona wadhamini mbalimbali wamejitokeza kuendesha mbio hizo ambazo zitasaidia kuendeleza mchezo wa riadha katika mkoa wao.

# Michezo

Ijumaa Septemba 13, 2019

Nipashe

## Zidane ajipanga kumsajili Kante

HABARI UK 30



Mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya England, Raheem Sterling, akijaribu kumtoka golikipa wa Kosovo, Arijanet Muric katika mechi ya kuwania kufuzu Euro 2020 iliyochezwa mapema wiki hii. England ilishinda mabao 5-3. **PICHA: MTANDAO**

# SIMBA, MTIBWA HAPATOSHI BARA

Kila upande watamba kufanya kweli katika mchezo huo wa raundi ya ...

**Na Somoe Ng'itu**

MBIO za kuwania ufalme wa soka nchini zinatarajiwa kuendelea tena kwa mabingwa watetezi, Simba kuwakaribisha Mtibwa Sugar katika mchezo wa raundi ya pili wa Ligi Kuu Tanzania Bara utakaochezwa leo kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam.

Simba ilianza ligi hiyo kwa ushindi wa mabao 3-1 dhidi ya "Maafande" wa JKT Tanzania wakati Mtibwa Sugar yenyewe ilichapwa idadi kama hiyo ya magoli na wenyeji wao Lipuli FC ya Iringa.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Simba, Patrick Aussems, alisema kuwa mechi hiyo ni ngumu kwa kila timu, lakini kikosi chake kiko imara kupambana ili wapate matokeo mazuri.

Aussems alisema kuwa wachezaji wake wanafahamu ushindi katika mchezo wa leo, utawaweka katika nafasi nzuri ya kutimiza malengo yao ya kupata matokeo bora zaidi ya msimu uliomalizika.

Mbelgiji huyo ambaye msimu uliopita aliifikisha Simba katika hatua ya robo fainali ya mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika, alisema pia amewataka wachezaji wake kutowadharau wapinzani wao na kutofikiria matokeo yoyote ya mechi zilizopita.

**"Tunajua kuwa hii ni ligi, tunahitaji kupata ushindi katika mechi zote na hasa hizi 10 za kwanza, hii itatuweka kwenye nafasi nzuri, kila timu inahitaji kukaa kwenye nafasi ya juu na ukifanikiwa kukaa hapo ni vema ukajiimarisha ili usiondolewe, tunahitaji kuwa mahali hapo," alisema Aussems.**

Naye Kocha Mkuu wa Mtibwa Sugar, Zuberi Katwila, aliliambia gazeti hili kuwa wachezaji wake wako tayari kwa ajili ya mchezo huo, na wamejipanga kulipiza "kisasi" cha kufungwa na Simba ambacho walikipata katika michezo miwili ya ligi hiyo msimu uliopita.

"Tuko katika hali nzuri, jeshi langu lipo sawa sawa na tayari kuvaana na Simba hapo kesho (leo), kwa kifupi timu na wachezaji wote wanajuana, hakuna mabadiliko makubwa yaliyofanywa, wachezaji ni wale wale," alisema Katwila.

Kocha huyo alisema kuwa kikosi chake kilitarajia kuwasili jijini jana jioni ili kukamilisha maandalizi ya mchezo huo na amewataka mashabiki wao wajitokeze kwa wingi kuwashangilia na kutokuwa na wasiwasi wa aina yoyote.

Ligi hiyo inatarajia kuendelea tena kesho kwa Namungo FC kuwakaribisha Singida United kwenye Uwanja wa Kassim Majaliwa ulioko mkoani Lindi, wakati JKT Tanzania itacheza dhidi ya Lipuli FC hapa Dar es Salaam na Mbao FC itavaana na Biashara United kwenye Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza.

## Shikalo aongeza mzuka Yanga

**Na Faustine Feliciane**

MAMBO yamenoga! Uamuzi wa Kocha Mkuu wa Yanga, Mwinyi Zahera, kuweka wazi kuwa atamtumia golikipa wa kimataifa wa timu hiyo, Farouk Shikalo katika mchezo wa Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Zesco United utakaochezwa kesho, kumekifanya kikosi chake kuonekana kuwa imara zaidi.

Shikalo alishindwa kuidakia Yanga katika mechi mbili za kimataifa zilizopita dhidi ya Township Rollers, kutokana na hati yake ya uhamisho ya kimataifa (ITC), kuchelewa kupatikana.

Akizungumza na gazeti hili jana, Zahera, alisema kuwa kupatikana kwa ITC hiyo kumeongeza matumaini ya kufanya vema katika mchezo huo wa kesho, ambao wanahitaji kupata ushindi ili kujiweka kwenye nafasi nzuri ya kusonga mbele katika mashindano hayo.

"Nafurahi ITC ya Farouk imefika, sasa anaweza kucheza dhidi ya Zesco, ni golikipa mzuri na niliyekuwa ninamwihitaji kwenye michezo hii ya kimataifa," alisema Zahera.

Hata hivyo, Zahera hakuwa tayari kuweka wazi kama atamtumia au hatomtumia gokilipa huyo katika mchezo huo wa kesho, huku akiongeza kwamba sasa wanasubiri ITC ya mshambuliaji wao, David Molinga.

## Azam yamwaga mamilioni Stars

**Na Shufaa Lyimo**

SHIRIKISHO la Soka Tanzania (TFF), limesaini mkataba wa miaka minne na Kampuni ya Azam Media kwa ajili ya kuidhamini Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), wenye thamani ya Sh. milioni 400.

Mkurugenzi wa Michezo wa AzamTV, Patrick Kahemele, alisema kuwa Taifa Stars itakuwa ikipata kiasi cha Sh. milioni 35 kila inapocheza mechi na kwa mwaka kampuni yake inatarajia kutumia Sh. milioni 100.

Kahemele alisema pia kampuni hiyo imesaini mkataba mpya wa kuendelea kuidhamini Ligi Kuu Tanzania Bara kwa muda wa miaka minne ambao una thamani ya Sh. bilioni 4.5.

Rais wa TFF, Wallace Karia, alisema mkataba huo utaleta maendeleo makubwa ya mchezo huo hapa nchini na shirikisho hilo litahakikisha linalinda haki za mikataba ya wadhamini wake wote.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >